# Nipashe

Jumanne Machi 5, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579857

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Kabudi awatumia salamu 'wanaoichafua' nchi nje

UKURASA 2


Nipashe
TESA
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI
JE, WAJUA? MAHARAGE YA NYAMA KUTOKA KWA WATURUKI
Miradi mipya yabadili upepo wa elimu wilayani Simanjiro
Wanafunzi Ngurdoto walipolipuka kufurahia ugeni wa umeme Sola

UKURASA 13

# JPM aibua hoja mpya kutekwa kwa MO Dewji

• **Ashangaa** Polisi kuwaona Watanzania kama wajinga, asema sakata hilo lilizua maswali yaliyokosa majibu hadi sasa... *Endelea ukurasa 2*


Nipashe
JUMAPILI
Maswali magumu 35 kupatikana MO Dewji
Kigogo jeshi la polisi auawa kwa mishale




## Kigogo wa OBC afikishwa kortini

UKURASA 2

UKURASA.3

Kaburi la aliyekuwa Mkurugenzi wa Vipindi wa Clouds Media Group (CGM), Ruge Mutahaba, aliyezikwa jana katika Kijiji cha Kiziru Wilaya ya Bukoba mkoani Bukoba. **PICHA: MTANDAO**

# Ruge azikwa kifalme Bukoba

# JPM aliibua upya sakata kutekwa kwa Mo Dewji

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli ameliibua upya sakata la kutekwa kwa mfanyabiashara maarufu Mohamed Dewji 'Mo' baada ya jana kueleza kushangazwa kwake na ukimya wa Jeshi la Polisi kuwafikisha wahusika mahakamani.

Alieleza kushangazwa na ukimya huo jana alipozungumza Ikulu, jijini Dar es Salaam baada ya kuwaapisha Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga na kushuhudia kuvishwa vyeo na kuapishwa kwa makamishna watano wa Jeshi la Polisi.

Rais Magufuli alisema kuna mambo ya kawaida ambayo jeshi hilo linatakiwa kuelewa kuwa Watanzania siyo wajinga, wanafahamu na wanajua kuchambua mambo.

"Niwatolee mfano tu alipotekwa Mohamed, tulipata habari nyingi, wameteka wazungu, lakini lilipokuja kumalizika suala hili, linaweka maswali mengi zaidi," Rais Magufuli alisema na kuongeza:

"Aliyetekwa amekutwa Viwanja vya Gymkhan usiku, watu wanajiuliza 'mmh... aliendaje pale?' Lakini alipokutwa pale na bunduki zikaachwa pale, unajiuliza huyu mtekaji amemleta hapa na ameamua kuondoka, aliondoka bunduki akaziachaje, angekutana na polisi wanaomtafuta?

"Wakajaribu kulichoma gari, lakini baadaye tunamwona aliyetekwa anakunywa chai na Kamanda (Lazaro) Mambosasa (Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam), maelezo hayapo.

"Baada ya siku chache, tukaambiwa nyumba aliyotekwa ni hii na aliyekuwa anawabeba watekaji ni huyu. Watanzania tukasubiri apelekwe mahakamani, baadaye kimya! Kimya mpaka leo (jana) miezi imepita."

Rais Magufuli alisema jambo hilo lina maswali mengi ambayo hayana majibu akieleza kuwa "labda ni mambo ya kisasa kama alivyo Mambosasa wa Dar es Sa-

INAENDELEA UK. 8

# Kabudi awatumia salamu 'wanaoichafua' nchi nje

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI mpya wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema Watanzania wasioweza kuizungumzia vizuri nchi yao wanapokuwa nje ya nchi, ni bora wakajifunza kukaa kimya.

Prof. Kabudi ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alitoa kauli hiyo Ikulu jijini Dar es Salaam jana mara tu ya kuapishwa na Rais John Magufuli kushika nafasi hiyo.

Alisema Watanzania wawe wazalendo kwa nchi yao na kwamba huu si wakati wa kuisema vibaya nchi.

"Huu si wakati wa kuisema vibaya nchi yetu, si wakati wa kuibagaza nchi yetu, si wakati wa kuibeza, nchi hii iliyojengwa na Mwalimu Julius Nyerere, si nchi ya kuchezeshwa, si nchi ya kudharauliwa na si nchi ya kudhihakiwa," alisema Prof. Kabudi na kuongeza:

INAENDELEA UK. 8

# Mkurugenzi OBC asomewa mashtaka uhujumu uchumi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Kampuni ya Uwindaji ya Ottero Business Corporation Ltd, (OBC), Isaya Mollel (59), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha na kusomewa mashtaka 10 yakiwamo ya uhujumu uchumi na kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. bilioni tano.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili Mkuu wa Serikali, Oswald Tibabyakomya, akisaidiana na Mwanasheria Mwandamizi wa Serikali, Martenus Marandu, na Mwanasheria wa Taasisi ya Kuzuia na

Kupambana na Rushwa (Takukuru), Dismas Muganizi mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Niku Mwakatobe, alidai mtuhumiwa huyo anakabiliwa na mashtaka 10 kati ya hayo mawili ni ya kuhujumu uchumi.

Tibabyakomya alidai kuwa Mollel akiwa Mkurugenzi wa Kampuni ya OBC, alitenda

INAENDELEA UK. 26


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,

04 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 12-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Tunduma** kuelekea **Dar-Es-Salaam**, gari hizo zenye namba za usajili:

**T 402 DFE / T 390 DHQ**
**T 624 DFA / T 777 AQR**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 20
Upana - mita 3.24
Kimo - mita 4.80

3. Njia itakayotumika: **Tunduma hadi Dar-Es-Salaam Kupitia Mikumi,** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

XXXXXXXX



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
March 4, 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano Tarehe 6/03/2019 kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka MWANZA kuelekea **S O N G E A NGAKA COAL MINING,** gari hilo lenye namba za usajili:

**T339 DEC/T634DCV**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 19.50**
**Upana - mita 3.50**
**Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika MWANZA, **SONGEA NGAKA COAL MINING Kupitia MOROGORO,** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

XXXXXXXX



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,

04 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 12-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam** kuelekea **Tanga**, gari hizo zenye namba za usajili:

**T 316 CZS / T 969 CPS**
**T 257 BXH / T 310 DDH**
**T 863 BZM / T 974 CPS**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 20
Upana - mita 2.84
Kimo - mita 4.80

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Tanga Kupitia Chalinze,** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

XXXXXXXX



**VACANCIES**

The following vacancies are available at T.M.J Hospital Ltd:-

1. **Consultant Gynaecologist** – Minimum 2 years Experience
2. **Consultant Opthamologist** – Minimum 2 years Experience
3. **Consultant Radiologist** - Minimum 2 years Experience
4. **Nursing Officer** – Minimum 3 years Experience
5. **Nurse Mid Wife** – Minimum 3 years Experience
6. **Accounts Assistant** – Minimum 1 year Experience
7. **Receptionist** – Minimum 1 year Experience
8. **Dialysis Technician** – Minimum 2 years Experience

Interested candidates may send their resume by post/Email to:-

**T.M.J Hospital Ltd,**
**P.O. Box: 20439**
**Mwai Kibaki Road,**
**Mikocheni**
**Dar es salaam.**

**Email: director@tmjhospital.co.tz**
**Last date: 15th March, 2019.**

XXXXXXXX

HABARI KITAIFA

# Mazishi ya Ruge usipime

**Na Waandishi Wetu**

MWILI wa Mkurugenzi wa Vipindi wa Clouds Media Group (CMG), Ruge Mutahaba, umezikwa na mamia ya waombolezi huku Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, akiahidi kuwa serikali itayaendeleza mambo ya maendeleo aliyokuwa akiyafanya.

Ruge alizikwa jana jioni katika kijiji cha Kiziru, Bukoba mkoani Kagera.

Shughuli za mazishi zilianza kwa kuaga mwili huo katika Viwanja vya Gymkhana, Bukoba na baadaye ulipelekwa nyumbani kwa wazazi wake eneo maalum la makaburi ya familia yake. Ruge alifariki dunia Februari 26, Afrika Kusini alikokuwa akiendelea na matibabu ya figo baada ya kulazwa tangu mwishoni mwa mwaka jana.

Katika mazishi hayo, mtangazaji wa Clouds FM, Hassan Ngoma, alisema matangazo ya redio ya Clouds yatazimwa kwa muda wa dakika tatu ikiwa ni sehemu ya kutoa heshima za mwisho kwa Ruge wakati mwili wake utakapokuwa unashushwa kaburini.

"Uongozi wa Clouds Media kupitia mkurugenzi wake, umekubaliana kwamba utazima redio ya Clouds wa dakika tatu, muda ambao jeneza la Ruge likishuka kwenye nyumba yake ya milele," alisema.

Akitoa salamu za rambirambi kwa niaba ya serikali, Waziri Kairuki alisema kifo cha Ruge kimetokea katika kipindi ambacho moto wa uchumi na fursa zingine za uwekezaji zinaendelea kupamba moto.

"Ruge alikuwa mmoja wa vijana aliyetoa mwanga na matumaini kwa vitendo na kuonyesha kwamba mengi yanawezekana kufanywa nchini na makundi mbalimbali hususani vijana," alisema.

Alisema akiwa Waziri wa Wizara ya Madini alipata nafasi ya kuzungumza mengi na Ruge.

Alisema Ruge alishiriki mengi kama mwekezaji mzawa na alionyesha namna ambavyo sekta binafsi ni injini ya ukuaji wa uchumi katika taifa.

"Amekuza vipaji, amesaidia vijana tumesikia namna alivyoshiriki kubuni malkia wa nguvu na kampeni nyingi, kampeni za afya, kampeni ya elimu, kampeni za uwezeshaji wananchi kiuchumi, alikuwa mchapakazi na jasiri alichanganyika na makundi ya watu wote, zaidi alikuwa makini na mwenye uthubutu mkubwa," alisema.

Akitoa neno la shukrani la familia, Makamu Mkuu mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Rwekaza Mukandara, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuonyesha upendo na kutoa misaada mbalimbali kwa familia ya Mutahaba wakati wa kuuguza hadi msiba.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Clouds Media Groups, Joseph Kusaga, alisema wana Bukoba kuwa wamepoteza lulu.

"Ruge ameijenga familia ya Clouds akiwa baba, ndani ya miaka mitano nilitoka kabisa nikamwacha, sikujuta shughuli zilikwenda kama zilivyotakiwa," alisema.

Kusaga aliwaahidi wakazi wa Bukoba kuwa yale ambayo Ruge aliyaacha watayapa kipaumbele ili yaweze kutimia.

"Familia tulikaa vizuri na Ruge na tunaendelea kumuenzi ndiyo maana tuliomba Ruge apite ofisini kwanza kabla ya kwenda sehemu nyingine, mila zilikuwa ngumu lakini mlikubali, ndani ya miaka 25 tulikaa na Ruge kujenga Clouds," alisema Kusaga.

Mbunge wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo), Zitto Kabwe, alisema Ruge ameonyesha kwamba iwapo sekta binafsi itapewa nafasi inaweza kufanya kazi na serikali na asasi zisizo za kiserikali kwa ufanisi.

Akitoa salamu kwa niaba ya kambi rasmi ya upinzani na vyama vya upinzani, Zitto alisema kazi ambayo Ruge ameifanya kwa vijana Tanzania wanawajibika kuiendeleza kwa sababu kazi kubwa aliyoifanya ni kwa ajili yao. Kwa upande wake, Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu Katokiki Bukoba, Methodius Kilaini, alisema wananchi wanapaswa kujituma na kutokata tamaa na watambue kwamba ajira zitakuja mbele.

"Kupitia Ruge wananchi na vijana mnatakiwa kujituma na kufanya kazi kwa kuthubutu na kukaa bila kusubiri ajira, fanya kazi ajira itakukuta mbele," alisema Askofu Kilaini.

Kilaini alitumia fursa hiyo kuwaasa watu kuishi kwa kutokuwa na kinyongo na visasi na wajenge kawaida ya kusameheana na kusahau mabaya ya mtu ambaye alikukosea.

Mwenyekiti wa Taifa Umoja wa Vijana (CCM) Taifa, Hery James, alisema ni muda wa vijana kujitafakari kuhusu wanavyoweza kuchukua na kuyaendeleza mazuri yote yaliyokuwa yakifanywa na Ruge.

***Imeandikwa na Romana Mallya, DAR na Restuta Damian, BUKOBA***



# Jafo amweka njia panda Meneja Tarura Dar

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ametoa wiki moja kwa Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Mkoa wa Dar es Saalam kuhakikisha anatengeneza mashimo na viraka vya barabara ndani ya jijini hilo.

Sambamba na hilo, amemtaka kujieleza sababu za barabara zake nyingi kukatwa huku zikikaa zaidi ya miezi miwili bila kurekebishwa.

Agizo hilo alilitoa jana alipozungumza na waandishi wa habari kwenye ziara ya siku moja kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Jiji la Dodoma. Jafo alimwagiza meneja huyo kuhakikisha anaziba barabara zilizokatwa na kukaa kwa zaidi ya miezi miwili bila kufanyiwa matengenezo na kuondoa vifusi vilivyoziba barabara.

"Maeneo mengi kwa Jiji la Dar es Salaam barabara zimekatwa halafu hazitengenezwi na hii ni moja ya kisababishi kikubwa cha ajali," alisema.

Hata hivyo alimtaka meneja huyo kuwa ifikapo Alhamisi wiki hii ampe maelezo kwa nini barabara zake nyingi zimekatwa lakini hazijarekebishwa kwa zaidi ya mwezi moja hadi miwili bila kufanyiwa matengenezo.

Alisema kama walikuwa wanajua hawana fedha za kufanyia matengenezo ya barabara hizo kwa nini wakate barabara hizo na kusababisha usumbufu kwa wananchi wanaozitumia.

Alitaja maeneo ambayo yanayolalamikiwa kwa changamoto hiyo ya miundombinu ya barabara katika jiji hilo ni Temeke, Kigamboni na Oysterbay. Aliongeza kuwa kuna maeneo mengi ya barabara za jiji hilo yana changamoto, hivyo wahusika wanatakiwa kuzishughulikia ili kuondoa kero hiyo.

Hata hivyo, alifurahishwa na uongozi wa mkoa wa Dodoma kwa kushughulikia kero ya miaka mingi ambayo ilisababisha kukwamisha ujenzi wa barabara ya Martin Luther hadi Area D, jijini Dodoma.

Alisema mgogoro uliokuwapo kati ya uongozi wa jiji na Kanisa la Tanzania Assembles of God, ulisababisha mkandarasi kushindwa kukamilisha ujenzi wa kipande hicho cha kilomita tano.

Katika ziara hiyo, Waziri Jafo alitembelea barabara ya Veta hadi Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Dodoma na kudai kuwa ilikuwa kero kwa watu wanaotumia kwenda bungeni.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema katika kuhakikisha hawacheleweshi ujenzi wa barabara, walifanya kikao cha pamoja ili kuondoa utata.

Alisema ili kuhakikisha wanakamilisha miradi ya maendeleo Kamati ya Ushauri ya Mkoa imekuwa ikifuatilia kila mradi ili kukamilika kwa wakati.


ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

**Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole**
**S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania**
**Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz** **Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu Na.19 cha sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 17 (4) ya Kanuni za Mafuta (Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Reja Reja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 380 la 2018)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na majina ya vituo vya mafuta kama ifuatavyo:-

1. **Jina la awali la kituo**: Amary A. Bawazir Petroleum – Pangani Petrol Station
   **Nambari ya Leseni:** PRL-2018-290
   **Mahali Kituo kilipo**: Kiwanja Namba 1840, Kitalu "B" Pangani Mjini, Wilaya ya Pangani, Mkoani Tanga
   **Jina linalopendekezwa**: GIGA Oil Company Limited – Pangani Petrol Station
   **Mmiliki wa awali**: Amary Abdallah Bawazir
   **Mmiliki mpya**: GIGA Oil Company Limited

2. **Jina la awali la kituo**: Bunazi Filling Station
   **Nambari ya Leseni:** PRL-2016-041
   **Mahali Kituo kilipo**: Kiwanja Namba 522, Kitalu "A" Bunazi, Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera
   **Jina linalopendekezwa**: Quick Service Station
   **Mmiliki wa awali**: Beach Evarist Makaga
   **Mmiliki mpya**: Quick Service Station

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mkurugenzi Mkuu,**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA,

XXXXXXX


# Serikali yaruhusu matumizi ya zebaki

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameruhusu matumizi ya zebaki ambayo awali serikali ilikuwa imeyazuia.

Akiendesha mkutano wa wadau wa kemikali nchini uliofanyika jijini Dar es Salaam jana kwa lengo la kujadili namna ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara, Ummy aliwataka waagizaji wa kemikali hiyo kujisajili Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) ili kupata kibali cha kuitumia kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Waziri huyo alitangaza uamuzi huo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wadau wa kemikali, akieleza kuwa awali walizuia matumizi ya kemikali hiyo lakini kutokana na marekebisho ya Sheria ya Madini, wameruhusu kemikali hiyo kutumika hadi mwaka 2028 utakapotolewa mwongozo mpya.

Katika kikao hicho, waziri huyo alisema serikali itafanya marekebisho ya sheria zinazoihusu GCLA ambazo zinakuwa kikwazo, ikiwa ni pamoja na tozo za vibali kwa wafanyabiashara hao na muswada utawasilishwa bungeni Septemba mwaka huu.

# Hati za kigogo Takukuru zatinga rasmi kortini

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imepokea hati tatu za viwanja kama kielelezo cha upande wa Jamhuri kutoka kwa mashahidi wawili tofauti katika kesi inayomkabili Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai na wenzake.

Aidha, mahakama imepokea hati hizo zinazomilikiwa na Gugai mkoani Pwani ikiwamo Kibaha kiwanja kimoja na viwili vilivyoko Kaole Bagamoyo.

Vielelezo hivyo vilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Shahidi wa saba, Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Gilly Simiyu (40), alidai kuwa majukumu yake ni kuidhinisha nyaraka zote zinazohusu ardhi pamoja uhamishaji wa miliki.

Alidai kuwa anamfahamu Gugai kupitia nyaraka zao kwamba anamiliki ardhi Kibaha, kiwanja namba 209 eneo la mkoani.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Awamu Mbagwa, akisaidiana na Mawakili wa Serikali George Barasa na Vitalis Peter.

Akiongozwa na Mbagwa, shahidi huyo alidai kuwa hakumbuki siku lakini maofisa wa Takukuru walikwenda ofisini kwake kutaka kujua mmiliki wa hati namba 209 ni nani.

Alidai kuwa aliitisha jalada na kubaini kwamba mmiliki wa hati hiyo ni Gugai.

"Takukuru waliandika barua kwa Mkurugenzi wa Halmashauri wakiomba jalada la Gugai, niliijibu na kuwakabidhi hati hiyo," alidai shahidi na kuomba mahakama kupokea hati hiyo kama kielelezo na ilikubali.

Shahidi wa nane, Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Khalid Habulegeni (40), alidai alipokea maelekezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo kuwapatia maofisa wa Takukuru hati mbili namba 103 na 104.

Shahidi aliomba mahakama ipokee hati hizo kama kielelezo cha Jamhuri katika kesi hiyo.

Gugai anakabiliwa kutakatisha fedha na kumiliki mali zilizozidi kipato chake.

Upande wa Jamhuri umeshaita mashahidi akiwamo Msajili wa Hati Msaidizi, kutoka Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Joanitha Kazinja na msaidizi wa hati Kanda ya Kaskazini kutoka Wizara Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Emmanuel Bundala.

---

## NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL(NEMC)

***BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA***

## TAARIFA KWA UMMA

### UTEUZI WA KAMATI MAALUMU YA KUISHAURI SERIKALI KUHUSU UVUNAJI ENDELEVU WA RASILIMALI YA MCHANGA NCHINI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mheshimiwa January Y. Makamba (Mb.), ameteua kamati maalum yenye wataalam 14 itakayofanya kazi ya kuishauri Serikali kuhusu namna bora na endelevu ya kuchimba mchanga katika mito na maeneo mengine nchini kote bila kuharibu mazingira wala kukiuka sheria zilizopo.

Uamuzi wa Waziri Makamba kuteua kamati hiyo umekuja baada ya kufanya ziara kukagua maeneo mbalimbali yanayochimbwa mchanga hususani katika baadhi ya mito iliyoko katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na kubaini changamoto za uchimbaji holela wa mchanga- unaopelekea uharibifu mkubwa wa mazingira na kingo za mito; kusababisha athari kwa jamii na kuikosesha Serikali mapato kufuatia mchanga huo kuuzwa kiholela.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kifungu cha 13 (1-3) inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Kusimamia Mazingira nchini, kuteua Kamati ya wataalam kutathmini kwa kina suala kama hilo linalohusu uharibifu wa mazingira na kuishauri Serikali namna bora ya kuvuna Rasilimali ya Mchanga na kwa utaratibu ulio endelevu.

Wajumbe 14 walioteuliwa wa kamati hiyo wanatoka katika Ofisi na Taasisi mbalimbali za serikali ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wizara ya Madini, Kamisheni ya Madini, Wizara ya Maji (Bonde la maji la Wami na Ruvu-Wami/Ruvu Basin Water Board (WRBWB), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na mkoa wa Pwani, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam -Chuo cha Uhandisi na Teknolojia -COET) na Chuo cha Sayansi na Mali Asili- Viumbe.

Mwenyekiti aliyeteuliwa kuongoza kamati hiyo ni Mhandisi Benjamin J. Mchwampaka kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) na orodha kamili ya majina ya wataalam ambao ni wajumbe wa kamati hiyo, fani zao na Taasisi/ofisi wanazotoka ni kama ifuatavyo:-

| Sno. | JINA | TAASISI/ MWAJIRI |
|---|---|---|
| 1. | Benjamin J. Mchwampaka- (*Mhandisi Migodi*) | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) (**Mwenyekiti wa Kamati**) |
| 2. | Angela Kileo (*Mwanasheria*) | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)-**Mjumbe** |
| 3. | Redempta Samwel (*Mhandisi wa Mazingira*) | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) -**Mjumbe** |
| 4. | Onesphory Kamukuru -(*Mhandisi Mazingira*) | Ofisi ya Makamu wa Rais-**Mjumbe** |
| 5. | Mshuda W. Kisasila (*Mhaidrojiologia*) | Wizara ya Maji -Wami/Ruvu Basin Water Board (WRBWB) -**Mjumbe** |
| 6. | Mariam Esanju (*Mhaidrolojia*) | Wizara ya Maji -*Wami/Ruvu Basin Water Board* (WRBWB) -**Mjumbe** |
| 7. | Dr. Churchil M. Mujuni (*Msimamizi wa Mazingira*) | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa – Dar es Salaam-**Mjumbe** |
| 8. | Gratius Haule (Mhandisi wa Maji) | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa – Dar es Salaam-**Mjumbe** |
| 9. | Cecil Siafu (*Mhandisi Mazingira*) | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa – Pwani-**Mjumbe** |
| 10. | Cleophace Gregory (*Msimamizi Mipango ya Mazingira*) | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa – Pwani-**Mjumbe** |
| | | |
| 11. | Godfery Nyamurunda (*Mchumi*) | Wizara ya Madini -**Mjumbe** |
| 12. | Ally Maganga (*Mhandisi Migodi*) | Wizara ya Madini-**Mjumbe** |
| 13. | Dr. Daniel Mussa Budeba (*Mhadhiri- Chemical and Mining Engenearing Department*) | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*Chuo cha Uhandisi na Teknolojia -COET*) -***Mjumbe*** |
| 14. | Dr. Emmanuel Kazimoto (*Mhadhiri - Geology department*) | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*Chuo cha Sayansi na Mali Asili- Viumbe-* ***Mjumbe)*** |

***Hadidu za Rejea za kazi hii ni kama ifuatavyo:-***

1. Kubaini na kuchambua madhara ya kimazingira na kijamii (Environmental and Social Impacts) ya uchimbaji mchanga kwa mfumo unaoendelea sasa katika maneo ya mito kwenye mkoa wa Dar es Salaam na Pwani;
2. Kutathmini mahitaji halisi ya mchanga (kwa mita za ujazo-M3) kwa mwaka katika Jiji la Dar es Salaam, mkoa wa Pwani na maeneo jirani na kuainisha kiasi cha mahitaji ya mchanga kwa miaka 10 ijayo na vilevile miaka 20 ijayo;
3. Mbali na machimbo ya mchanga kwenye mito, kubainishaa maeneo mengine yanayofaa kwa uchimbaji wa mchanga badala tu ya mito inayochimbwa sasa, ikiainishwa na mahitaji ya mchanga kwa miaka 10 ijayo na vilevile miaka 20 ijayo;
4. Kufanya mapitio ya Sheria na miongozo mbalimbali inayosimamia mazingira ya mito ikiwemo uchimbaji wa mchanga katika mito ili kubaini mapungufu na kutoa mapendekezo ya maboresho;
5. Kubainisha na kupendekeza njia au mfumo bora wa uchimbaji wa mchanga kwenye mito, utafiti wa kiteknolojia ukizingatiwa ili kuondoa athari mbaya za uchimbaji wa mchanga katika mazingira ya mito, ikiwa ni pamoja na uchimbaji holela katika maeneo hayo (Mfano-maeneo ya mito yagawanywe kwa wakandarasi kwa makataba ambao watapewadhamana ya kutunza mazingira na kurudisha gharama zao kwenye mauzo ya mchanga, na kadhalika) na ;
6. Kushauri hatua au utaratibu unaofaa kuchukuliwa kuhakikisha maeneo ya mito yaliyoathirika na uchimbaji holela yanasafishwa kwa utaratibu endelevu usioathiri kingo za mito hiyo na Mazingira.

Muda wa kamati iliyoteuliwa kufanya kazi hii ni mwezi mmoja (siku 30) ambapo taarifa ya kina kuhusu agizo hili itawasilishwa Serikalini. Jamii inaombwa kutoa ushirikianao kwenye kamati hii katika kipindi hiki cha kutekeleza majukumu yake.

**Taarifa hii imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma,**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**
**Plot No. 28, 29 &30-35 Regent Street, P.O. Box 63154, Dar es Salaam.**
**Simu: +255 22 2774889, Direct line: +255 22 2774852Mobile: 0713 608930/ 0692108566**
**Fax: +255 22 2774901, Email: dg@nemc.or.tz**

215089202

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Onyo la serikali kuhusu 'earphones' lisipuuzwe*

**TANZANIA** juzi iliungana na nchi nyingine ulimwenguni kuadhimisha Siku ya Usikivu Duniani na serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ilionya matumizi ya muda mrefu ya spika za masikioni (earphones) zinavyoweza kusababisha tatizo la usikivu.

Tangu teknolojia ya mawasiliano ilipoingia kwa kasi duniani, vifaa vinavyotumika kwa teknolojia hiyo vimeongezeka kwa wingi kupitia matumizi kama ya simu za mkononi na kompyuta.

Kila kitu kina faida na hasara zake, ingawa teknolojia imerahisha vitu vingi, lakini athari zake kiafya ni kubwa ambazo zinafanya taifa kutumia fedha nyingi kuagiza dawa za matibabu.

Katika nchi zinazoendelea vifaa hivyo vimekuwa vikiingizwa kwa njia mbalimbali ambazo zingine ni vigumu kuzidhibiti ili kuepuka watu wasiingie kwenye madhara ya afya.

Matumizi makubwa kwa sasa ya vifaa hivyo ni kwenye simu na kompyuta na wengi hupenda kuangalia sinema au nyimbo wakiwa wameweka vifaa hivyo kwa kufungulia sauti kubwa kwenye masikio yao. Baadhi ya wanaovitumia pia imekuwa ni mtindo wao kuweka na kushinda na vifaa hivyo siku nzima bila kujali madhara yake. Juzi wakati Tanzania ikiadhimisha siku hiyo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alionya kuhusu kuzidisha matumizi ya vifaa hivyo kwa muda mrefu na athari inayoweza kujitokeza.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, watu hao wako hatarini kupata matatizo ya usikivu na kuwataka kupunguza ili kuepuka taifa na ugonjwa wa usikivu. Watu wa rika mbalimbali wamekuwa wakionekana kupendelea kutumia 'earphones' wawapo na kompyuta ofisini au simu za mkononi kwa muda mrefu hali inayo hatarisha kupata tatizo la usikivu.

Kibaya zaidi baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwasikilizisha watoto wao wachanga simu kwa kuwawekea vifaa hivyo, bila kujua kuwa kwa kufanya hivyo anamletea mtoto matatizo makubwa.

Serikali imesema itawasiliana na Shirika la Viwango (TBS) kuhakikisha vifaa hivyo (earphones) vinavyoingizwa nchini vinakuwa na ubora unaotakiwa kwa kuwa amepatiwa taarifa kuwa kuna vinavyoingizwa ambavyo havina ubora na kuongeza tatizo la usikivu. Kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia tano ya watu duniani (sawa na watu milioni 466) wana ukosefu wa usikivu.

Kati yao, milioni 432 ni watu wazima na milioni 34 ni watoto na kwamba ifikapo mwaka 2050, zaidi ya watu milioni 900 watakuwa na changamoto ya ukosefu wa usikivu duniani.

Aidha, wagonjwa waliohudumiwa katika Idara ya Masikio, Pua na Koo kati ya Novemba mwaka jana na Januari mwaka huu, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ni 5,959 na kati yao, 454 (asilimia nane) walikuwa na ukosefu wa usikivu.

Serikali katika kukabiliana na changamoto hiyo imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo tiba kwa wagonjwa wenye ukosefu wa usikivu. Kwa mwaka jana wagonjwa 117 walipatiwa vifaa vya kukuza mawimbi ya sauti na 43 walifanyiwa upasuaji wa kuziba tundu la ngoma ya sikio.

Serikali pia imesema kwa mwaka huu, kipaumbele chao ni kuboresha huduma za usikivu katika hospitali za rufani kwa kuwa bado zina changamoto.

"Hii changamoto tumeiona, tutahakikisha hospitali za rufani za mkoa zinakuwa na daktari bingwa wa masuala ya pua, masikio na koo na vifaa vinakuwapo ili viwasaidie katika utendaji wao wa kazi," alisema Ummy.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Makwaiya Makani, hospitali hiyo, Machi mosi, ilianza kutoa huduma ya usikivu na jumla ya wananchi 264 walijitokeza. Kati ya 172 walihitaji uchunguzi wa kusikia na 64 walikutwa na matatizo ya usikivu na wamepatiwa rufani ya matibabu.

Hata hivyo, serikali ina jukumu kubwa la kutoa elimu kwa wananchi wake ili kuepusha taifa lisiingie kwenye tatizo la usikivu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

**BUSARA**

**KUB ADILISHA TAREHE YA KUZALIWA**
**KATIKA MIFUMO YA KULA HELA ZA UMMA, KUNA MCHEZO WA KUBADILISHA TAREHE YA KUZALIWA KABLA YA KUSTAAFU ILI KUENDELEA KUFANYA KAZI. WANAAPA MAHAKAMANI WAKIENDELEA KUBAKI KAZINI KULA JAMBO LA WENGINE. HOJA HIYO!**
**NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## *Tusikwepe kuhudumia kambi, ndiko kwenye ufaulu shuleni*

**MATOKEO** mabaya ya mitihani, ni changamoto inayozikabili baadhi ya shule nchini na kukwamisha maendeleo ya shule na wanafunzi wake.

Zipo baadhi ya shule ambazo zimebuni mbinu za kukabiliana na changamoto na kufanikiwa kupata matokeo mazuri kwenye mitihani hiyo, mfano hai ukiwa huko wilayani Ngurdoto, kama ilivyo katika sumulizi ya ukurasa wa 16 wa gazeti hili. Mbinu mojawapo ni kuanzisha kambi za taaluma, ili kuwanoa vizuri wanafunzi na mwisho wa siku unapoletwa mitihani, inawakuta wamejipanga kuufanya bila hofu na kufanikiwa kufaulu.

Kwa mfano, mkoani Simiyu kambi za kitaaluma zimeonyesha matokeo mazuri kwa wanafunzi waliowekwa kambini, kujinoa kitaaluma. Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, alishakaririwa na vyombo vya habari, akisema kambi hizo zimeongeza ufaulu na kuufanya Simiyu kushika nafasi ya 10 kitaifa mwaka 2018.

Matokeo hayo ni ya kidato cha nne na kwamba mwaka 2017, mkoa ulishika nafasi ya 26 kitaifa, lakini baada ya kuanzishwa kwa makambi mwaka 2018, walipanda na kushika nafasi ya kumi.

Hiyo ndio njia mojawapo ambayo, baadhi ya shule za msingi na sekondari zimekuwa zikiitumia, ili kuongeza uelewa na ufaulu wa mitihani kwa wanafunzi na inapaswa kuigwa na mikoa mengine nchini. Wakati jamii inaendelea kufurahia matunda ya elimu bila ya malipo, ni vyema ikawekwa mikakati ya kusaidia wanafunzi kufanya vizuri, kama ambavyo baadhi ya mikoa imebuni uanzishwaji wa kambi za kitaaluma.

Kambi hizo zina mahitaji yake muhimu, zikiwamo vyakula kwa wanafunzi, ambavyo wazazi wanatakiwa kuchangia kwa ajili ya maendeleo ya watoto wao.

Tatizo la baadhi ya wazazi kutochangia vyakula, ili kufanikisha kambi hizo limekuwa likijitokeza kwenye maeneo mbalimbali nchini, huku wakidai kwamba serikali ilishatangaza kutoa elimu bure. Baadhi ya wadau wa elimu wa Halmashauri ya Morogoro Vijijini, waliwahi kulalamikia hali hiyo, walipokutana kujadili maendeleo ya wanafunzi shuleni.

Hiyo ilikuwa mwaka jana wakasema baadhi ya wazazi hawataki kusikia habari za kuchangishwa vyakula kwa sababu serikali ilishazuia michango ya aina yoyote, pia inatoa elimu bure.

Hata kama serikali imezuia michango au ameamua kutoa elimu bure, sidhani ni tatizo iwapo walimu na wazazi watakutana na kuweka mikakati ya kuboresha elimu kwenye maeneo yao.

Vilevile, sidhani kama serikali inazuia mipango inayolenga kuboresha elimu, hivyo waliokuwa wakikataa kutoa chakula kwa ajili ya kambi za taaluma, watafakari kisha wachukue hatua za kuwasaidia watoto wao. Wazazi wa aina hii, bado wanahitaji kuelimishwa, watambue wana nafasi kubwa katika maendeleo ya kielimu ya watoto wao, ili kuchangia kambi za taaluma zinazoonekana kuwa matokeo mazuri.

Ikumbukwe kwamba, kambi za kitaaluma huwakutanisha wanafunzi wenye uwezo tofauti darasani, kutoka shule mbalimbali na kubadilishana uzoefu wakiwa na walimu wao wanaowaongezea maarifa. Kwa kawaida, watu hujifunza kutoka kwa wengine, hivyo hata kwenye suala hilo la kambi za taaluma, ni vyema kuigwa hasa kutokana na ukweli kwamba, zimekuwa matokeo mazuri kama ilivyokuwa mkoani Simiyu.

Mkoa wa Simiyu umeonyesha njia, mingine nayo inaweza kuiga, pia wazazi wao mstari wa mbele kuunga mkono njia hiyo kwa kuchangia chakula, ili watoto wao waweze kula wakiwa kambini.

Bila kukubaliana na ukweli huo, wataendelea kulalamikia matokeo mabaya ya mitihani kwa watoto wao, kumbe hata wenyewe wana mchango wa kufanya yawe hivyo.

Hivi mzazi, anaona ugumu gani kutoa chakula kwa ajili ya mtoto wake, ambaye yuko kambini akijiandaa kujiweka sawa kwa ajili ya mitihani? Anataka nani ampe chakula mwanawe?

Elimu inatajwa mara zote ni ufunguo wa maisha, hivyo mtoto anapopata elimu, anakuwa ameshapata mbinu za kusimamia maisha atakapokuwa mtu mzima, hivyo asikatishwe tamaa.

Wazazi wakubali kwamba maisha ya shule ni safari ndefu na zina changamoto zake, zikihusisha mbinu nyingi, kama kuweka kambi ya kuwanoa vizuri wanafunzi.

## HABARI KITAIFA

# Wasiojulikana wafyeka hekta 60 za muhogo

**Na Dege Masoli,** HANDENI

TUKIO la kufyekwa hekta zaidi ya 60 zilizo kuwa zimepandwa mbegu za muhogo lililofanywa na watu wasiojulikana wilayani Handeni, Mkoa wa Tanga, limezua hofu kwa wakulima wilayani humo.

Watu hao wanadaiwa kuvamia mashamba ya wakulima katika Kijiji cha Bongi kilichopo Kata ya Sindeni, wilayani hapa.

Wakitoa kilio chao kwa Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe, aliyetembelea eneo hilo kujionea hali halisi, wananchi hao walidai kuwa watu waliohusika na tukio hilo kama hawatakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria watasababisha uvunjifu wa amani kwa wakazi hao.

Mmoja wa wakazi hao Said Adam, alisema tukio hilo limewafanya wananchi kuingiwa na hofu na linaweza kusababisha uvunjifu wa amani.

Aidha, alisema uharibifu huo ni sawa na mauaji kwa kuwa mazao yaliyofyekwa yalikuwa tegemeo la maisha na familia zao na kitendo hicho kitawasababishia janga la njaa.

Mkazi mwingine, Asha Salehe, alimueleza Mkuu huyo wa wilaya kuwa baada ya kupata taarifa za uharibifu huo na kwenda kujionea mazao yao yalivyofyekwa mashambani, wamepoteza matumaini kwa kuwa walikuwa wakitegemea zao hilo.

Hata hivyo, Gondwe licha ya kulaani watu waliotekeleza tukio hilo aliloliita kuwa ni la kinyama, aliahidi kupatikana kwa kila aliyejihusisha na ukatili huo na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Aliwataka wakazi wa maeneo hayo kushirikiana na vyombo vya usalama kwa kutoa kila taarifa wanazozipata zinazohusu tukio hilo ili kurahisisha kukamatwa kwa wahalifu hao.



Waziri wa Katiba na Sheria Balozi Augustine Mahiga, Waziri wa Mambo ya Nje, Profesa Palamagamba Kabudi pamoja na makamishna watano kutoka Jeshi la Polisi wakila kiapo cha uadilifu kwa viongozi wa umma Ikulu jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: IKULU**

# PM ataja sababu za kuwabadili Mahiga, Kabudi

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli, ametaja sababu za mabadiliko madogo aliyoyafanya ndani ya Baraza la Mawaziri kuwa ni ya kawaida katika kuboresha utendaji kazi kwenye serikali yake.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam baada ya kuwaapisha mawaziri aliowabadilisha wizara ambao ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga.

Rais Magufuli alisema ni kawaida kwa kocha wa timu kufanya mabadiliko.

"Niliamua kufanya mabadiliko kwenye Wizara ya Sheria na Mambo ya Nje, ni mambo ya kawaida ukiwa na timu yako na wewe ni kocha unaweza kufumua timu yako ukamchukua mlinzi ukampeleka kushambulia na mshambuliaji ukamfanya mlinzi," alisema.

"Kwa wakati huu nafikiri huyu nimpeleke mshambuliaji na wakati huu nimfanye mlinzi. Wapo wanaosema huyu siyo mwanasheria, kwani anakwenda kufundisha sheria?" Alihoji.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, mawaziri waliopita hawakuwa na taaluma ya sheria kwenye wizara hiyo na kwamba Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu ni wanasheria hivyo sio lazima kuwa na wanasheria.

Rais Magufuli alisema kwenye Wizara ya Mambo ya Nje anahitaji watu kama Kabudi wa kuwasukuma na ndiyo maana aliamua kumpeleka huko.

"Niliamua kumpeleka pale ili diplomasia iliyopo ikaungane na sheria, nafikiri mambo yatakwenda vizuri," alisisitiza.

Mwaka 2015 alipoteua Baraza la kwanza la mawaziri alianza kazi na mawaziri 19 na manaibu 16, lakini kwa mabadiliko ya juzi walioanza na nafasi zao bila kuondolewa wamebaki wanane.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitikiswa mwaka jana kwa Naibu Waziri Susan Kolimba, huku Wizara ya Katiba na sheria mabadiliko yakimuhusu Waziri.

Mawaziri walioanza na Rais Magufuli na hadi wakiwa kwenye nafasi zao ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Willium Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenister Mhagama.

Wengine ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, January Makamba, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango na Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo, Prof. Joyce Ndalichako.

Aidha, mawaziri alioanza nao na kuwabadilisha na bado wako ndani ya Baraza la Mawaziri ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Angella Kairuki, ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji).

Mwingine ni Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ambaye alianza kama Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, na Dk. Harrison Mwakyembe, ambaye alianza kama Waziri wa Katiba na Sheria na sasa ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

# Bilioni 23/- kufua umeme upepo

**Na Mary Geofrey**


KAMPUNI ya uzalishaji wa nishati ya umeme kwa kutumia upepe ya Windlab, imetia saini mkataba wa Dola za Marekani milioni 10 (Sh. bilioni 23.4) na Kampuni ya Eurus Energy Holdings Corporation ili kutekeleza miradi ya uzalishaji wa nishati hiyo katika nchi nane za Ethiopia, Kenya, Tanzania, Zambia, Uganda, Rwanda, Burundi na Malawi.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Windlab ilieleza kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Roger Price, aliingia makubaliano hayo na kampuni hiyo ya Eurus ili kutoa huduma katika nchi za Afrika.

Alisema wameingia mkataba na Tanzania ili kuzalisha umeme MW 1,650 ambao utekelezaji wake unaendelea katika ngazi ya awali.

"Windlab itatumia fedha hizi kuongeza kasi ya maendeleo ya miradi ya msingi Afrika Mashariki kukidhi mahitaji makubwa ya umeme ambayo hayajafikiwa kwa kutumia upepo," Price alinukuliwa katika taarifa hiyo.

Alisema kuwa kwa upande wa Kenya, kampuni hiyo imeingia mkataba wa ushirikiano na serikali ya nchi hiyo kuzalisha umeme wa upepo, jua na uhifadhi kwa njia ya betri ambao umefikia MW 166 chini ya mpango wa ushirikiano na sekta binafsi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Seleman Jafo (kushoto), akiwaangalia mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara ya Veta na Chuo cha Biashara (CBE) jijini Dodoma jana. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# JPM aliibua upya sakata kutekwa

INATOKA UK.2

laam, Watanzania walitarajia kesho yake angekuwa mahakamani na angeweza kuwataja wenzake."

"Watanzania walitaka kuona mmiliki wa nyumba anajibu kwamba 'nyumba yako anaweza kuja mtu akakaa siku ngapi bila kujua walioingia ni kina nani?' Lakini hakuna majibu. Haya hata kama Watanzania watanyamaza, mioyo yao haitaridhika," Rais Magufuli alisema.

Alisema vitu hivyo vinatia dosari ambazo zinalichafua Jeshi la Polisi licha ya kuwa linafanya kazi nzuri katika maeneo mengi.

Bilionea huyo kijana alitekwa Oktoba 11, mwaka jana saa 11 alfajiri na watu wasiojulikana kwenye Hoteli ya Colosseum iliyoko Oysterbay jijini Dar es Salaam alikokwenda kufanya mazoezi kwenye 'gym' ya hoteli hiyo kisha kuachiwa usiku wa kumkia Oktoba 20.

Baada ya kupatikana kwa Mo, ikiwa siku tisa tangu kutekwa kwake, Jeshi la Polisi lilieleza kuwa alipatikana akiwa ametelekezwa ndani ya gari eneo la Viwanja vya Gymkhan jijini.

Bilionea huyo alipatikana ikiwa ni siku chache baada ya familia yake kutangaza kitita cha Sh. bilioni moja na alipopatikana, Kamanda Mambosasa aliwaambia waandishi wa habari kuwa watekaji hao walikuwa wakimpa huduma zote na walimtelekeza akiwa na bunduki.

### KAULI YA IGP SIRRO

Oktoba 20, mwaka jana, Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, alizungumza na waandishi wa habari na kuwaonyesha picha za gari lililotumika kumteka mfanyabiashara huyo na kuahidi kuwa ni lazima wawakamate wote waliomteka.

IGP alisema watekaji hao walitaka fedha na walitaka kuchoma gari kupoteza ushahidi na kwamba walimwachia majira ya saa nane usiku. Alisema upelelezi unafanyika kwa kushirikiana na Polisi wa Kimataifa (Interpol).

Nipashe ilizungumza na IGP Sirro jana kwenye Viwanja vya Ikulu jijini ikitaka kujua hatua zaidi zinazochukuliwa baada ya Rais kulizungumzia suala hilo.

"Yule mtuhumiwa bado yuko mahabusu, tunaendelea kushirikiana na Interpol kuwasaka walioshirikiana naye ambao ni raia wa kigeni. Unajua kuna utaratibu wa kuwaandikia wenzetu na mchakato wa kuwakamata ukamilike, hivyo tutawakamata," alisema Sirro.

Rais Magufuli pia alisema haikuwa rahisi kuwapata makamishna kwa kuwa alilazimika kushirikisha Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Katibu Mkuu na IGP kuchambua kila jina kulingana na utendaji kazi wao.

Makamanda waliopandishwa vyeo ni Charles Mkumbo kuwa Kamishina wa Intelejensia na Jinai, Liberatus Sabas kuwa Kamishina wa Operesheni na Mafunzo, Leonard Paulo kuwa Kamishana wa Fedha na Ugavi na Benerdict Wakulyamba kuwa Kamishna wa Utawala na Menejiment ya Utumishi.

"Katika kazi za kutumikia taifa, kunahitaji kujitoa, huwezi kuwa Kamanda wa Opareshini halafu unaona askari wako wanapigwa risasi, wanakufa halafu unajiita Kamanda wa Operesheni, leo wanakufa saba, kesho wawili, tulimjaribu Liberatus Sabas, tukaona anafaa ndiyo maana tukamteua," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri, ukiondoa dosari ndogondogo za watu wachache, huku akiweka wazi sababu za kutumbuliwa kwa Mkuu wa wa Upelelezi (OC- CID) wa Wilaya za Rombo, Tanga, Pangani na Kasulu.

"Ni kwa sababu wale 'ma-OCD' ndiyo washiriki wakubwa wa magendo na dawa ya kulevya, lakini hawajali. Natoa wito pamoja na kazi nzuri mnayofanya, wachache wanaowaharibia jina mjitahidi kuwarekebisha," alisema.

### KIKOSI CHA TAZARA

Rais Magufuli pia alisema aliamua kukivunja kikosi cha Tazara kwa kuwa kazi yake ilikuwa kutafuta fedha kutoka kwa wafanyabiashara kwa kuomba rushwa.

"Kitengo kilikuwa kinaitwa 'Financial Crime', hakuna 'crime' (jinai) yoyote ya fedha iliyopelekwa mahakamani, tukasema hatuhitaji kitengo kama hicho, tukasema wakafanye mikoani na wilayani walikokuwa," alisema.

Kuhusu tukio la kukamatwa kwa dhahabu ya mabilioni ya shilingi jijini Mwanza, Rais Magufuli alisema upo ushahidi wa kutosha kuwa polisi walihusika kusindikiza dhahabu na wakahongwa mabilioni ya shilingi na mambo kama hayo na mengine yanatia dosari jeshi hilo.

Alimtaka IGP kutoogopa kupeleka kwake majina ya viongozi ndani ya jeshi hilo ambao anataka wapunguzwe nyota zao kwa kuwa imezoeleka kutoa nyota, hivyo ifike mahali washushwe vyeo.

"Ambao wanashindwa kufanya kazi vizuri, wasipelekwe makao makuu, kama RPC ameshindwa usimpeleke makao makuu, mpeleke akawe chini ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa (RPC) mwingine," alisema.

# Kabudi awatumia salamu 'wanaoichafua' nchi nje

INATOKA UK. 2

"Mtanzania yeyote ambaye ana matatizo na nchi yetu, atutendee jambo moja tu -- akae kimya kama imemshinda kutokusema yasiyofaa kusema kwa nchi yake. Lakini tujue tuna jukumu kubwa la kuijenga nchi, kuimarisha mahusiano na urafiki na wale wanaotutakia mema."

Alisema kazi ya miaka mitatu ya Rais Magufuli katika kusimamia haki ya maji, elimu na afya ambazo wengi wanadhani siyo haki ya msingi, imefanyika na ni lazima dunia ielezwe.

"Tumefanya pia haki za binadamu za siasa na kijamii, lakini haki za binadamu za kiuchumi, kijamii na kiuchumi na ndiyo maana tamko la haki za binadamu la dunia halikuzitenganisha haki hizo," alisema.

Prof. Kabudi alisema: "Tanzania ndiyo nchi pekee ambayo imeweka suala la haki za binadamu ndani ya katiba yake, hatuhitaji kukumbushwa ila tunahitaji kuwaambia watu wengine kuwa nchi hii ni ya kidemokrasia katika muktadha na mazingira ya Tanzania, yapo ambayo hatutabadilika kwa sababu ni ya Watanzania na utanzania wetu."

Ingawa Prof. Kabudi hakuwataja aliwaolenga katika hotuba yake hiyo, kauli yake huenda imelenga kuwaonya Watanzania wanaoikosoa serikali wakiwa nje ya nchi wakiwamo Mbunge wa Singida Mashariki na Mwanasheria Mkuu wa Chadema, Tundu Lissu (Ubelgiji), Mange Kimambi (Marekani) na Thobias Marandu (Marekani) ambao wamekuwa wakiikosoa waziwazi serikali ya awamu ya tano.



Prof. Kabudi pia alimshukuru Rais Magufuli kwa kumteua huku akimwelezea Waziri Augustine Mahiga ambaye sasa ni Waziri wa Katiba na Sheria, kuwa alimfahamu toka akiwa kidato cha kwanza na amekuwa mwalimu wake kwa muda mrefu.

Waziri Kabudi alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa miaka miwili, huku Waziri Mahiga akishika wadhifa wa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa miaka mitatu na miezi miwili.

Katika hotuba yake jana Ikulu, Waziri Mahiga, alisema nchi yoyote inakuwa na sura mbili; ya ndani ambayo ndiyo chimbuko la amani, uhuru, umoja, tabia na taswira ya taifa na ya nje ambayo sera ya mambo ya nje inakuwa kioo cha sera ya mambo ya ndani.

Alisema nchi yoyote ni lazima itafute, ijenge, ilinde na kuendeleza nafasi katika jumuiya ya kimataifa.

"Misingi ilishajengwa na Mwalimu Nyerere, leo tunaweza kusema hatuna adui duniani, tuna marafiki wengi, siasa yetu imetupa heshima na kuwa na misingi inayotufanya tusitetereke," alisema.

Alisema katika kutafuta nafasi kwenye jumuiya hizo, ni lazima iwe na malengo ambayo kwa Tanzania ni diplomasia ya uchumi ya kuielekeza Tanzania katika uchumi wa kati 2025 na uchumi wa viwanda.

"Nikiwa waziri, nimesimamia kuandika upya sera ya mambo ya nchi za nje ili kuonyesha mwelekeo na mbinu ya utekelezaji wa sera ya diplomasia ambayo itaipa Tanzania kuweza kuwa na uchumi wa kati," Dk. Mahiga alisema.

"Katika jumuiya ya kimataifa, vitu havikai bila kubadilika, unapolinda marafiki na kutengeneza ubia na ushirika, lazima uwe macho jinsi ya kuwashughulikia na kuwasiliana na mataifa mbalimbali."

Mahiga ambaye amekaa nje ya nchi akifanya kazi katika jumuiya za kimataifa kwa miaka 30, alisema kazi aliyopewa ilikuwa inafanana na kazi aliyoifanya nje tangu mwaka 1983 na kupata ujuzi mkubwa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324435
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa [illegible],
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,

04 - 03 - 2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 12-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es -Salaam** kuelekea **Singida**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 135 CCP / T 161 BDU**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 28 |
| Upana | - | mita | 3.7 |
| Kimo | - | mita | 5.4 |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Singida Kupitia Morogoro,**

gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

XXXXXXXX

HABARI KITAIFA

# Samia awapa tano wakulima wa Shy

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewapongeza wakulima wa mkoa wa Shinyanga kwa kuzalisha mazao ya biashara na chakula kwa wingi na kufanya mkoa kuwa na chakula cha akiba kulinganisha na mikoa mingine.

Samia aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara wilayani Kahama na kuelezea kufurahishwa kuona wakulima wengi mkoani Shinyanga wamejitokeza na kulima kwa wingi mazao ya chakula na biashara.

Alisema mkoa wa Shinyanga kwa msimu wa kilimo uliopita, ulizalisha mazao ya biashara na chakula zaidi ya tani 500,000 na kuufanya kuwa na akiba ya chakula kingi cha kutosha.

Makamu wa Rais aliwataka wakulima mkoani hapa kuendelea kulima kwa wingi na kuuza mazao yao katika nchi za jirani na kuongeza kilimo kimekuwa kikiwanufaisha wakulima wengi na kimekuwa kikiingizia nchi fedha nyingi za kigeni.



Mbali na uzalishaji huo, aliwataka kukata bima za afya kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa pindi wanapouza mazao yao na kupata fedha. Alisema hali hiyo itawafanya kumudu gharama za matibabu na kusababisha hospitali kuwa na dawa za kutosha, kwa kuwa fedha za bima ya afya zinatumika kununuliwa dawa na vifaa tiba.

Alisema kuwa, Wilaya ya Kahama ina zaidi ya kaya 49,437 kati ya hizo ni 9,000 pekee ndizo zilizokata bima ya afya ya CHF, huku kundi kubwa likibaki likitumia gharama kubwa za matibabu.

"Ndugu zangu wakulima, kateni bima za afya ili kumudu gharama za matibabu pindi mnapofika hospitalini kupatiwa huduma. Kumbukeni mnakunywa bia ngapi? Ni kiasi gani cha fedha mnapeleka nyumba ndogo na kwa nini mnashindwa kukata bima za afya? Alihoji Samia.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Inocent Bashungwa, alisema kutokana na mkoa wa Shinyanga kulima mazao mengi ya kibiashara, serikali ina mkakati wa kujenga kiwanda kikubwa cha usindikaji wa mazao Kanda ya Ziwa ili nchi za jirani za Rwanda, Uganda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrassi ya Congo zifike Kahama kununua mazao.

Alisema serikali imekuwa ikiwajali wakulima kwa kuwapelekea pembejeo kwa muda mwafaka ikiwa ni pamoja na kuwatafutia masoko ya kuuza mazao yao na kwamba kila mkulima ana wajibu wa kuuza mazao yake katika nchi za jirani ili kujiongezea kipato.

# Kampuni yapigwa 'stop' kusafirisha vinasaba

**Na Rose Jacob,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, imeipiga marufuku kampuni binafsi inayosafirisha vinasaba vya binadamu iliyoko mkoani Kagera.

Kampuni hiyo, Tutume, imepigwa marufuku kufanya kazi hiyo baada ya kubainika kuwa haina vibali vinavyoiruhusu kusafirisha vifurushi na vipeto. Pia ameipatia siku saba kuwasilisha vielelezo vinavyothibitisha kama imesajiliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Nditiye alisema hayo jana wakati akizungumza wa watumishi wa Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL) mkoani Mwanza na kusema kampuni hiyo inadaiwa kupokonya kazi zilizokuwa zinafanywa na Shirika la Posta.

Alisema Shirika la Posta liliingia mkataba na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kusafirisha sampuli za damu na vinasaba vingine kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kurejesha majibu na kujikuta likisimamishiwa kazi hiyo bila kujua chanzo chake.

**Natoa wito kwa kampuni yoyote inayojihusisha na usafirishaji, ihakikishe ina vibali. Kinyume cha hapo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao bila kujali wadhifa wa mtu.**

"Suala la kusafirisha damu na vinasaba ni nyeti sana na linahitaji kufuata sheria si watu kukaa na kufanya uamuzi kwa maslahi binafsi, hivyo hatuwezi kuruhusu hali ya namna hii iendelee hapa nchini.

"Natoa wito kwa kampuni yoyote inayojihusisha na usafirishaji, ihakikishe ina vibali. Kinyume cha hapo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao bila kujali wadhifa wa mtu," alisema Nditiye.

Aidha, Nditiye aliwatumia salamu za onyo watumishi wa TTCL makao makuu Tanzania wanaoingia mikataba hewa na isiyo na tija kwa kupeleka mawasiliano kwenye kampuni kubwa kwa kutumia mkono wa TTCL. Aliwataka watu wajiandae kuchukuliwa hatua na kusisitiza wasifanye hivyo na badala yake kila hatua ifuate sheria, kanuni na taratibu zote za kimikataba.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa Shirika la Posta Tanzania mikoa ya Mwanza na Geita, Phillipo Mchelle, alisema kwa mkoa wa Mwanza wanafanya vizuri, lakini mkoa wa Geita walihudumu kwa miezi mitatu tu wakaambiwa wasitishe huduma, hivyo bado wanaendelea kufanya mawasiliano na mganga mkuu wa mkoa huo ili wabaini kwa nini walisimamishwa.

"Tunampongeza mganga mkuu wa mkoa wa Mwanza kwa ushirikiano wake na tumeshakaa vikao kadhaa na watu wa AGPAHI na watu wa afya. Hakuna dosari katika kutekeleza hili la kusafirisha vinasaba na katika kupeleka majibu ya wagonjwa hospitalini," alisema Mchelle.

Naye Meneja wa TTCL, Jalili Senkopwa, alisema mara nyingi maeneo ambayo kunafanyika mchezo wa mikataba hewa ambao hauna afya wala tija yoyote ndiko shirika limewekeza kiasi kikubwa cha fedha.




Makamu Mwenyekiti wa Mawaziri wa Sekta ya Uvuvi wa nchi zinazozunguka Ziwa Victoria, Luhaga Mpina, akisaini makubaliano ya kufanya operesheni ya pamoja ya kukabiliana na uvuvi haramu katika Ziwa Victoria. Kushoto ni Waziri wa Kilimo, Wanyama na Uvuvi wa Uganda, Vincent Ssempijja. Kulia ni Katibu Mkuu Uvuvi wa Kenya, Prof. Micheni Ntiba. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Buhigwe yawezeshwa mil. 993/- elimu

**Na Magreth Magosso,** Kigoma

WAZIRI wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, amesema Sh. milioni 993.2 zimeelekezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe kutatua changamoto ya miundombinu ya elimu katika shule mbalimbali ikiwamo Shule ya Sekondari ya Janda.

Pia amewapongeza wakazi wa vijiji vya Janda na Kalungu kwa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya Janda, huku akimuhimiza mkuu wa shule hiyo kuendelea kuhamasisha wananchi katika kutatua kero za miundombinu.

Ndalichako alisema hayo jana wilayani Buhigwe alipotembelea shule hiyo ikiwa sehemu ya ziara yake mkoani Kigoma inayolenga kuongeza kasi ya kutatua kero na changamoto mbalimbali katika sekta ya elimu.

"Fedha hizo ni awamu ya kwanza tulizogawa katika wilaya kupitia programu ya lipa kulingana na matokeo. Tangu Januari 17, fedha ziko kwenye akaunti husika. Wewe ofisa elimu umepitwa na wakati umeomba fedha kwa Shule ya Msingi Muyama, Oktoba, 2017, lakini fedha ipo tangu Januari. Hebu fuatilia na tumieni fursa ya muda kutatua changamoto kwa fedha hizo," alisema.

Alisema serikali iko makini na ahadi zake na kuwataka wanafunzi wa kike wathubutu kuinua kiwango cha ufaulu dhidi ya wanafunzi wa kiume na kusisitiza changamoto ya uhaba wa walimu kwenye masomo ya sayansi isiwe kigezo cha kushindwa kuongeza ufaulu.

"Ufaulu wenu ni hafifu kwa watoto wa kike. Kwa miaka miwili 2017 na 2018 mfululizo, hakuna aliyefanya vizuri, wengi ni daraja la nne na sifuri hakuna daraja la kwanza. Pamoja na uhaba wa vitabu na walimu wa masomo ya sayansi, isiwe kigezo cha kushindwa kufaulu, ongezeni bidii msipende kuwezeshwa," alisema.

Awali, akisoma risala mbele ya waziri, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Janda, Sandel Kikombe, alisema wanakabiliwa na changamoto ya ufaulu duni kwa wanafunzi hususan wa kike.

Kikombe alisema mwaka jana wanafunzi waliofanya mtihani ni 36 na matokeo yake hakuna daraja la kwanza na katika daraja la pili kulikuwa na wavulana wawili tu, wakati daraja la tatu walikuwa wavulana watatu na wasichana wawili.

# Operesheni wauaji watoto, vikongwe yaja

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kigoma na chama cha waganga wa asili na wakunga wa jadi wanaotetea watu wenye mazingira hatarishi nchini (ASIDEP), wamekubaliana kuanza operesheni ya kubaini wahalifu wa mauaji ya watoto, vikongwe, wenye ulemavu wa ngozi na raia kwa ujumla.

Kauli hiyo imejitokeza mwishoni mwa wiki Halmashauri ya Kigoma Ujiji, kwenye jukwaa la waganga husika lilioshirikisha Jeshi la Polisi, wenyeviti wa mitaa, madiwani kwa lengo la kulaani mauaji ya watoto na raia kwa ujumla na namna ya kudhibiti mauaji hayo.

Mwenyekiti wa ASIDEP, Abdallah Joseph, amekiri kuna baadhi ya watu wanaotumia kivuli cha waganga wa jadi na tiba za asili kinyume cha taratibu na sheria za kitabibu.

"Ili kubaini wahalifu tuanze operesheni ya kuwatambua waganga wote na kukagua kazi zao, watakaobainika wanavunja sheria kwa matumizi yasiyo halali ya tiba na nyara za serikali mfano wasiosajiliwa kisheria, hata wanaovaa kofia mbili wauaji wanaojiita waganga watawajibishwa," alisema Joseph.

**Polisi haiwezi kubaini wahalifu bila wananchi, miongoni mwenu hutoa dawa kwa wahalifu tusiwakamate, sasa ili kurudisha hadhi yenu mjipambanue kwa uwazi shughuli zenu, acheni ramli chonganishi.**

Alisisitiza kuwa, waganga feki ndio chanzo cha kuongezeka kwa mauaji ya watoto na raia, lakini kwa ushirikiano na jeshi hilo ni chachu ya mabadiliko kwa waganga kufanya kazi kwa uaminifu kutokana na zoezi lijalo la kuwafichua wachawi waliojificha kwa kivuli cha uganga.

Aidha, ameilaumu Idara ya Afya ya manispaa hiyo kwa kuwatenga waganga hao kiutendaji na kuwaona wote ni wauaji, badala ya kuwaelimisha kwa kuwa shughuli zao zinashabihiana na mlengo mmoja wa kutibu wagonjwa.

Akifafanua ushirikiano huo kwa niaba ya Kamanda wa Polisi Mkoa, Martin Ottieno, Ofisa Operesheni ASP Gida Saida, alithibitisha kushirikiana na ASIDEP katika kuimarisha ulinzi wa watu na mali zao.

"Polisi haiwezi kubaini wahalifu bila wananchi, miongoni mwenu hutoa dawa kwa wahalifu tusiwakamate, sasa ili kurudisha hadhi yenu mjipambanue kwa uwazi shughuli zenu, acheni ramli chonganishi, mnaotumia ngozi za wanyamapori kateni kibali cha umiliki wa ngozi hizo kabla ya operesheni maalum dhidi ya waganga wote," alisisitiza ASP Saida.

Mwanachama wa Asidep, Abed Awadhi, alisema watu wa Kigoma hawana tabia ya kutumia binadamu kama tiba, lakini kabla ya operesheni ya kubaini waganga na vifaa vyao wapewe elimu elekezi ya namna ya kupata kibali cha kumiliki ngozi za wanyamapori kwa nia ya kutoa tiba kwa mujibu wa sheria husika.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Rusimbi, Bakari Songoro, alisema atahakikisha waganga waliopo katika mtaa wake wanafanya kazi kwa weledi kwa kuzingatia vibali mtambuka hasa cha umiliki wa ngozi za wanyama aina ya chui, simba kwa tija ya kutii sheria bila shuruti kwa ustawi wa jamii na taifa kiujumla.

Wakati huo huo Mkunga wa Jadi Mariam Juma, amesema pamoja na kusaidia wajawazito kujifungua katika vituo vya afya, wamekuwa wakitolewa lugha chafu na watumishi wa idara ya afya ilhali wanaokoa uhai wa mama na mtoto katika mazingira magumu hasa waishio nje ya mji wa Kigoma mjini na kuikumbusha serikali ithamini uwepo wao.



Dereva wa Bodaboda akiwa amebeba abiria wawili huku wakiwa hawajavaa kofia ngumu ya kichwani katika Barabara ya Morogoro, eneo la Manzese, jijini Dar es Salaam jana kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali kupiga jeki utalii wa kitamaduni

**Na Lusungu Helela,** MTWARA

SERIKALI ya Tanzania imeanza mkakati maalum wa kuinua utalii wa kiutamaduni na wa kihistoria kwa kuvigawa vituo 16 vya Malikale kwa taasisi za uhifadhi nchini.

Lengo likiwa ni kuziwezesha taasisi hizo ziweze kuvikarabati na kuvisimamia ili kuchangia pato la taifa kupitia sekta ya utalii nchini.

Hatua hiyo imekuja baada ya serikali kupitia upya sera ya malikale ya namna ya kuyahifadhi maeneo hayo kufuatia changamoto za kifedha zinazoikabili Idara ya Malikale na kufanya majengo mengi ya kale na ya kihistoria kuwa katika hali mbaya ya uchakavu.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, wakati alipotembelea mji wa kihistoria wa Mikindani uliopo katika Manispaa ya Mikindani katika Mkoa wa Mtwara ambao kwa sasa eneo hilo linasimamiwa na kuendeshwa na Taasisi ya Makumbusho ya Taifa.

Aidha, alisema uamuzi huo wa serikali umeifanya changamoto ya kifedha iliyokuwa ikiikabili idara hiyo kutatuliwa na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Hifadhi za Taifa (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Makumbusho ya Taifa (NMT), pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Alisema taasisi hizo zitakuwa na jukumu la kusimamia, kukarabati, kuendeleza, kuendesha pamoja kutangaza vituo hivyo vyenye utajiri mkubwa wa kihistoria na kiutamaduni.

Kwa mujibu wa tathmini ya ukaguzi iliyofanyika mwaka jana, jumla ya majengo 85 ya kihistoria yalikuwa hatarini kudondoka na kupotea kama yasingekarabatiwa.

Kufuatia hali hiyo, Kanyasu alisema taasisi hizo zitasaidia kuyakarabati majengo hayo ili yaweze kurudi katika hali yake ya mwanzo na kuwa kichocheo cha utalii.

Akizungumzia mkakati wa kutangaza vivutio hivyo vya Malikale, Kanyasu, alisema vitakuwa vikitangazwa kwa mfumo wa vifurushi ili kuwawezesha watalii wanapokwenda Mtwara waweze kutembelea vivutio vingi vilivyopo katika mkoa huo kwa vile ni ngumu kwa mtalii kwenda Mtwara kwa ajili ya kutembelea mji wa Mikindani pekee.

"Tunataka vivutio vya utalii vya Kusini na maeneo mengine ya nchini yawekwe kwenye vifurushi ili mtalii akipanga kwa mfano kutembelea mkoa wa Mtwara atembelee Pori la Akiba la Lukwika Lumesule, akitoka hapo atembelee majengo ya kale, ajionee vikundi vya ngoma za asili kisha aende akapumzike kwenye fukwe zetu nzuri," alisema.

# CCM Ruvuma yajipanga uchaguzi serikali mitaa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Ruvuma, Jimson Mhagama, amesema kupitia makatibu wake wa kata wamejipanga kuhakikisha mitaa yote 95 ya Songea mjini inachukuliwa na CCM kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu.

Alisema CCM ni chama ambacho kimekuwa kikitekeleza ilani yake ya uchaguzi kwa vitendo kwa kuwafuata wananchi kusikiliza kero na changamoto zao zinazowakabili na kuzitatua na wananchi wanaendelea kukiamini kutokana na kuwa na mshikamano wa pamoja kati ya wanachama na viongozi wao.

Alisema hayo juzi mjini hapa, wakati alipokutana na makatibu wa kata wa Wilaya ya Songea Mjini kuwa bila ya kuwa na umoja na mshikamano wa pamoja kati ya wanachama na viongozi wake, CCM isingeweza kufikia hapa ilipo kutokana na sera zake nzuri zenye kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Aliwaagiza makatibu hao wahakikishe wanawabana viongozi wa serikali kwenye kata zao na miradi ya maendeleo pamoja na kupata taarifa sahihi za utekelezaji wa kazi za miradi ili ikifikia muda wa kampeni za serikali za mitaa mwaka huu, kupita kuwanadi wagombea tiketi ya CCM viongozi wawe na cha kuwaelezea wapigakura kwa kila kata.

Alisema serikali ya CCM, Mwenyekiti wa Taifa, Rais Dk. John Magufuli amekuwa akihimiza kila Mtanzania achape kazi kwa kutumia kaulimbiu yake ya "Hapa kazi Tu" na kuwahimiza makatibu hao wafanyekazi ya kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Ilani ya CCM kwenye miradi ya maendeleo kwenye kata zao.

Aliwakumbusha kuwa sera hiyo imekuwa ikiwabaini mafisadi na wahujumu uchumi ambao wana tabia ya kujinufaisha kwa kujipatia fedha za miradi inayotolewa na serikali na nguvu za wananchi, alijigamba kwa kusema sera hiyo ndio ushindi mkubwa wa CCM kwa kuwa wapinzani watakosa na kubaki kuendelea kusema uongo.

# Wanne kortini kwa kukwepa kodi, kughushi nyaraka

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Manyara, imewafikisha mahakamani watu wanne kwa kosa la kukwepa kulipa kodi na wengine kwa kughushi nyaraka.

Naibu Mkuu wa Takukuru, mkoani Manyara, Isidory Kyando, aliwataja waliofikishwa mahakamani kuwa ni wakili wa kujitegemea, Samson Rumende, aliyekuwa Ofisa Wanyamapori wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Nashon Macokecha, aliyekuwa Kaimu Katibu wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge (Juhibu), Francis Mwasombele, na Mwenyekiti wa Kijiji cha Vilima Vitatu, Erasto Belela Kou.

Alisema washtakiwa hao wanne wanashtakiwa kwa kosa la kukwepa kodi kinyume cha Sheria ya Magari (ushuru wa usajili namba 124/2006) kifungu cha 15 (b).

Alisema washtakiwa hao wote wanne walishtakiwa kwenye kesi hiyo namba 3/2019 iliyofunguliwa Februari 22, mwaka huu, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Hata hivyo, washtakiwa wawili, mshtakiwa wa kwanza Macokecha na mshtakiwa wa tatu, Mwasombele hawakuweza kufika mahakamani hapo na hakimu akatoa hati za wito kwa washtakiwa hao.

Alisema mshtakiwa wa pili Kou na wanne wakili wa kujitegemea Rumende wanashtakiwa kwa kughushi nyaraka katika kesi hiyo.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Aprili 4, mwaka huu, ambapo itaendelea tena mahakamani hapo kwa hatua ya kutajwa.

# Maharage lishe mkombozi kwa wajawazito Mbulu

**Na Allan Isack,** MBULU

TAASISI za utafiti wa mbegu na mazao ya kilimo ya TARI na CIAT, zimebaini kuwa maharage lishe yanaongeza nguvu za kiume na damu kwa wajawazito kutokana na kuwa na madini joto na chuma.

Wakizungumza wakati wa ziara ya kutembelea wakulima wa maharage lishe, wilayani Mbulu mwishoni mwa wiki iliyopita, wataalamu kutoka katika taasisi hizo, Radegunda Kessy (CIAT), na Denis Mcharo (TARI), walisema kutokana na maharage lishe kuwa na madini joto na chuma wamekuwa wakiwahamasisha wananchi kulima kwa wingi maharage hayo.

"Maharage lishe yanaongeza damu kwa wajawazito na kwa upande wa wanaume yanaongeza nguvu za kiume kwa sababu yana virutubisho vya madini joto na chuma," alisema Radegunda.

Aidha, walisema wakulima wengi vijijini hawalimi maharage hayo kwa wingi kutokana na kutokuwa na elimu mtambuka ya umuhimu wa maharage lishe.

**Soko la maharage lishe ni la uhakika na kilimo hiki kinamwondoa mkulima katika umaskini kutokana na maharage haya kuwa tofauti na mengine na kuwa na bei yenye kukidhi haja ya wakulima.**

"Tumekuwa tukitoa elimu kwa wakulima lengo likiwa kuhakikisha wakulima vijijini wanazalisha maharage haya kwa ajili ya kuongeza wigo wa uzalishaji wa zao hili ambalo ni muhimu kwa chakula na biashara," aliongeza Mcharo.

Julita Cosmas na Rose Sipirian, wakazi wa Kijiji cha Moringa Kata ya Daudi, walisema maharage hayo, hayana gesi kwa matumizi ya binadamu pia yanastahimili ukame na jua.

Hata hivyo, walisema maharage hayo, yakipikwa yanaiva ndani ya dakika 15 ikilinganishwa na maharage mengine ya kawaida.

Licha ya kuzungumza hayo, walisema kilimo cha maharage lishe kina faida kwa wakulima wa Mbulu kutokana na kuwa na soko la ndani na nje ya nchi, hivyo wakulima wanaongeza kipato.

"Soko la maharage lishe ni la uhakika na kilimo hiki kinamwondoa mkulima katika umaskini kutokana na maharage haya kuwa tofauti na mengine na kuwa na bei yenye kukidhi haja ya wakulima," alisema.

Ofisa Kilimo na Uvuvi wa Halmashauri ya Mbulu, Mosses Nduliku, alisema kilimo cha maharage ndiyo kilimo kinachochangia kiasi kikubwa cha mapato katika halmashauri hiyo.

"Kilimo cha maharage kinalimwa kwa asilimia 70 katika Wilaya ya Mbulu na kinachangia pato la halmashauri yetu kwa asilimia 85, kwa mantiki hiyo tunatoa kipaumbele kwa kilimo cha maharage haya," alisema.

Abel Baida, Wakala wa Mbegu na Pembejeo wilayani humo, alisema amekuwa akisambaza mbegu za maharage kwa wakulima vijijini kwa muda mrefu ili kurahisisha upatikanaji wa mbegu na dawa kwa wakulima.

Akizungumzia utofauti wa mbegu za kawaida na za kisasa za maharage, Baida alisema mbegu za kisasa uzao wake ni mkubwa kuliko za kawaida, ambapo hekari moja ya mbegu za kisasa mkulima anavuna gunia nane mpaka 10, lakini kwa upande wa mbegu za kawaida mavuno yake ni kati ya guni mbili hadi nne.

Aliongeza katika usambazaji wa mbegu, mbolea na dawa ameshawafikia wakulima kutoka Wilaya za Hanang, Babati Mjini, Mbulu, Karatu na Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida.



Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Leonard Maboko, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mauaji ya wanawake yaibua wadau kulea wazee

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

TISHIO la wanawake wazee kuuawa katika eneo la Mto wa Mbu wilayani Monduli, limeibua harakati za wadau kuanzisha Shirika la Uzee na Furaha la kulea wazee na kutetea haki za wanawake dhidi ya ukatili na mauaji.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa shirika hilo, Jackline Samson, alisema kwa kushirikiana na marafiki zake wa nchini Ireland wameamua kuwasaidia wazee wanawake na wanaume ambao wanataabika katika mji huo.

Alisema kwa kuanzia zaidi ya wazee 20 wameanza kupewa huduma mbalimbali majumbani baada ya kutambuliwa na baadaye wale wasio na ndugu watapata hifadhi.

"Tayari tumejenga jengo maalum la kuwasaidia wazee, kwa sasa tunawapa huduma za afya na chakula majumbani na taratibu zikikamilika ikiwepo upatikanaji wa fedha baadhi tutawahamishia kituoni," alisema.

Fatuma Adam (86), mkazi wa Mto wa Mbu Mnadani ambaye hivi karibuni, alinusurika kuuawa na vijana wanaofanya matukio ya ukatili, alisema wanashukuru kwa misaada inayotolewa na kituo hicho cha kulea wazee.

"Mimi nilifanyiwa ukatili na hadi sasa nimekuwa napatiwa matibabu tunashukuru Mungu kupatiwa msaada wa huduma za afya na chakula na tunaomba usaidizi zaidi, lakini pia polisi wakamate wahusika wanaotuwinda," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii, Tarafa ya Manyara, Swedi Kiluvia, alisema kuanzishwa kwa kituo cha kulea wazee katika mji huo ni faraja kwa wazee kwa kuwa sasa watakuwa na uhakika wa maisha yao.

"Tatizo lipo, tuna idadi kubwa ya wazee ambao walikuja miaka mingi iliyopita katika mji huu kufanyakazi na baadhi hawana ndugu sasa wamekuwa wakihangaika kujimudu kuimaisha," alisema.

Kufuatia mauaji ya wanawake katika mji huo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kange Lugola, alilazimika kuingilia kati Julai mwaka jana kwa kulitaka Jeshi la Polisi mkoani Arusha, kufanya uchunguzi wa kina na kuwabaini watu wanaohusika kufanya vitendo vya ubakaji na mauaji kwa wanawake na wazee.

# Komu azungumzia maisha mapya ya Lowassa CCM

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MBUNGE wa Moshi Vijijini, Athony Komu, amesema Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa amerejea Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa sababu anajua kucheza vizuri na msemo wa Waingereza usemao, ukishindwa kupigana nao, ungana nao.

Komu ametoa kauli hiyo jana kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Facebook na Whatsapp, kuhusiana na kauli ya Lowassa kwamba ataweka wazi sababu zilizomwondoa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na kurejea CCM.

"Mimi nafikiri tumtakie safari njema, huenda amechoka, hawezi tena siasa ngumu, akachagua ule msemo wa Waingereza usemao ukiwashindwa jiunge nao. Sisi hatujawashindwa, pia hatujachoka, hivyo basi rai yangu ni kuendeleza mapambano bila ya kuyumba na kutumia muda kugombana na historia," alisema mbunge huyo.

**Mimi nafikiri tumtakie safari njema, huenda amechoka, hawezi tena siasa ngumu, akachagua ule msemo wa Waingereza usemao ukiwashindwa jiunge nao.**

Lowassa kabla ya kuhama Chadema wiki iliyopita, alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu na alitangaza kukihama chama hicho kikuu cha upinzani nchini Ijumaa iliyopita na kurejea chama tawala akipokewa na viongozi wakuu wa CCM walioongozwa na Mwenyekiti, Dk. John Magufuli.

Mwaka 2015 wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, Lowassa alikuwa mgombea kiti cha urais kupitia Ukawa.

Alipewa ridhaa hiyo na vyama vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi, baada ya jina lake kuenguliwa kwenye mchakato wa kumpata mgombea wa urais katika Chama Cha Mapinduzi.

Lowassa ambaye ni Waziri Mkuu wa kwanza kuhamia upinzani katika historia ya Tanzania, alitangaza kujiengua CCM Julai 28, mwaka 2015.

Katika uchaguzi huo, Lowassa aligombea nafasi ya urais kupitia Ukawa ambayo iliundwa na Chadema, CUF, NCCR Mageuzi na NLD.

Akiwa mgombea wa Ukawa, alipata kura 6,072,848 (sawa na asilimia 39.97) akiwa nyuma ya Dk. John Magufuli aliyetangazwa mshindi kwa kupata kura 8,882,935 (asilimia 58.46).



Mwanafunzi wa kidato cha sita Shule ya Sekondari ya Tabora Boys, Daud Costantine (kulia), akionyesha mashine ya kutengenezea gundi kwa kutumia mabaki ya maboya kwa kuchanganya na mafuta ya taa, wakati wa nusu fainali ya mashindano ya kitaifa ya sayansi na ubunifu kwa shule za sekondari, yaliyoandaliwa na Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Shule ya Feza, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# DC atoa siku 21 kupitia majalada ya walimu

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amempa siku 21, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo na watendaji wake wa idara ya utumishi kufanya ukaguzi maalumu wa majalada yote ya walimu ambao wana madai mbalimbali, ili kubaini kama kuna waliocheleweshwa kwa makusudi kupandishwa madaraja, awapandishe haraka.

Pia, ametaka wanaodai stahiki zao ikiwamo mishahara, wawe wamelipwa ndani ya wiki tatu, ili kuwapa motisha zaidi ya kuipa heshima wilaya hiyo katika matokeo ya mitihani ya kitaifa ya darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita. Sabaya ametoa agizo hilo, baada ya kukutana na kufanya mazungumzo ya saa mbili na walimu wakuu wa shule za msingi, sekondari, waratibu wa elimu kata, watendaji wa vijiji, kata na maofisa elimu katika kikao kazi cha siku moja.

"Watu wa utumishi, ofisa utumishi uko hapa, mkurugenzi uko hapa. Sasa ili tupate uhalali wa kazi wanayoifanya walimu hawa, walipeni stahili zao na kama ni madaraja, naagiza nendeni mkakague mafaili yote hayo kuanzia sasa na walio kazini muda mrefu wapandisheni madaraja wale wanaostahili. Nakupa siku 21 walimu wote wenye madai yao wapate haki yao," aliagiza.

Alisema mwalimu ni mtu muhimu katika ujenzi wa taifa, kwa kuwa kila mtu lazima apelekwe shule ili aweze kupata elimu na asilimia 90 ya malezi ya watoto ni walimu na sio mzazi.

Kuhusu taarifa za walimu wanne wanaotuhumiwa kwa ulevi uliokithiri, Sabaya ameeleza kuchukizwa kwake na hali hiyo na kutoa onyo kwao kwamba iwapo wataendelea na tabia hiyo wataingia matatani dhidi ya mwajiri.

"Mimi nimewaita kuwaelekeza mambo machache, na wakati nakuja hapa, nimepata taarifa za baadhi yenu, sifurahii sana kusikia mwalimu ni mlevi.

# Waziri Mwakyembe akerwa ufinyu wa barabara

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amempa somo Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, akimtaka 'achakarike' haraka kutengeneza andiko la kuomba kufanyika kwa upanuzi wa barabara iendayo Hospitali ya Rufani ya KCMC hadi YMCA, ili kuruhusu shughuli za kijamii kufanyika bila bughudha nyingine.

Mwakyembe amemshauri Mboya kufanya hivyo muda mfupi ujao na kulipeleka andiko hilo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), akieleza umuhimu wa shughuli za kijamii zinazofanyika kila mwaka kupitia barabara hiyo yakiwamo mashindano ya kimataifa.

Alimpa ushauri huo baada ya kumalizika kwa mbio za Kili Marathon za mwaka 2019, ambazo zilikusanya zaidi ya wanariadha 10,000 wa ndani na wa nje ya nchi.

"Nimeambiwa kwamba imebidi wakimbiaji wengine mamia kwa mamia, wazuiwe kushiriki kwa sababu ya barabara ya KCMC inayotumika ni nyembamba. Mstahiki Meya (Mboya), uko hapa naomba andikeni andiko mkionyesha umuhimu wa barabara hii namna inavyoingiza watalii wengi wa kimataifa wanaokuja katika mashindano," aliagiza Waziri Mwakyembe.

Barabara hiyo ya KCMC, pia ndio inayoongoza katika mji wa Moshi kwa kuwa na idadi kubwa ya abiria wanaokwenda na kutoka hospitali ya rufani ya kanda, vyuo vikuu vinne vya Mwenge, Ushirika, KCMCo na Chuo cha Kimataifa cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori cha Mweka.

Mwaka ujao, barabara hiyo itatumika kwa ajili ya mshindano ya Mbio za Nyika za Bara la Afrika ambazo zinatarajiwa kufanyika katika mji wa Moshi zikishirikisha nchi 54.

Pia, barabara hiyo hiyo itatumika kwa ajili ya mbio za kimataifa za Kili Marathon ambazo hufanyika kila mwaka, lakini pia itatumika tena kwa maonyesho ya kimataifa ya Karibu Kili Fair 2020 yanayotangaza utalii wa Tanzania duniani.



Baada ya agizo hilo la waziri, Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, alimweleza Mwakyembe kuwa amelipokea wazo hilo na kuahidi kulifanyia kazi, ingawa alishalifikisha suala hilo katika Kamati ya Ushauri ya Maendeleo ya Mkoa (RCC).

"Ni kweli ni ninafurahi waziri ameliona hili, baada ya wanariadha wengi kuzuiwa kukimbia kutokana na vigezo vya kimataifa. Barabara hiyo imebeba sura ya taifa letu, achilia mbali hospitali. Tutazungumza na Tarura (Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini) na Tanroads (Wakala wa Barabara nchini) kuona tunatekelezaje agizo hili. Tayari tulishatoa amri waliojenga barabarani wavunje," alisisitiza meya.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 5, 2019
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?
MAHARAGE YA NYAMA KUTOKA KWA WATURUKI



## Miradi mipya yabadili upepo wa elimu wilayani Simanjiro

Ukurasa 15




# Wanafunzi Ngurdoto walipolipuka kufurahia ugeni wa umeme Sola

Ukurasa 16



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Achezeaye tope humrukia

"MTU anayecheza na tope huishia kuchafuliwa nalo." Hii ni methali ya kuwakanya watu dhidi ya kuandamana au kuhusiana na watu wenye sifa mbaya. Anayehusiana na mtu mbaya huishia kuambukizwa ubaya huo.

Aidha, "Adui wa mtu ni mtu" kwani binadamu huhasiriwa na binadamu mwenzake. Methali hii yatukumbusha kuwa aghalabu matatizo tuyapatayo husababishwa na watu tunaoishi nao kila siku.

'Iga' (igwa, igia, igiza, igizana, igizika) ni kitendo cha mtu kufanya jambo kwa namna ile ile iliyofanywa na mtu mwingine. 'Igiza' ni kufanya jambo kwa kufananisha na jingine (Bara) jengine (Zanzibar).

"Yanga waliamsha dude Mbeya" ni kichwa cha habari kwenye moja ya magazeti ya michezo nchini. Neno 'dude' lilianzishwa na gazeti moja la michezo na sasa latumiwa na magazeti yote ya michezo! Iga, igiza, igizana.

Hilo 'dude' lililoamshwa Mbeya lilikuwa limelala wapi? Kwa mujibu wa Kiswahili fasaha, 'dude' ni kitu kikubwa kisichojulikana; dubwana. Pia ni mtu anayedharauliwa; lakabu ya kuonesha dharau kwa mtu mwingine.

Ina maana timu iliyopambana na Yanga ni 'dude' au ni 'jina' la utani badala ya Tanzania Prisons ambalo ndilo jina lake halisi?

Moja ya sentensi za habari inayohusu mchezo huo iliandikwa: "Rekodi hiyo ndiyo iliyoibua hasira kwa Prisons na kupanga kucheza kufa na kupona kuhakikisha inajiongezea pointi ili ijinasue kutoka mkiani."

Kwa Kiswahili fasaha haisemwi "kucheza/jitahidi kufa na kupona" bali ni "kucheza/jitahidi kufa au kupona." Haiwezekani mtu acheze/ajitahidi "kufa na kupona" yaani afe na wakati huohuo apone!

"Kaimu Mwenyekiti wa Yanga, Samweli Lukumay, alisema kwa timu yao imeondoka jana mchana kwenda Mbeya kwa usafiri wa ndege, nia yao ikiwa ni kuendeleza ubabe dhidi ya Prisons na kuzidi kujikita kileleni."

Sentensi hiyo ningeihakiki (kitendo cha kuchambua maandishi, hasa kazi za fasihi; kuthibitisha uhalisi wa kitu) hivi:

"Kaimu Mwenyekiti wa Yanga, Samweli Lukumay, alisema timu yao iliondoka jana mchana kwa ndege kwenda Mbeya kwa lengo la ushindi na kuwa kileleni." Nimeacha 'ubabe' kwani maana yake ni ujanja na hila za kutumia nguvu; tendo la dhuluma na uonevu. Yanga haikwenda Mbeya 'kibabe.'

Ukurasa huohuo kulikuwa na kichwa kilichoandikwa: "Mtibwa wakwe pipaa kuivaa Dynamo" kikifuatiwa na maelezo yafuatayo:

"Kikosi cha Mtibwa Sugar kinatarajia kuondoka nchini kibabe kuelekea Shelisheli kwa ajili ya kuwafuata wapinzani wao, Northern Dynamo, kikiwa na wachezaji 18 kwa ajili ya mchezo wa marudiano uliopangwa kufanyika Jumanne ya wiki hii."

Hebu tusaidiane: "Mtibwa wakwe pipaa kuivaa Dynamo" inaashiria (toa ishara; onesha dalili, toa maana ya kitu) nini? 'Mkwe' ni umoja wa 'wakwe' na maana yake ni baba au mama wa mume au mke wako; mume au mke wa mwana wako au binti yako.

Bila shaka mwandishi alikusudia neno 'wakwea' na si 'wakwe' ingawa hata hivyo si mahala pake. 'Kwea' ni kitendo cha kupanda juu ya kitu; kwenda kwa kuelekea sehemu ya juu ya kitu kama mti au mlima.

Ili kuendeleza upotoshaji wa maneno ya Kiswahili, mwandishi aliandika 'pipaa' akimaanisha ndege! Wengine huandika 'pipa' eti kwa maana ya 'ndege!'

'Pipa' ni chombo aghalabu kirefu na duara ambacho maji na mafuta hutiwa; tangi. Ndege si 'pipa.' Ingawa latumiwa sana magazetini, neno hilo si rasmi kwa Kiswahili fasaha.

'Kibabe' ni neno linalotumiwa sana na magazeti ya michezo kumbe ni kupotosha maana yake kama nilivyoeleza huko juu.

'Vaa' ni: i) Funika mwili kwa nguo; weka mapambo katika sehemu ya mwili: vaa saa, mkufu, ushanga, pete. ii) Kibao kwenye chombo cha bahari kama dau, mashua au jahazi kitumikacho kufungia tanga (kitambaa kinachopachikwa kwenye mlingoti wa chombo cha majini ili kitege upepo wakati wa kukiendesha.)

Maana nyingine ya 'vaa' ni kitendo cha kumwingia mtu mwilini; vamia au kitendo cha kumrukia mtu kwa maneno Kwa hiyo timu za mchezo wowote 'hazivaani' bali hupambana, hushindana.

Hivyo "Mtibwa wakwe pipaa kuivaa Dynamo" ingeandikwa "Mtibwa yaifuata Dynamo kwao."

Gazeti hilohilo lilikuwa na habari hii: "Mkutano huo ulikuwa na ajenda mbili, kupewa sababu za kutofanyika mkutano na pia masuala mazima ya uchaguzi."

'Masuala' ni wingi wa 'suala' na maana yake ni mambo yanayohitaji kujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi. "Masuala mazima ya uchaguzi" maana yake nini? Ingeandikwa "suala la uchaguzi" badala ya kuongeza neno 'mazima' lisilokuwa na maana yoyote!

Msomaji mwenye namba 0766 192 021 alinitumia ujumbe ufuatao: "Mwal. Nisaidie tofauti ya 'usafiri' na 'usafirishaji.' Awali ya yote napenda kumfahamisha kuwa mimi si mwalimu kama adhaniavyo bali najitolea kusahihisha maneno yanayotumiwa tofauti na maudhui yake.

'Usafiri' ni chombo kinachochukua watu (abiria) au vitu (mizigo) kutoka sehemu moja hadi nyingine. 'Usafirishaji' ni tendo la kupeleka watu au mizigo kutoka pahali pamoja hadi pengine kwa kutumia chombo cha usafiri.

Gazeti hili unalosoma sasa liliandika kichwa: "Mshindi bajaj SportPesa apagawa. Akizungumza baada ya kukabidhiwa bajaj yake, Malick alisema ulikuwa ni wakati wa historia katika maisha yake baada ya kuiona timu ya SportPesa ikimfuata mpaka nyumbani mwake kwa lengo la kumkabidhi na hakuamini macho yake mpaka aliposhuhudia akikabidhiwa ndipo alipopiga shangwe za ushindi."

'Pagawa' ni kupandwa na pepo, pandwa na shetani. Kichwa kilichoandikwa na mwandishi wa habari husika hakikuwa sahihi. Katika habari yake hakuna popote alipoandika jinsi mshindi alivyopandwa na pepo/shetani!

**Methali: Usilolijua ni usiku wa kiza.**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

## ELIMU KUTOKA POLISI



Kamishna wa Polisi (DCP) Ahmed Msangi. **PICHA: MTANDAO**

# Wananchi acheni tabia ya kujichukulia sheria mkononi

KUJICHUKULIA sheria mkononi ni kitendo cha kuadhibu mtu aliyefanya kosa bila ya kufuata utaratibu wa sheria za nchi. Vitendo vya wananchi kujichukulia sheria mkononi vimekuwa vikikithiri siku hadi siku na kuleta madhara kwenye jamii yetu, ingawa tunashukuru juhudi kubwa ambazo zimekuwa zikichukuliwa na taasisi zinazohusika katika kuzuia hali hiyo isiendelee kutokea hapa nchini.

Vitendo hivi vya wananchi kujichukulia sheria mkononi vimekuwa vikijitokeza huku sheria ikiwa inakataza wananchi kutoa adhabu na badala yake watuhumiwa wapelekwe kwenye vyombo vya sheria vinavyohusika.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Ahmed Msangi, katika mahojiano na mwandishi wa makala haya alieleza kuwa jambo la kujichukulia sheria mkononi halikubaliki popote pale duniani na hata kwenye vitabu vya dini imekatazwa kutoa uhai na kuhukumu mtu pasipo kufuata sheria zilizowekwa katika nchi pamoja na kufuata misingi ya utawala bora na haki za binadamu.

"Nchi yetu inafuata misingi ya utawala bora hivyo hakuna mahala popote duniani ambapo utawala bora unakubali kutoa roho ya mtu bila kufuata utaratibu, vitendo hivi havikubaliki" alisema DCP Msangi.

Jambo lolote au mgogoro wowote duniani suluhisho lake ni kufanya mazungumzo ya amani kwa pande zote zinazokinzana. Hii ndio njia pekee ya kutatua yale yote yanayomkera mtu kwa kufuata taratibu za majadiliano yenye manufaa kwa jamiii.

Serikali za Mitaa zimepewa mamlaka ya mambo matatu ambayo ni kushughulikia uchumi, ustawi wa jamii na ulinzi na usalama ambapo kwa kupitia kamati zake tatu mambo hayo yanatekelezwa hivyo ndizo zinazopaswa kutumiwa na wananchi katika kutatua migogoro yao kwakuwa zina nguvu hasa kwa kufanya mazungumzo ili kuepuka kujichukulia sheria mkononi.

Naibu Kamishna Msangi aliongeza kuwa kwakuwa zipo njia za utatuzi wa migogoro, sisi kama Polisi hatutakuwa na huruma ama upendeleo kwa wale wote ambao watakuwa wanavunja sheria, kanuni na taratibu ili kuhakikisha kunaweqpo na usalama na amani.

Kwa kauli hizo ndipo wajibu wa kila mmoja unapoonekana hasa kwa kila mtu kutekeleza wajibu wake katika kulipinga jambo hili la watu kujichukulia sheria mkononi.

Mchango wa viongozi wa dini ni kufanya doria za kiroho ili kuepukana na jukumu la kujibu mbele ya mwenyezi Mungu, na viongozi wa serikali wanawajibu wa kujibu na kukemea vitendo vinavyoendelea ambavyo havifuati utaratibu wa sheria.

Wananchi kwa namna moja ama nyingine hawana budi kufuata sheria za nchi kwa kuwakamata wahalifu na kuwakabidhi kwa Jeshi la Polisi ama mamlaka zingine za kisheria ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria badala ya kuwaadhibu jambo ambalo linaweza kusababisha majeruhi hata mauaji kwa watuhumiwa.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

# ELIMU

NA NOVATUS MAKUNGA

# Miradi mipya yabadili upepo wa elimu wilayani Simanjiro

- Kila mzazi aota mtoto kuona sekondari
- Shule ya mwisho mkoa sasa 'usipime'
- ECLAT yageuza Emboret kata ya hamasa

Ni ukweli usiokuwa na shaka, elimu ina nafasi kubwa ya kubadilisha kwa kasi jamii yoyote. Ni hali inayojidhihirisha kwa jamii ya wafugaji wa Kimasai, katika kata ya Emboret wilayani Simanjiro, mkoani Manyara.

Mabadiliko hayo yanajitokeza kwa kasi kubwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, baada ya kuimarika kwa shule ya sekondari ya Kata ya Emboret, ambayo wananchi wake walianza kuijenga kwa nguvu zao tangu mwaka 2008, ikiwa na wanafunzi 40 tu.

Ilikuwa kipindi cha vuguvugu za ujenzi wa shule za kata uliofanywa na serikali ya awamu ya nne, wananchi walijenga jengo moja na serikali ikajenga lingine na sekondari zilianza hivyo, huku kwa matokeo ya kuhitimu elimu ya sekondari, ikishika nafasi mbaya.

Shule ya Sekondari Emboret, ilianza kuimarika mwaka 2015 mara baada ya shirika lisilokuwa la kiserikali la ECLAT Development Foundation, kujiingiza rasmi kuimarisha miondombinu ya shule hiyo.



Baadhi ya madarasa ya shule za msingi, Kata ya Emboret, wilayani Simanjiro. **PICHA ZOTE: NOVATUS MAKUNGA**

**VIVUTIO UMEME, MAJI, KOMPYUTA**

Miongoni mwa mabadilko yaliyoivutia jamii hiyo ikahamasika kutamani kupeleka mtoto sekondari, ni pamoja na shule kuwa na umeme unaotokana na nishati ya nguvu za jua na maji ya bomba, yaliyotokana na kuchimbwa kisima kirefu.

Aidha, kuwepo maabara kubwa ya kompyuta, vyoo bora ambavyo imefikia hatua, uongozi wa wilaya ya Simanjiro kupendekeza ramani yake itumike kwa wilaya nzima, katika ujenzi wa vyoo vipya shuleni.

Ufunguzi wa jengo la maabara ya kompyuta likiwa na kompyuta zake ishirini na jengo la maktaba, ilifunguliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleman Jafo, Oktoba 20 mwaka jana

Ujenzi wa nyumba za uhakika za kuishi walimu zenye umeme wa nguvu za jua, umeendelea kuvutia walimu wengi kutamani kufundisha shule hapo.

Awamu ya kwanza ya nyumba sita, ambazo kila moja ina sehemu ya kuishi familia mbili, zilifunguliwa rasmi na Mkuu wa mkoa wa Manyara, Alexender Mnyeti, Januari 23 mwaka jana.

Pia, katika kupunguza uharibifu wa mazingira wa ukataji miti kwa ajili ya kuni, sekondari hiyo ya Emboret inatumia mtambo wa gesi ya kinyesi cha biogas kwa ajili ya kupikia.

**YANASULIWA MKIANI**

Mwenyekiti wa ECLAT, Peter Toima, anasema tangu waanzishe taasisi hiyo mwaka 2008, wamekuwa na lengo la kushirikiana na jamii na serikali katika kuboresha maisha ya jamii masikini nchini.

> "Jamii yetu ya wafugaji inakabiliwa na changamoto nyingi, hivyo ili watoto wapate elimu bora tumehakikisha wote, wanalala shuleni kwa kujenga mabweni matano yenye uwezo wa kuchukuwa wasichana na wavulana 320,"



Mwenyekiti wa shirika la ECLAT, Peter Toima (kushoto), akipata maelezo kwa mkandarasi wa jengo la shule ya msingi, katika kata ya Emboret, wilayani Simanjiro.

Anasema, jitihada hizo zilizaa matunda mwaka 2015 katika shule ya sekondari ya Emboret, ilifanikiwa kujinasua kutoka shule inayoburuta mkia na kuwa ya kwanza wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, ikishika nafasi ya nane, ikiwa ni matokeo ya jitihada za ECLAT.

Wilaya ya Simanjiro ina shule za sekondari 16 na mkoa wa Manyara una jumla ya sekondari 64 na kwa sasa ndiyo pekee ya serikali, wilayani Simanjiro yenye kidato cha tano na Sita.

"Jamii yetu ya wafugaji inakabiliwa na changamoto nyingi, hivyo ili watoto wapate elimu bora tumehakikisha wote, wanalala shuleni kwa kujenga mabweni matano yenye uwezo wa kuchukuwa wasichana na wavulana 320," anasema Toima.

Anaeleza kwa sasa shule ina nyumba za walimu, vyumba vyote vitatu vya maabara na maktaba na sasa shule ina walimu wa kutosha zaidi ya 20 na mkoa unaifanya shule kamili ya mchepuo wa sayansi.

Mmoja ya walimu wa shule hiyo, Samwel Kaitua, anasema kutokana na ubora huo, shule imekuwa kimbilio kwa jamii ya Wamasai ambayo awali ilikuwa nyuma kwa elimu na kupuuzia na kujali la elimu.

Aidha Mwalimu Kaitua anasema hivi sasa kuna shinikizo kubwa la wazazi wa maeneo ya mbali kutaka nafasi ya vijana wao katika shule hiyo.

**BAJETI BIL. 3.5**

Msimamizi wa Miradi wa shirika la ECLAT, Masham Bakiri, anabainisha kuwa kwa kushirikiana na wahisani wa Shirika Lisilokuwa la Kiserikali Upendo Society la nchini Ujerumani,

wameitengea shule hiyo bajeti ya kiasi cha Sh. milioni 500 kila mwaka hadi mwaka 2020 ambapo hadi mradi wa uboreshaji wa shule hiyo utakapokamilika utakuwa umegharimu kiasi cha Sh. bilioni 3.5

Toima anaeleza awali ilikuwa vigumu sana kupata wanafunzi wenye sifa ya kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hiyo kutoka katika kata ya Emboret lakini baada ya kubaini tatizo kuwa ni shule za msingi za kata ya Emboret, waliamua nazo kuboresha miundombinu.

Anaeleza kuwa kata hiyo ina shule za msingi saba ambapo kabla ya kuamua kuziimarisha, miongoni mwa shule hizo zilikuwa na wanafunzi ambao walikuwa wanasomea chini ya miti na nyingine zilikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi.

Miongoni wa uboreshaji wa miundombinu uliofanyika ni pamoja na ujenzi wa madarasa saba, ofisi ya walimu na vyoo viwili katika shule ya msingi Ormotoo, ujenzi wa shule mpya kabisa ya Satellite Loiborsoit A kutokana na shule mama kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi.

Uboreshaji wa shule hizo za msingi kwa ujenzi wa madarasa, vyoo na shule mpya umetengewa kati ya Sh. milioni 130 mpaka milioni 145 kwa mwaka kwa kila shule

Anasema kwa sasa wanajivunia kuona kwamba kumekuwapo na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na kidado cha kwanza na pia katika shule za msingi sambamba na ubora wa elimu inayotolewa katika shule hizo.

**WATAMANI SHULE**

"Kuna vitu vingine tunaweza kuona ni vidogo, lakini huongeza hamasa sana katika jamii, mfano kufanyika kwa sherehe za mahafali katika shule ya sekondari ya Emboret kila mwaka, imekuwa hamasa kubwa kwa wazazi kiasi kila mmoja anatamani mwanaye ajiunge na sekondari badala ya kwenda kuchunga ng'ombe ana kuozwa," anafafanua Toima

Toima anaeleza katika mwelekeo huo huo wa elimu, tayari wameanza mchakato wa ujenzi wa chuo cha ufundi kitakachoanza na wanafunzi 24 wa fani ya uashi Machi mwaka huu,

Inaendelea Uk.18

## TEKNOLOJIA

**NA BEATRICE PHILEMON**

# Wanafunzi Ngurdoto walipolipuka kufurahia ugeni wa umeme Sola

## ■Nusu karne yapita hawaujui umeme
## ■Maisha; vijinga, moto, vibatari, tochi
## ■Mwalimu Mkuu: Karibu somo tehama

UPATIKANAJI umeme wa nishati ya jua katika kijiji cha Ngurdoto, ni tukio la kuamsha furaha kubwa kwa wakazi wake na hasa katika Shule ya Msingi Ngurdoto, wilayani Arumeru, mkoa wa Arusha.

Ni ugeni ambao una tafsiri ya moja kwa moja, kusaidia kwa kiasi kikubwa kufundishia somo la Tehama, ambalo hivi sasa lipo kwenye mtaala wa elimu ya shule za msingi.

Ni hatua itakayiwezesha kuinua kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu somo hilo la Tehama ambalo hivi sasa linatumika katika nchi mbalimbali duniani katika masuala ya mawasiliano, pia kusukuma maji ya kisima kwa matumizi shuleni.

Matarajio yaliyoko ni kwamba, utatumika kufundishia watoto shuleni kwa matumizi ya projekta, pia kunufaisha wananchi kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato, kusikiliza radio, kuangalia TV na kupata taarifa mbalimbali duniani kupitia vyombo hivyo vya habari.

**NEEMA UMEME**

Akizungumza na Nipashe, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ngurdoto, Neema Urio, anasema unapotaja kijiji cha Ngurdoto, hakifahamiki kwa wengi.

Anafafanua kwamba, kijiji cha Ngurdoto kipo kata ya Maji ya Chai na kilianzishwa mwaka 1973 ambapo mpaka sasa kina vitongoji vitano vyenye wakazi 4000.

Kwa muda wa miaka 45, wananchi waliishi kwenye giza la kukosa umeme na walitegemea mbadala wa vijinga vya moto, vibatari na tochi katika kupata mwanga wa matumizi ya nishati nyumbani na watoto kujisomea.

**MWALIMU MKUU**

Mwalimu Mkuu anasema, hivi sasa hali ya maisha ya wananchi kijijini imeanza kubadilika, wananchi wako furahani, hasa wanafunzi baada ya Serikali ya Korea Kusini, kupitia Kituo cha Ubunifu wa Tekinolojia na Nishati (ITEC), kimejenga kituo cha kuzalisha umeme wa nishati ya jua, ili kuboresha sekta ya elimu, afya na kusaidia wananchi kuanzisha shughuli za kujiongezea mapato, hali inayoelezwa kuwa mafanikio makubwa ya miaka 45 sasa.

"Ninaishukuru sana Serikali ya Korea kupitia ITEC kuleta mradi huu katika kijiji cha Ngurdoto, kwa sababu wanafunzi watatumia umeme huu kujisomea na kuongeza ufaulu zaidi .

"Itasaidia ofisi za walimu na madarasa ya wanafunzi kuwa na umeme, lakini pia walimu watatumia umeme huo kujifunza compyuta ili waweze kuzitumia kufundishia wanafunzi darasani", anasema.

Pia ameiomba serikali ya Korea Kusini kupitia ITEC na Serikali ya kijiji, iwasaidie kufikisha umeme huu shuleni ili kutumia kupampu maji ya kisima kwa matumizi ya kupikia, kunywa, chooni na kadhalika.

Pia, wanawaomba wafadhili hao kuwasaidia kupata kompyuta walau 30, ili wanafunzi wajifunze Tehama kwa vitendo, mtaala unaofunzwa kuanzia darasa la tatu hadi la tano.

> Tunamshukuru Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kukubali mradi huu kuwepo katika kijiji chetu, hasa kitongoji cha Mseseweni na serikali ya Korea kumtuma DK.Rhee kuja kuona hali tuliyokuwa nayo hapa kijijini, ambayo imesababisha leo kijiji chetu kupata umeme wa nishati ya jua,"



Kutoka kushoto, Mwenye nguo ya kitenge, Ofisa Mtendaji wa Kitongoji cha Mseseweni, Christina Ndewo, akifuatiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Nishati na Teknolojia ya Ubunifu (ITEC) Dk. Herb Rhee na Mwenyekiti wa Kijiji cha Ngurdoto (mwenye suti yabluu), Moses Ayo, wakiwa kwenye picha ya pamoja, mara baada ya kutia saini Hati ya Makubaliano (MoU) na ITEC wilayani Arumeru. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**




Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (wa tano kutoka kushota), kwenye picha ya pamoja na Mkurugenzi wa ITEC na viongozi wengine wa Ubalozi wa Korea Kusini, Chuo kikuu cha Nelson Mandela na vijiji jirani na Mseseweni, baada ya kuzindua kituo cha kuzalisha umeme wa nishati ya jua.

Anasema, somo la sayansi na teknolojia linahitaji kompyuta na ujenzi wa vyumba viwili vya vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 30, ili wanafunzi wengi wanufaike.

Mpaka sasa Shule ya Msingi Ngurdoto, ina wanafunzi 800, walimu 17 na kuna mwalimu mmoja mahsusi kwa kompyuta na vyumba 14 vya madarasa.

Mwalimu Urio anasema, pia wanahitaji madarasa matatu kwa ajili ya wanafunzi, vyumba viwili vya kompyuta na mwalimu wa kompyuta wa kuwafundisha walimu wengine.

**CHANGAMOTO**

Mwalimu Mkuu anasema, katika mfumo wa maji yanayosukumwa kutoka umeme wa chanzo cha Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco).

Hata hivyo, Mwalimu analalamika katika chanzo hicho cha maji katika Shule ya Msingi Ngurdoto, bado kuna tatizo kubwa kwa sababu wazazi hawatoi pesa za kununua uniti za umeme, ambayo ni kuchangia Sh. 100 kwa mwaka.

"Hivi sasa hali imebadilika sana, wazazi hawatoi hela kabisa, hivi sasa natumia fedha za familia yangu kununua uniti za umeme.

"Kwa mwezi natumia zaidi ya Sh.10,000 ili wanafunzi waendelee kupata maji. Nafikiri upatikanaji wa umeme wa nishati ya jua, utasaidia kupunguza gharama hapa shuleni," anasema.

Anasema, pamoja na kuwapo kisima, bado maji yanayopatikana hayatoshelezi matumizi ya shule, kwa sababu ni kisima cha kuvuna maji ya mvua wakati wa kiangazi na siyo cha kuchimba.

"Tunavuna maji ya mvua kutoka kwenye mabati, yanaenda moja kwa moja kwenye kisima na tunatumia dawa ili kuua vijidudu na maji yake salama kwa matumizi ya wanafunzi na walimu," anasema.

**MWANAFUNZI MHITIMU**

Grory Lyimo ni mwanafunzi aliyemaliza kidato cha nne mwaka jana, katika Shule ya Sekondari Ngurdoto, anautafsiri hiyo ni mabadiliko makubwa katika mazingira ya kimasomo anayoyajua.

"Kutokanana na matumizi ya vibatari macho yalikuwa yanauma na saa nyingine kifua kinauma na nilikuwa natumia 'lisaa limoja' tu kujisomea.

"Sasa hivi tunamshukuru Mungu, katika kijiji chetu hali imebadilika, wanafunzi wanajisomea vizuri na kila mtu anatembea barabarani bila woga, kwa sababu taa zinawaka kila mahali. Wananchi wamenunua friji wanataka kuanzisha biashara za 'ice cream' kwenda kuuza shuleni", anasema.

**KITUO ITEC**

Mkurugenzi mkuu wa Kituo cha Ubunifu wa Tekinolojia na Nishati (ITEC), DK. Herb Rhee, anasema kituo kina uwezo wa kuzalisha kilowati 6.5 za umeme na mpaka sasa kuna jumla ya nyumba 43 katika kitongoji cha Mseseweni zimeunganishiwa umeme huo.

Hiyo ni kwa ajili ya matumizi majumbani na shughuli nyingine za kujiongezea kipato pamoja na taa 10 za usalama barabarani usiku.

Ili kuufanya mradi endelevu, kijiji kimeunda kamati ya kukusanya fedha kutoka kwa wananchi kulingana na matumizi yao ya umeme na zitasimamiwa na kamati iliyoteuliwa na serikali ya kijiji, chini ya ITEC.

"Mradi huu utakabidhiwa Serikali ya Kijiji cha Ngurdoto. Fedha zote zitakazokusanywa na kamati, zitatumika kumlipa meneja wa Kituo kwa ajili ya kuendeshea mtambo na kufanya matengenezo, kama kutatokea hitilafu yoyote kwenye mtambo na matengenezo mengine," anasema.

Vile vile ITEC itaendelea kuunganisha umeme bure katika nyumba nyingine na fedha za matumizi ya umeme zitatozwa na kamati kulingana na matumizi ya kila nyumba kila mwezi. Aidha ITEC kitaendelea kufunga smart mita kwa ajili ya kufuatilia matumizi ya umeme kila nyumba.

Hiki ni kituo cha pili kujengwa na ITEC, kituo cha kwanza kilijengwa katika kijiji cha Mkalama kilichopo kata ya Masama-Rundugai wilaya ya Hai mkoa wa Kilimanjaro na jumla ya nyumba 50 kijijini mkalama ziliunganishwa umeme huo.

Aliwaomba wananchi wa kijiji cha Ngurdoto hasa kitongoji cha Mseseweni kutumia umeme huo kupambana na umasikini na kusaidia watoto kusoma katika mazingira mazuri.

"Ebu shangilieni upatikanaji wa umeme wa jua katika kijiji chenu, huu ni mwanzo, pamoja tunaweza kufanya vitu vingi vya kuleta maendeleo katika kijiji chetu na vijiji jirani, tukiwa pamoja hakuna kitu kisichowezekana," anasema.

**MWENYEKITI KIJIJI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ngurdoto, Moses Ayo, anasema kilianzishwa mwaka 1973 na sasa kina wakazi 4,000 ikiwa na vitongoji vitano anayovitaja ni: Bondeni, Mburiashi, kati, Msamaneni na Mseseweni.

"Tunamshukuru Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kukubali mradi huu kuwepo katika kijiji chetu, hasa kitongoji cha Mseseweni na serikali ya Korea kumtuma DK.Rhee kuja kuona hali tuliyokuwa nayo hapa kijijini, ambayo imesababisha leo kijiji chetu kupata umeme wa nishati ya jua," anasema

"DK.Rhee alipokuja kijijini, alitukuta tupo kwenye giza na leo hii wananchi wamepata umeme, jumla ya nyumba 43 tayari zimeunganishwa na umeme wa nishati ya Jua," anafafanua

Mwenyekiti kijiji anaendelea kuwa ujio wa umeme huo wa jua ni hatua moja, bado wanahitaji umeme wa Tanesco kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kwa sababu mahitaji ni makubwa kijijini hapo na umeme umeshafika katika kitongoji kimoja tu, kati ya vitano.

**DC ARUMERU**

Naye mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, anaishukuru serikali ya Korea Kusini, kusaidia wananchi wa kitongoji cha Mseseweni kupata umeme wa nishati ya jua.

"Hii ni hatua nzuri ambayo imefanywa na serikali ya Korea Kusini katika kuunga juhudi za Mheshimiwa Rais Awamu ya Tano, Rais John Magufuli, katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi," anasema.

"Nitoe wito kwa uongozi wa kijiji, mradi huu umetokana na kodi za wananchi kutoka Korea Kusini, tumieni mradi huu kuondokana na umasikini, mhakikishe mradi unawanufaisha," anasisitiza.

Kupitia mradi huu watoto watakuwa wanasoma katika mazingira mazuri yenye mwanga wa kutosha na kuongeza ufaulu shuleni.

"Nitoe wito, kamati nyingi zinashindwa kufanya kazi kwa sababu ya majungu na mambo ya kisiasa. Wekeni siasa pembeni, siasa iliyo safi ni ile inayoondoa changamoto za wananchi.

"Hatutaki siasa katika mradi huu, hizi ni fedha za moto, ukila zitakutumbua na mimi nitafuatilia ukusanyaji wa fedha hizi na kila anayepata umeme apewe risiti,' anawatahadharisha

## JIELIMISHE



Fatima Khamis. **PICHA: UN**

# Kigogo wa mawasiliano UN anayedhihirisha '50 kwa 50'

KUTOKANA na sababu mbalimbali, zikiwamo za utamaduni, takwimu mbalimbali zinaonyesha bado kuna umuhimu wa kuweka mazingira ya kuwahamasisha wasichana kujiunga katika fani za sayansi.

Fatima Khamis kutoka nchini Sudan, ni mwanamke pekee katika Kitengo cha Uhandisi wa Mitambo ya Mawasiliano ya Walinda Amani, walioko chini Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Katika nchi hiyo ambayo imegubikwa na ukosefu wa usalama na amani kwa muda mrefu, kuna zaidi ya walinda amani 13,000 wanaosaidia kurejesha amani na utulivu. Katika kundi hilo, ni asilimia tano pekee ndio wanawake.

Hapo ndipo unamkuta Fatima Khamis, ambaye baada ya 'panda shuka' katika minara mirefu ya mawasiliano, sasa yuko ofisini kwake akipokea na kutoa maelekezo kwa njia ya simu.

Fatima, alijiunga na Mpango wa Ulinzi wa Amani wa Umoja wa Mataifa, huko Afrika ya Kati Minusca, akifanya kazi kama mhandisi wa mtandao wa intaneti. Anasema, alikokulia ni kama vile elimu ilikuwa maalumu kwa wavulana tu.

Anasimulia: "Kazi hizi zote zimesheheni wanaume na kunapokuwa na mwanamke, wanafikiri hawezi. Ili kuibadili dhana hii tunatakiwa kufanya kazi sana".

Fatima anasema, mwanzo alipojiunga na Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP), walikuwa wanawake sita tu, katika chumba cha redio na alipohamia katika kikosi cha sasa, yeye ni mwanamke peke yake.

Hivi sasa Fatima anataka kutengeneza jina lake katika fani hiyo ya uhandisi wa mitandao ya mawasiliano.

"Kama unavyofahamu, hii fani inabadilika haraka sana. Ninatakiwa kusoma sana. Nimeanza masomo yangu ya uzamili baada ya kujiunga na kazi hii na sasa nusu ya masomo yangu imeshakamilika. Ninajiandaa kwa ajili ya nafasi kubwa katika maisha haya."

Kama ilivyo kwa Fatima, wanawake wengi wanaofanya kazi katika Umoja wa Mataifa wanafungua mianya mipya katika teknolojia ya habari.

**UN**

## JE, WAJUA?



# Maharage ya nyama kutoka kwa Waturuki

MAHARAGE ni mlo ambao hutengenezwa katika maeneo mengi duniani toka enzi za mababu. Maharage hupikwa katika maeneo tofauti kuanzia Amerika ya Kusini hadi Mashariki ya Mbali.Hupikwa Afrika hadi Ulaya na mara nyingi huliwa na wali pembeni.

Waturuki nao hupenda kupika maharage kwa supu ya nyama na kadhalika.Wengine huita maharage kama chakula cha taifa nchini Uturuki na hupendwa kuliwa wakati wa jioni.

Leo tutatizama jinsi maharage yanayopikwa katika ladha ya kipekee nchini uturuki na huliwa na wali pamoja na achari pembeni.

Mahitaji: Vikombe 2 vya maharage; kitunguu kimoja kilichokatwa; Vijiko viwili vya nyanya ya kusaga/kopo; vijiko viwili vya siagi; gramu 250 za nyama iliyokatwa; vipande 2 vya pilipili ndefu; chumvi kijiko kimoja; nusu kijiko pilipili nyekundu; na vikombe sita au saba vya maji.

Inavyopikwa; Kwanza, weka maharage yako katika maji na uyaache kwa muda wa angalau saa nane mpaka yavimbe, yaoshe vizuri, chuja maji yake na kisha yachemshe katika maji mengi.

Wakati wa kuchemsha, ondoa povu na kisha uchuje tena maji. Wakati huo huo, yeyusha siagi kwenye sufuria nyingine, na ukaange vitunguu pamoja na pilipili ndefu.

Weka nyama na uendelee kukaanga .Ongeza nyanya na uendelee kukoroga kisha weka maji ya moto.

Wakati mchanganyiko wako ukichemka, ongeza maharage uliyochemsha na weka chumvi na pilipili nyekundu.Subiri mpaka maharage yalainike.

Chakula chako sasa kipo tayari kula kwa wali na achari pembeni.

Furahia chakula chako!

## UTAFITI

# Uturuki yaweka kambi ya utafiti barani Antaktika

KINACHOELEZWA ni katika maono ya kisiasa ya Rais Recep Tayyip Erdo an wa Uturuki, kuwa na kambi ya Utafiti katika Bara la Antaktika, kwa mujibu wa Radio Uturuki.

Uturuki imeamua kuweka kambi yake ya muda barani Antaktika kuendesha utafiti, kama ilivyoelezwa na Waziri wa Viwanda na Teknolojia, Mustafa Varank, katika taarifa aliyoitoa akiwa mjini Bolu.

Varank anasema, Uturuki imeweka kambi ya muda ya utafiti katika bara la Antaktika na hilo ni moja katika maono ya Rais wake kwamba hivi sasa watafiti wa Uturuki, wapo katika safari yao ya tatu ya kutafiti Bara la Antaktika.

Varank anasema kwamba picha za watafiti wa Uturuki walioko Antaktika zimewafikia na kwamba hilo ni suala la kujivunia kuona bendera ya Uturuki ikipepea katika bara hilo.

Waziri Varank, anasema Uturuki imeunda kambi ya muda ya utafiti katika bara la Antaktika. Alitumia muda huo pia kuwashukuru watafiti wa nchi yake ambao pamoja na hali ya hewa isiyo rafiki kwao, wameendelea kuiwakilisha nchi vizuri sana na wanajivunia hilo.

**Habari zote ni kwa mujibu wa taarifa za Mtandao**




Kambi ya kitafiti ya Uturuki, Bara la Antaktika. **PICHA: MTANDAO**

# Miradi mipya yabadili upepo wa elimu wilayani

**Inatoka Uk.15**

kisha itafuatiwa na useremala

"Lengo ni kuhakikisha jamii ya Wamasai wanahifadhi utamaduni wao, lakini waweze kuendelea zaidi kwa kupata elimu," anaeleza Toima, akisema mkakati wao ni kuwa sehemu ya matatizo kwa kutafuta ufumbuzi wake.

**KINAMAMA WAJASIRIAMALI**

Anafafanua kwamba, kupitia mwamko huo wa kufanya mapinduzi katika elimu, kinamama wa Kimasai wameanza kujikita katika ujasiriamali kwa kuunda vikundi zaidi ya 100.

Toima anasema, mila za jamii hiyo zipo wazi kwamba nyumba ni mali ya mama, hivyo ili kuhakikisha mwanamke anajikwamua na hali ngumu kimaisha na kujijengea uwezo wa kuhudumia nyumba, ndipo wameunda vikundi vya ujasiriamali.

Anataja miradi hiyo wanayoendesha kwa kusaidiwa na vijana, ni kununua ng'ombe na mbuzi, wanawanenepesha na baadaye wanawauza kwa bei nzuri.

Toima anasema, kwa sasa kila likundi kina ng'ombe 100, wana uhakika wa kupata mapato makubwa, hasa bei inapokuwa juu.



Moja ya jengo la vyoo vipya vya kisasa, katika shule za msingi kata ya Emboret.

Mwenyekiti wa Kikundi cha kinamama cha Esupat, Paulina Muvina, anasema msaada walioupata wa kuanzishwa mradi mbadala wa mashine za kukoboa nafaka kwa vikundi 10, umewasaidia kujikimu wakati wanasubiri muda wa kuvuna ng'ombe na mbuzi uwadie sokoni.

Toima anasema, ili kuwawezesha waendeshe miradi kwa ufanisi, wamewaanzishia kituo cha maendeleo ya mafunzo kwa wanawake na kila mwanakikundi anahudhuria mafunzo ya siku tano yanayofanyika kwa mzunguko.

"Mafunzo hayo ni endelevu na kituo hicho ni cha kudumu hivyo kila awamu uwa na wanawake wasiopungua 30, lengo ni kuhakikisha katika miradi yao, wanakwenda na wakati ili kuhakikisha inakuwa endelevu na kamwe wasifilisike," anafafanua Toima

Toima anaeleza wameanza kusaidia wilaya nyinginezo kwa kuboresha miundombinu ya elimu, zikiwemo Monduli, Ngorongoro, Mtwara na Lindi

Mradi waliosaidia ni wa Shule ya Msingi Lengijape, iliyopo wilayani Monduli, Arusha, ambayo mnamo Juni mwaka jana, walikabidhi vyumba vinne vya madarasa vilivyozinduliwa na Mkuu wa Mkoa, Mrisho Gambo.

**Mwandishi anapatikana kwa anwani ya baruapepe: makunganova@gmail.com na simu (+255) 0784682268**

ELIMU

NA ELIZABETH ZAYA, ALIYEKUWA KIBAHA

# Tasaf ilivyobadili masikini watoro, hadi wasiokosa mahudhurio shule

## ■Sera ya kukata pesa imefanya kazi yake



Baadhi ya wakazi wa kijijini Vikuge, Kibaha, wakiwa katika moja ya mikutano ya maendeleo. **PICHA: MAKTABA**

KUNA mbinu mbalimbali, ambazo watu wanaweza kuzitumia, pale wanapoona jambo haliendi ili kutafuta majibu au kutoka katika eneo la tatizo na kusonga mbele zaidi.

Mafanikio au kusonga mbele, hutegemea namna kila mhusika au wahusika wenyewe wanavyojipanga kutafuta mbinu au kuweka mikakati madhubuti ya kutafuta mafanikio chanya ya kuondoa mahali walipo.

Hiyo ndiyo mbinu inayotumiwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Tasaf), mkoa wa Pwani, kuleta watoto wa kaya zinazoishi katika mazingira magumu ya kiuchumi, kupenda shule.

Kupitia mtazamo huo, sasa kunaonekana mfano wa kuigwa, kutokana na mahudhurio yao mazuri shuleni kama anavyoeleza Mratibu wa Tasaf mkoa huo, Irene Itewele.

Mratibu huyo anasimulia kwamba ilikuwa ni kazi ngumu kuwashawishi watoto wanaoishi katika kaya masikini kupenda shule, kama ilivyo kwa watoto wengine, lakini zilipoingizwa katika mpango unaoelezwa, mambo yamebadilika.

"Kabla watoto hawa hawajaingizwa katika mradi, ilikuwa ni vigumu kwenda shuleni. Walikuwa hawapendi kusoma na hata wazazi wao hawakuwa na uwezo wa kuwanunulia hata daftari. Kwa hiyo, wakawa wamekata tamaa ya kusoma," anasema Itewele na kuongeza:

"Ulipokuja mpango huu wa uhawilishaji fedha kwa kaya masikini, ulifanyika utafiti wa kubaini kaya zote zilizo katika mazingira magumu, nyingi zilizokuwa katika hali mbaya sana ziliingizwa katika mpango na kipaumbele zaidi kiliwekwa katika kaya zenye watoto wenye umri wa kwenda shule."

**KUDHIBITI MAHUDHURIO**

Itewele anasema utaratibu uliowekwa na Tasaf, hususan kwa watoto wanaosoma, waliwekewa kwenye mpango wa kaya kupatiwa kiwango cha fedha kamili na lazima wahakikishe wanawasimamia watoto wao kusoma kwa bidii na kuhudhuria shuleni inavyotakiwa.

Anasema, utaratibu uliowekwa na Tasaf, ni kwa kaya zenye watoto wanaosoma, pindi wasiposimamiwa vyema na kuachwa wanatoroka shule, zinakatwa pesa za mgawo walizoidhinishiwa na wanapaswa kupewa kamili.

"Tasaf wameweka utaratibu mzuri sana, kwamba kwa wanafunzi walioko katika mpango, wanapokuwa wanatoroka shuleni pesa zao hukatwa, kwa hiyo imesaidia sana, hata wazazi huwa wanahakikisha wanawasimamia watoto wao kwenda shuleni kila siku," anasema Itewe.

"Pamoja na kwamba wao wanakuwa wanajitahidi kufanya hivyo ili wasikatwe pesa yao ya kila mwezi, lakini sisi tunafurahi kwamba imewasaidia watoto kupata elimu na hata maendeleo yao ni mazuri sana, kwa sababu wana umakini mzuri sana katika ufuatiliaji wa masomo shuleni," anasema.

> "Lengo tunataka kwamba nyumbani kuwe na kipato cha kutosha, tunataka hata watoto wakiwa shuleni wasiwe wanyonge, waone wazazi wao wanapambana kuondoa umasikini,"

**MRATIBU TASAF**

Mratibu wa Tasaf wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Sijaona Muhunzi, anasema wakati wanaanza uhamasishaji kwa kaya za walengwa kuwapeleka watoto shuleni, ilileta ugumu na walitumia nguvu, lakini kwa sasa kazi imekuwa rahisi kwao.

"Yaani tunafurahi sana kufika hapa tulipo. Huwezi kuamini kwamba, tulianza hatua ya sifuri kuhamasisha wazazi kuwapeleka shuleni watoto wao, upokeaji wake ulikuwa unafanyika taratibu sana.

"Lakini, hatukukata tamaa tuliendelea kuwahamasisha na mpaka hivi ninavyokuambia tuna asilimia zaidi ya 90 ya watoto wa walengwa wanaohudhuria shuleni. Wamekuwa na mwitikio mkubwa na wa mfano," anasema Muhunzi.

Mhunzi anasema wamekuwa wakifanya kazi ya ufuatiliaji wa watoto kwa kushirikiana na wazazi pamoja na walimu.

"Kazi kubwa ambayo tumekuwa tukiifanya, hatukati tamaa katika uhamasishaji. Tunashirikiana na wazazi au walezi wao, pamoja na walimu katika shule wanazosoma.

"Mbali na kufuatilia, lakini huwa zipo fomu maalum ambazo zinapelekwa katika shule hizo, ambazo walimu hujaza mahudhurio na maendeleo ya watoto," anasema Mhunzi.

Anafafanua zaidi: "Kwa hiyo inakuwa inatupa urahisi sisi wasimamizi kufahamu kaya zipi ambazo watoto wanalegalega shuleni na inatupa mwanya wa kuwafuatilia zaidi. Kwa hiyo, imesaidia sana watoto hata ambao walikuwa wavivu kuogopa kutoroka."

Kwa mujibu wa Mhunzi, ni hali inayosaidia kuwaweka watoto hao kutoka kaya maskini zilizolengwa, kuwa mfano wa kuigwa hata kwa wengine ambao hawako katika kaya za walengwa.

"Hawa watoto sasa hivi wana maendeleo mazuri katika msomo, huenda wenyewe walikuwa wanafanya hivyo ili wasikatwe pesa, lakini tunashukuru kwamba pia ni njia ambayo imetumika wapate elimu ambayo ubora wake hauishi leo wala kesho," anasema Mhunzi.

Anasema ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika masomo yao, pia wamekuwa wakihakikisha wanapatiwa mambo muhimu, ikiwamo kujiunga na bima ya afya ya kuwasaidia kupata matibabu pale wanapougua.

"Hatuishii tu katika kuwasimamia katika elimu, tunawasimamia pia kuhakikisha wanakuwa na afya njema, hatutaki kusikia visingizio vya aina yoyote.

"Mtoto anaweza akaugua halafu akasema haendi shule kwa sababu anaumwa na hajatibiwa, tunawasimamia na hata katika mambo hayo," anasema Mhunzi.

**WAZAZI KUPAMBANA**

Anasema, kazi nyingine wanayofanya ni kuhakikisha wanaendelea kutoa elimu kwa wazazi wa watoto hao, watafute mbinu mbadala wa kujiongezea kipato, kupitia ujasiriamali.

"Lengo tunataka kwamba nyumbani kuwe na kipato cha kutosha, tunataka hata watoto wakiwa shuleni wasiwe wanyonge, waone wazazi wao wanapambana kuondoa umasikini," anasema Mhunzi.

Akitoa taarifa mbele ya maofisa wa Mfumo wa Maendeleo ya Jamii kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo(DRC) waliofika nchini kujifunza, Itewele anasema kuanzia Januari 2014 hadi Desemba 2018, mkoa ulipokea Sh. bilioni 29.89 kusaidia kaya hizo.

Anasema elimu ya kila mara, imekuwa ikitolewa kwa walengwa katika kaya hizo na imewasaidia kuondokana na umaskini na kufikia hatua ya kuwa na uhakika wa kujikimu kimaisha na kujifunza namna ya kuweka akiba.

Mnufaika, Halima Kibavu, kutoka kijiji cha Vikuge, wilayani Kibaha, anaipongeza serikali kupitia Tasaf, kwamba imemsaidia kwa kiwango kikubwa kunusuru na umaskini aliokuwa nao kabla ya kuingizwa kwenye mpango huo.

Anasema, Tasaf pamoja na elimu ya ujasiliamali inayoitoa, imemsaidia kuanzisha miradi ya ufugaji na kilimo kinachomsaidia kuondokana na umasikini.

**Usikose makala ya harakati zao za mazingira siku ya Alhamisi.**



WADAU **SABATO KASIKA**

# UKOSEFU wa elimu ya afya ya uzazi kuanzia kwenye mabadiliko ya miili kwa wasichana, ni miongoni mwa mambo yanayotajwa kuchangia kuendelea kuwapo kwa mimba shuleni.

Wadau wana maoni gani?



**AMIR ABUBAKARI (MWALIMU WA DINI, MKAZI WA DAR ES SALAAM)**

KATIKA maisha, kila mtu anahitaji kuwa na watoto na tena siyo watoto tu bali wenye furaha na wenye kujitahidi kuwa na sifa njema, ambazo watazitumia watakapokuwa watu wazima. Kwa hiyo, ili kuwa na watoto wa aina hiyo yanahitajika malezi mazuri, ambayo yanaambatana na elimu ya afya ya uzazi kwa ajili ya kuwaepusha mambo yanayoweza kuwaharibia kile walichopanga kukifanya katika maisha yao ya baadaye.

Kwa kawaida, malezi mazuri hutoka kwa wazazi, kwa sababu ndio wenye wajibu wa kumlea mtoto. Labda nifafanue kwamba, malezi ni mfumo wa maadili ambao mtoto anapewa kutoka kwa wazazi au walezi wake ama jamii inayomzunguka na hata katika dini.

Ikumbukwe kuwa, malezi ni mpangilio. Kanuni za maisha zinazotolewa na wazazi au walezi ama jamii kwa ujumla ili wakue vizuri kimaadili na pia malezi ni mafundisho yanayotolewa na mzazi kwa mwanaye ili aweze kukua katika maadili mema na kuwa na maisha mazuri. Malezi hayo ni lazima yanaambatana na mafundisho ya kumwezesha mtoto kutambua na hata kuwa makini na vishawishi vya kumuingiza katika matendo yasiyofaa.

Inapokuja hoja kwamba ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi kuanzia kwenye mabadiliko ya miili kwa wasichana, ni miongoni mwa mambo yanayotajwa kuchangia kuendelea kuwapo kwa mimba shuleni, sina ubishi kwa hilo, kutokana na jinsi jamii ilivyotawaliwa na mambo ya utandawazi, ila jambo la msingi ni kwamba wazazi na walezi wawasaidie watoto kuwafundisha maadili mema. Mwenyezi Mungu anatutaka tuwalee watoto katika maadili mema.



**PFIRIAEL KIWIA (MKURUGENZI WA SHIRIKA LA KIMARA PEER EDUCATORS)**

BADO tuna safari katika vita hii ya mimba shuleni. Mimi naamini kwamba, ili kujenga taifa bora ni muhimu kuzingatia elimu ya afya ya uzazi na mambo yanayofanana nayo.


Ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi, unachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la mimba za utotoni, ndoa za utotoni na maambukizi ya magonjwa ya zinaa kama vile Ukimwi, Kaswende, kisonono na mengine mengi.

Elimu hiyo ikitolewa kikamilifu itawasaidia kuongeza uelewa, kusimamia na kutetea haki zao na za wengine bila woga, ndio maana asasi mbalimbali zimekuwa zikiendesha mafunzo ya afya ya uzazi na magonjwa ya ngono katika shule mbalimbali nchini.

Lakini, wapo baadhi ya wazazi ambao wanajiweka pembeni kwenye utoaji elimu, sababu kubwa ni suala la mila na desturi. Yaani, wanaona aibu kukaa na watoto wao na kuwaelimisha kuhusu masuala ya afya ya uzazi na kujamiiana ili waepuke mimba za utotoni, ndoa za utotoni na maambukizi ya magonjwa ya zinaa.

Wazazi wasionee aibu hatari inayonyemelea watoto wao, kwa sababu tu ya mila na desturi. Jukumu la kutoa elimu siyo la kundi fulani au serikali, bali la kila mtu, hivyo mila zinazoifanya wazazi waone aibu kukaa na watoto wao na kuwafundisha, hazina budi kuachwa ili kuokoa watoto hao.

Naomba nitoe wito kwa serikali ibadilishe sheria zote zinazomkandamiza mtoto wa kike na wanawake wadogo na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria hizo, ili kupata jamii inayozingatia usawa na haki kwa wote. Jamii nayo inatakiwa kulinda na kutetea haki za watoto, bila ya kujali jinsia.



**BELLY BUSAGI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

ELIMU ya afya ya uzazi, ni muhimu kwa watoto, pia wapewe uhuru wa kusikilizwa maoni yao ili kuepusha mimba za utotoni na maambukizi ya magonjwa yatokanayo na ngono, ili waweze kufikia malengo na kutimiza ndoto zao, kwani elimu hiyo inahusiana na mfumo wa uzazi wa mtu, na kwa watu.

Pia, inahusu mambo yote yanayojumuisha uzazi na jinsia.Kwa hiyo kila mmoja wetu hana budi kumsaidia mtoto wake kutambua hilo katika makuzi yake ili aweze kuepuka kujiingiza katika mtego ambao mwisho wa siku unaweza kumletea madhara makubwa.

Cha ajabu ni kwamba baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakikwepa jukumu la kuwapa watoto wao elimu ya afya ya uzazi wakidai kuwa wametingwa na shughuli nyingi, lakini ukweli unabaki palepale kwamba kila mmoja wetu ana wajibu wa kutoa elimu hiyo kwa mtoto wake. Watoto wanaokaribia umri wa kupevuka au kubalehe ama kuvunja ungo ni muhimu waelimishwe kuhusu afya ya uzazi.

Jamii iachane na mawazo kwamba kuwaelimisha watoto kuhusu afya ya uzazi ni sawa na kuwaruhusu wakafanye ngono. Mimi sikubaliani na hilo kabisa, ninajua kuwa kumpa elimu hiyo ni kumsaidia kujilinda dhidi ya vishawishi, hasa kwa kuzingatia kwamba mimba za utotoni licha ya kukatisha ndoto za mtoto, pia wataalam afya wanasema zina madhara makubwa kiafya.




**HIDAYA ALAWI (MRATIBU WA CHAMA CHA WAZAZI WENYE WATOTO WA KICHWA KIKUBWA NA MGONGO WAZI, ASBAHT)**

MZAZI siyo wa kuzaa tu, bali ana vitu vingi anavyotakiwa kumwelekeza mtoto wake kadri anavyokua, ili aweze kukabiliana navyo anapofikia umri wa kupevuka. Haki na wajibu wa malezi ni vya kwanza kwa wazazi, kwani wazazi ambao kimsingi ni walezi wakuu wa watoto, wanapaswa kuwa chanzo cha malezi bora ya watoto wao.

Hivyo, ni lazima watoto wapate malezi hayo kutoka nyumbani kwao, ili waweze kuwatii na kuwaheshimu watu wengine. Vinginevyo, wanaweza kuwa watoto wa ajabu. Malezi hayo ni lazima yaambatane na kuwapa elimu ya afya ya uzazi, kwani hiyo inahusiana moja kwa moja na mfumo wa uzazi wa mtu na via vya uzazi kwa watu.

Mtoto anatakiwa kuelezwa, ili atambue mabadiliko katika mwili wake na pia jinsi ya kukwepa vishawishi anavyoweza kukutana navyo katika makuzi yake, lakini mzazi akikaa kimya katika hilo, basi mtoto anaweza kuharibika.

Mzazi ana mchango mkubwa katika kuepusha mimba za utotoni. Kwa bahati mbaya, wapo baadhi ya wazazi wengi wamejisahau katika hili wanadhani kwamba siyo jukumu lao kukaa na watoto na kuwaelekeza mambo muhimu yanayohusu maumbile yao pale wanapopevuka, wazazi wa aina hii wabadilike.



**DK. TUMAINI MGUTU (HOSPITALI YA ALEXIA HEALTH CENTRE, DAR)**

Mimba za utotoni zina madhara ya kiafya, kutokana na ukweli kwamba, kuna sababu nyingi na ushahidi wa kisayansi unaoonyesha kuwa, msichana akipata mimba ni hatari kwa afya yake na mustakabali wa maisha yake na mtoto wake, ingawa siku hizi wasichana wengi huanza kupevuka, lakini wanakuwa hawajakomaa kiakili na uwezo wao ni duni katika maamuzi juu ya kufaa kwa mtu atakayekuwa mwenzi sahihi wa maisha.

Kwa upande wa kimwili, ni kwamba katika umri huo anakuwa hajawa tayari kuyakabili majukumu ya uzazi na unyumba, nyonga za msichana anaeendelea kukua, mara nyingi huwa changa na finyu kiasi kwamba husababisha matatizo mengi ya uzazi wakati wa kujifungua kwa njia ya kawaida.

Wengi wao wanachelewa kujifungua au huchukua saa nyingi za uchungu kabla ya kujifungua, hali hii inaweza kusababisha kifo cha mama au mtoto ama wote wawili iwapo matibabu ya dharura ya upasuaji kwa ajili ya uzazi hayatafanyika.

Wasichana wanaopata mimba na kujifungua katika umri mdogo wengi wao pia hupata tatizo la fistula na kujikuta wakitokwa haja ndogo au kubwa bila kujizuia. Ugonjwa huu kwa kawaida kuharibu afya ya mwili na hisia za mhusika.

Hivyo, elimu ya afya ya uzazi ni muhimu kwa vijana wadogo kama wataipata na kuitumia inavyotakiwa. Lakini wazazi, walezi, walimu na jamii kwa ujumla wakiwa kimya, vita dhidi ya mimba za utotoni itakuwa ngumu kuimaliza.



# TFDA kupambana uingizwaji chumvi isiyo na viwango

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Chakula na Dawa nchini (TFDA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imeanza kupambana na uingizwaji na uzalishaji wa chumvi ambayo haina madini joto ili kukabiliana na madhara ya udumavu kwa watoto.

Akizungumza wakati wa mafunzo, Meneja wa TFDA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Rodney Alananga, alisema matumizi ya chumvi hiyo yanasababisha madhara mbalimbali kwa wananchi ikiwamo udumavu wa watoto.

Alisema ili kupambana na hali hiyo wameanza kutoa mafunzo maalumu kwa maofisa lishe wa mikoa, wataalamu wa maabara za TFDA zilizoko kwenye mikoa yote na watumishi wengine wa mamlaka hiyo.

Alisema wameanza kutoa mafunzo kwa wataalamu hao ili kuongeza ukaguzi kwenye mikoa na wilaya zote za mkoa huo ili kuhakikisha matumizi ya chumvi hiyo yanakomeshwa na kuwaokoa wananchi na madhara ya chumvi hiyo.

Alananga alisema pia wanakusudia kuyatumia mafunzo hayo kuongeza idadi ya sampuli ya chumvi inayotumiwa na wananchi kwa kuikusanya kutoka kwa waingizaji wa chumvi, wauzaji na hata inayotumiwa na wananchi majumbani.

**Lengo la haya mafunzo ni kuhakikisha tunalinda afya za Watanzania, sasa tuna changamoto ya baadhi ya waingizaji wa chumvi na wazalishaji kuleta chumvi ambayo haina madini joto, sasa tunaamini haya mafunzo yatatusaidia.**

"Lengo la haya mafunzo ni kuhakikisha tunalinda afya za Watanzania, sasa tuna changamoto ya baadhi ya waingizaji wa chumvi na wazalishaji kuleta chumvi ambayo haina madini joto, sasa tunaamini haya mafunzo yatatusaidia," alisema Alananga.

Alisema wameamua kuimarisha mifumo ya ukaguzi ili kudhibiti wasambazaji wa chumvi na wazalishaji na kuhakikisha halmashauri zinaongeza ukaguzi wa chumvi.

Ofisa wa Mkoa wa Njombe, Willium Msenenda, alisema katika mkoa wa Njombe, Wilaya ya Wanging'ombe ndio yenye changamoto kubwa ya matumizi ya chumvi ambayo haina madini joto na hivyo kusababisha madhara.

Alisema wachimbaji hao wanatumia chumvi ya asili ambayo ina madini joto kidogo na inazalishwa katika mazingira ambayo usafi wake sio wa uhakika na hivyo inaweza kuwaletea madhara ya kiafya.

Alisema chumvi hiyo inachimbwa na wachimbaji wadogo katika wilaya hiyo na kusambazwa kwa wananchi ambao wanaitumia bila kujali madhara ya kiafya yanayoweza kuwakuta kutokana na matumizi ya chumvi hiyo.

"Tukiletewa ile chumvi ili tuipime kwenye maabara zetu tunakuta ina madini joto kidogo sana na hivyo haifai kwa matumizi ya binadamu, lakini wale wachimbaji wadogo wanaendelea kuizalisha na inatumiwa na wananchi," alisema Msenenda.

Kwa upande wake Mratibu wa Lishe wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sang, alisema wapimaji wa sampuli ya chumvi wanakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi vya kupimia chumvi hiyo hali inayosababisha kasi kuwa ndogo.

Alisema wakati mwingine vifaa hivyo huwa wanategemea wapewe na wafadhili hali ambayo inasababisha kuchelewa kupima na kwamba mpaka sasa kwenye halmashauri hakuna vipimo hivyo.



Dereva wa malori ya mizigo, Juma Nachikolo, akiuliza swali kwa Mkuu wa Kitengo cha Usalama na Mazingira kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Julius Chambo (hayupo pichani), baada ya kupewa elimu ya Sheria mpya ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoanza kutumika tarehe 1 Machi, mjini Tunduma, mkoani Mbeya juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Askofu ataka makanisa kuisaidia serikali

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

ASKOFU wa Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo Kusini, Kenan Panja, amesema makanisa yana wajibu wa kusaidiana na serikali katika kudhibiti vitendo vya dhuluma dhidi ya binadamu hasa ukatili kwa watoto ambao wanakatishwa maisha yao kwa imani za ushirikiana.

Akizungumza jana kwenye ibada maalum ya kuwapandisha madaraja ya kichungaji mashemasi na makasisi wa kanisa hilo iliyofanyika wilayani Rungwe mkoani Mbeya, Askofu Panja alisema katika karne hii watu wanaotumia ushirikina kutafuta utajiri wamekosa maarifa na fikra bunifu zenye kuwawezesha kutumia fursa zilizopo nchini kujiletea maendeleo.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wepesi kuchangia na kushiriki katika vitendo vya imani za ushirikina badala kuchangia shughuli za maendeleo zenye manufaa katika ujenzi wa taifa.

"Watu hawako tayari kuchangia 50,000 kwenye shughuli za maendeleo kama ujenzi wa zahanati, lakini lambalamba wakitoa tangazo la kutoa utajiri wapo tayari kutoa hata Sh. 1,000,000 hii inaashiria dunia kujaa maovu," alisema Askofu Panja.

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo wamesema kuwa ubarikio wa wachungaji hao ukalete chachu ya maendeleo katika vituo vyao vya kazi ili kuelimisha jamii kuhusu uzalendo na kudumisha amani ya nchi.

Baadhi ya wachungaji waliopandishwa madaraja akiwamo Vumilia Mwantimo alisema hatua hiyo imekuwa chachu kwao kwa kuwa wataenda kuhamasisha waumini kuendelea kutenda mema na kuachana na imani za kishirikina.

Takribani wachungaji 90 wa kanisa hilo wakiwamo wanawake na wanaume wamekula kiapo, kupandishwa madaraja na kupewa vitendea kazi na wana mamlaka ya kufanya huduma mbalimbali za kiroho zikiwamo za ubatizo kwa waumini wao pamoja na kufungisha ndoa.

# Wananchi watoa kilio kwa vigogo wa CCM

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WANANCHI wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamelalamikia kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo ambayo ilianza kujengwa tangu mwaka 2011, kuwa kunaathiri upatikanaji wa huduma muhimu za afya.

Walitoa malalamiko hayo jana wakati wa kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM, wilayani humo, ambacho kilikutana na wataalamu kwa ajili ya kuchambua na kutathmini utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Katika kikao hicho ambacho kilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ili kupima ubora wa huduma kwa wananchi na kutathmini miradi ya maendeleo kama inaendena na thamani ya fedha inayotengwa kwa ajili ya miradi hiyo.

Wananchi hao walisema jengo la Kituo cha Afya Rujewa ambacho kinatumika kutolea huduma kwa sasa hakikidhi mahitaji kutokana na changamoto ya miundombinu na uchache wa vifaa tiba na wataalamu.

Mmoja wa wananchi hao, Sharifa Mhepile, alisema ujenzi wa hospitali hiyo ni miongoni mwa miradi iliyotajwa kuwa na changamoto kubwa kutokana na ujenzi wake kutokamilika kwa wakati.

"Huduma ya mama na mtoto katika kituo hiki cha Rujewa sio rafiki kwa sababu ya majengo kuwa machache lakini pia wataalamu hawatoshi, tunalazimika kufuata huduma za afya kwenye vituo vingine vya afya, tunaomba serikali ikamilishe hospitali yetu haraka," alisema Sharifa.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Godfrey Mwakalila, alisema shughuli ya ujenzi zinaendelea baada ya serikali kutoa shilingi bilioni 1.5, na inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi mitano ijayo.

Mwakalila alisema hospitali hiyo imejengwa kisasa na itaweza kutoa huduma zote muhimu ikiwamo upasuaji kwa kinamama na wagonjwa wengine, maabara nzuri na stoo ya kutunzia chanjo ambazo zitakuwa zitatolewa kwenye vituo vya afya na zahanati zote za wilaya hiyo.

Mbunge wa Jimbo la Mbarali ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa wilayani humo, Haroun Mohammed, alisema vipaumbele vyake ni kuhakikisha wakulima na wafugaji wanaendelea kunufaika na shughuli zao.

Alisema kuwa wilaya hiyo ina rasilimali nyingi, lakini wananchi wengi bado wamekosa uthubutu wa kutumia fursa hiyo kujikwamua kiuchumi.





# Wazazi wakubaliana kujenga uzio wa shule

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BODI ya Shule ya Sekondari ya Dodoma kwa kushirikiana na wazazi inatarajia kuchangisha fedha kwa ajili ya kujenga uzio ambao utagharimu kiasi cha Sh. milioni 264.3.

Akizungumza na wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo jana, mwenyekiti wa bodi hiyo, Philbert Bagenda, alisema kuwa anatambua kwamba serikali imetoa agizo la elimu bure na kuwataka walimu au bodi kutowachangisha michango yoyote.

Alisema pamoja na kuwa serikali imekataza kutoza michango, lakini bado serikali haijazuia wazazi au wadau mbalimbali wa elimu wenye nia njema kuchangia elimu kwa hiari yao kwa manufaa ya Watanzania na jamii kwa ujumla.

"Pamoja na serikali kutoa kiasi cha Sh. bilioni 1.44 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya shule na mabweni ya wanafunzi, lakini bado inakabiliwa na tatizo la uzio jambo ambalo linasababisha wanafunzi kukosa utulivu wanapokuwa shuleni," alisema.

**Katika mahafali ya kidato cha nne Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, aliagiza bodi kuhakikisha inafanya kila jambo ili kujenga uzio.**

Alibainisha kuwa pamoja na shule hiyo kuwa kongwe, lakini haina uzio kwa miaka mingi.

"Katika mahafali ya kidato cha nne Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, aliagiza bodi kuhakikisha inafanya kila jambo ili kujenga uzio.

Aliongeza "Tulianza kwa kuweka mipango kazi, jambo la kwanza tulianza kutafuta na kuweka mipaka ya shule kwa usahihi, kufuatilia michoro ya uzio pamoja na kutafuta thamani halisi ya ujenzi wa uzio na hayo yote yalifuata utaratibu kwa kupitia halmashauri ya jiji, ambapo tayari yote yameishakamilika na kupata kibali cha kuanza ujenzi na wataalamu wa jiji ndiyo waliotupatia thamani halisi ya Sh. milioni 264.3 hadi ujenzi wa uzio unakamilika."

Aidha, Bagenda alisema kutokana na kumaliza taratibu hizo bodi kwa ujumla iliona ni jambo jema kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo ya elimu.

Akichangia hoja hiyo mmoja wa wazazi, Nasoni Manyere, alisema kuwa licha ya serikali kukataza michango lakini si jambo baya iwapo wazazi watakubaliana kwa hiari yao kufanya shughuli za kimaendeleo.

Alisema yeye anakubaliana na wazo la bodi la kuwashawishi wazazi kutoa michango yao wa hiari kwa nia ya ujenzi wa uzio wa shule hiyo, kwa kuwa ni njia mojawapo ya kuunga mkono juhudi za serikali za uboreshaji wa elimu.

Naye Tekra Mushi, alisema kuwa wazo la bodi ni la muhimu katika ustawi wa elimu shuleni hapo na linatakiwa kuungwa mkono kwa lengo la kuboresha mazingira rafiki ya wanafunzi kujisomea bila kuwa na usumbufu.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (katikati), akionyeshwa eneo wanalotumia kuchota maji na mkazi wa eneo la kihistoria la Mikindani, Said Halfani, katika kisima cha asili cha Haikata kilichopo tangu mwaka 1545, ambapo hadi sasa kinatumiwa na wakazi wa mji wa kihistoria wa Mikindani katika ziara yake eneo hilo mkoani Mtwara juzi. **PICHA: WMU**

# Wafanyabiashara wanawake wapata viongozi wapya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHEMBA ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Mkoa wa Dodoma, imepata viongozi wapya watakaoongoza kwa kipindi cha miaka mitatu.

Uchaguzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki, ambapo Grace Onea alichaguliwa kuwa mwenyekiti huku nafasi ya mwenyekiti msaidizi ikishikwa na Joanita Kahangwa.

Akizungumza na wafanyabiashara hao, mwenyekiti huyo mpya aliwataka wanachama kuwa na mshikamano ili chama kisonge mbele.

Naye Katibu wa Chemba hiyo, Neema Msina, aliwataka wanawake wafanyabiashara kutumia fursa zilizopo kujiinua kiuchumi.

Kadhalika, Mkurugenzi wa TWCC, Kibibi Jafari, alisema Mkoa wa Dodoma umepata sura mpya katika uongozi na kuwataka kusaidia kuinua uchumi wa wanawake.

Awali, akifungua mkutano huo wa uchaguzi, Katibu Tawala mkoa wa Dodoma, Kessy Maduka alisema TWCC inahitaji watu wenye weledi katika uongozi na uendeshaji wa biashara na kutumia vizuri fursa zinazowazunguka.

Alisema mkoa wa Dodoma umepewa heshima kubwa kuwa makao makuu ya nchi na serikali na upendeleo huo umetoa fursa na maendeleo ya kasi ya ukuaji na utoaji huduma mbalimbali.

"Mjadili suala la ubora na usafi wa bidhaa ukiamsha uchumi wa wanawake unajenga taifa imara na kuwa na mipango inayotekelezeka," alisema.

Aliwataka kufanyia kazi changamoto zao wakiwa ndani ya chama ili biashara zao zisimame.

Alisema wanawake wamekuwa katika harakati za kujikwamua kwa miaka mingi na juhudi hizo zitatakiwa kuungwa mkono.

Ofisa Maendeleo ya Biashara wa Shirika la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO), Mkoa wa Dodoma, Crispin Kapinga, aliwataka viongozi waliochaguliwa kufanya kazi kwa bidii na kusaidia wanachama wao kupaa kiuchumi.

# Mkoa wa Dodoma wakumbwa uhaba wa damu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKOA wa Dodoma unakabiliwa na upungufu wa damu, ambapo chupa zinazokusanywa kwa mwezi ni kati ya 400 hadi 600, huku mahitaji yakiwa zaidi ya 1500.

Kauli hiyo ilitolewa jana na mratibu wa kitengo cha damu salama mkoani humo, Leah Kitundya baada ya Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiya Kanda ya Dodoma kujitokeza kuchangia damu ikiwa ni maadhimisho ya siku ya mwana aliyeahidiwa (Musleh Maud).

"Bado tunahitaji damu ya kutosha kwa kuwa kwa mwezi tunatakiwa kukusanywa chupa za damu 1,500 hadi 1,600 lakini kwa sasa zinakusanywa chupa 400 hadi 600 tu," alisema.

Aliziomba taasisi mbalimbali kujitokeza kujitolea damu ili kuwezesha kupambana na upungufu huo.

Kwa upande wake, Rais wa jumuiya hiyo, Twaha Nyange, alisema pamoja na kujitolea damu pia jumuiya hiyo imekuwa ikitekeleza mipango mbalimbali ikiwamo ya kueneza elimu ya kidini pamoja na kutoa misaada mbalimbali kwa wana jamii.

"Kutoa damu ni sehemu kamili ya ibada na maandiko, kwetu tunaagiza kutimiza haki za Mungu na kutimiza haki ya viumbe wa Mungu, kwa maana hiyo kujitolea damu ni kutimiza maagizo ya Mungu ya kulinda haki ya kusaidia viumbe vya Mungu," alisema.

Alisema kwa sasa jumuiya imejipanga kwa ajili ya kuanzisha zahanati, wapo katika mchakato wa kubadilisha matumizi ya kiwanja ambacho wamekodishwa.

"Zahanati hiyo ambayo inatarajiwa kujengwa eneo la Area D itakuwa inatoa huduma kwa watu wote bila kujali itikadi za dini, rangi, cheo wa itikadi ya kisiasa na hiyo huduma inalenga kutolewa kwa uweledi ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali za kuhamia Dodoma na kuzingatia kuwa kwa sasa Dodoma ni makao makuu," alieleza Nyange.

Naye Shehe wa Msikiti wa Jumuiya hiyo, Khawaja Muzafar, alisema kitendo cha kujitolea damu ni dalili kubwa ya upendo na umoja wa kweli usiokuwa na ubaguzi wa aina yoyote.





## Serikali yatangaza vita na wafanya-biashara 'matapeli'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachukuwa hatua kali kwa mfanyabiashara yeyote atakayeingiza bidhaa zisizokuwa na kiwango kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Aliyasema hayo huko katika Bandari ya Malindi mjini Zanzibar alipofika kuangalia zoezi la kuhamisha tani 520 za sukari kwenda kuangamizwa kwenye mashimo ya mchango katika kijiji cha Zingwezingwe baada ya kugundulika kukosa kiwango kwa matumizi ya binadamu.

Alisema kuwa serikali iko makini kulinda afya za wananchi wake, hivyo haitakubali kuingizwa bidhaa yoyote isiyofaa kwa matumizi ya wananchi ili kuwaepusha madhara ambayo yanaweza kutokea.

Aidha, alisema ulinzi mkali wa vikosi vya ulinzi na usalama umeandaliwa kwa ajili ya kusimamia sukari hiyo ili kuhakikisha hakuna mtu atakayefanya mbinu ya kuipata mpaka zoezi zima la kuiangamiza limalizike.

Aliwataka wafanyabiashara kuendesha biashara zao kwa njia za halali na kuacha tabia ya kununua bidhaa za gharama nafuu bila ya kuangali ubora wake kwa lengo la kutafuta faida kubwa.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Chakula na Dawa, Dk. Khamis Ali Omar, alisema makontena 20 ya sukari isiyo na kiwango yenye uzito wa tani 520 ya Kampuni ya Rashid Ali Trader yaliingizwa Zanzibar mwaka jana kwa awamu mbili na alipewa tahadhari kuhusu tatizo la sukari hiyo alipoingiza kwa mara ya kwanza, lakini aliendelea kuiingiza.

Alisema baada ya sukari hiyo kufanyiwa uchunguzi ilionekana haina kiwango na kuchukuwa hatua za kisheria ili isiweze kufika kwa wananchi kwa matumizi mbalimbali.

Alisema baada ya kugundulika kasoro hiyo, mmiliki huyo alishauriwa kuirejesha ilikotoka ama kuiteketeza lakini mashauri yote mawili aliyakataa.

Zoezi la kuiteketeza sukari hiyo limeongozwa na maofisa wa Bodi ya Chakula na Dawa Zanzibar na kuvishirikisha vikosi vya ulinzi na usalama na wafanyakazi wa kitengo cha mazingira Zanzibar.

# Wanafunzi, walimu wajisaidia porini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

**Baada ya serikali kuanza kuchukua hatua kuanzia Machi na Novemba mwaka 2017, baadhi ya watu walianza kulalamika kuwa serikali inachukua mchanga wao.**

WANAFUNZI na walimu wa Shule ya Msingi Tumbatu visiwani Zanzibar, wanalazimika kujisaidia baharini na porini kutokana na ukosefu wa huduma ya vyoo katika eneo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Suleiman Khamis Sheha, alisema kuwa kukosekana kwa huduma hiyo kumesababisha wananfunzi na walimu kujisaidia baharini au porini.

Alisema kuwa vyoo vilivyopo ni vibovu na havifai kabisa kutumika, hivyo ukosefu huo wa vyoo unapunguza hamasa kwa wanafunzi katika kupata elimu.

Alieleza kuwa ni hatari zaidi kwa watoto wa kike, kwa kuwa kwenda kujisaidia msituni wapo katika hatari ya kuweza kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

"Vyoo vilivyopo ni vibovu kwa kuwa vilijengwa baada ya mapinduzi wakati ilipofunguliwa shule hii na aliyeifungua ni Rais wa kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume mwaka 1973, hadi leo havijafanyiwa matengenezo," alisema.

Aidha, alisema Mamlaka ya Maji Zanzibar Zawa pia ilijenga vyoo vingine shuleni hapo, lakini vimeshindwa kutumika kwa sababu ujenzi wake haukuwa katika kiwango bora.

Alieleza kuwa shule hiyo ina wanafunzi 1733, hivyo kitendo cha kujisaidia porini kunaweza kukasababisha mlipuko wa maradhi mbalimbali ikiwamo kipindupindu.

Alieleza pia licha ya kwamba hakuna huduma ya vyoo, lakini huduma ya majisafi na salama pia haipatikani shuleni hapo, hivyo wanafunzi wanapoenda kujisaidia porini hulazimika kujisafisha kwa kutumia majani.

Mwalimu mkuu huyo aliiomba serikali kuharakisha ujenzi wa vyoo kwa sababu huduma hiyo ni muhimu kwa ajili ya kukinga afya za wanafunzi shuleni hapo.

Kwa upande wao wanafunzi wa kike wa shule hiyo walieleza kuwa inakuwa vigumu wanapokuwa katika siku zao za hedhi kutokana na kukosekana kwa huduma ya vyoo na maji.

Walieleza kuwa wanapoenda kujisaidia porini hukutana na wanyama wakali na wakati mwingine hufukuzwa na ng'ombe.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Tumbatu, Suleiman Khamis, akionyesha moja kati ya jengo la choo ambacho hakitumiki kutokana na kuchakaa hali inayosababisha kutokuwa na huduma ya vyoo shuleni hapo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wabunge watoro majimboni wamulikwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Juma Abdullah Mabodi, amekemea kitendo cha baadhi ya wabunge na wawakilishi kushindwa kufika majimboni.

Alisema kitendo hicho ni cha kidhalimu kisichokubalika na wapigakura pamoja na CCM.

Aliyasema hayo wakati akifungua mkutano mkuu wa CCM wa Jimbo la Mahonda ulioelezea utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa Mwakilishi na Mbunge wa Jimbo hilo katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2019, uliofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa CCM huko Mahonda Kaskazini Unguja.

Mabodi alisema kwamba tabia hiyo ya utoro majimboni kwa baadhi ya wabunge na wawakilishi ambayo kwa kiasi kikubwa hubebwa na mizozano inayosababishwa na makundi ya wanasiasa hao haitavumiliwa tena na CCM.

Alisema ipo timu ya CCM iliyoteuliwa kufuatilia utendaji wa chama katika ngazi mbalimbali kuanzia matawi, majimbo hadi mikoa na kubaini baadhi ya changamoto zinazosababishwa na baadhi ya viongozi ambazo iwapo zitaachiwa kuendelea zinaweza kupunguza nguvu za chama kiutekelezaji.

Naibu Katibu Mkuu huyo wa CCM aliupongeza uongozi wa Jimbo la Mahonda kwa kuibua miradi muhimu ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wao na kuitekeleza kwa mafanikio makubwa licha ya changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wake. Dk. Abdullah Mabodi aliuomba uongozi wa jimbo hilo kuendelea kuwa darasa kwa majimbo mengine yasiyofikia kiwango chao cha utekelezaji wa majukumu waliyojipangia ikiwamo utekelezaji wa ilani ya CCM.

Akiwasilisha utekelezaji wa ilani ya CCM katika Jimbo la Mahonda kuanzia mwaka 2016 hadi 2019, Mwakilishi wa Jimbo hilo, Balozi Seif Ali Iddi, alisema amekuwa mtu mwenye furaha kutokana na ushirikiano anaoendelea kuupata katika kuwatumikia wananchi.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa ilani ya CCM 2016 hadi 2019, Jimbo la Mahonda limefanikiwa kusimamia sekta za afya, huduma za maji, umeme, elimu, kilimo, barabara, michezo, vikundi vya wajasiriamali pamoja na kuimarisha kazi na shughuli za kisiasa za chama tawala.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Mahonda, Bahati Abeid Nassir, alisema tatizo la huduma za majisafi na salama lilikuwa sugu, lakini kutokana na jitihada kubwa zilizochukuliwa na uongozi kwa kushirikiana na wananchi changamoto hiyo imepunguwa kwa asilimia kubwa.

# Rubani wa Makamu Rais Kenya afa ajali ya chopa

**NAIROBI,** Kenya

JESHI la Polisi nchini Kenya limesema rubani wa Naibu Rais, Willium Ruto, Mario Magonga, amefariki baada ya helikopta aliyokuwamo kuanguka.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa ndege hiyo ilianguka siku ya Jumapili majira ya saa mbili usiku katika eneo la Turkana, chanzo cha ajali hiyo bado hakijajulikana.

Imeelezwa kuwa Kapteni Magonga amefariki pamoja na abiria wengine wanne waliokuwano ndani ya ndege hiyo.

Polisi walieleza kuwa helikopta hiyo ilianguka katika eneo la Labolo kisiwa chenye milima ya Volcano katikati ya ziwa Turkana-Central Island National Park kaskazini magharibi mwa Kenya.

"Taarifa zilizoko zinaashiria kwamba ndege mbili zilitua mapema katika kambi ya Lobolo katika kisiwa hicho kilichopo kwenye mbuga ya kitaifa, hata hivyo moja ndiyo ilifanikiwa kutua salama katika eneo hilo," ilieleza taarifa iliyotolewa na idara ya polisi.

Kutokea kwa ajali hiyo, vikosi vya usalama vimetumwa katika eneo hilo ili kusaidia kwenye jitihada za kuondosha miili na masalio ya ndege hiyo.

Magonga alikuwa rubani wa Naibu Rais wa Kenya, Willium Ruto na aliwahi kuwa rubani katika Jeshi la Kenya. Ni mzawa wa Nyamataro, kusini magharibi mwa Kenya.

Baba yake ni mwanajeshi mstaafu aitwaye Brigedia Magonga, aliwahi kuwa rubani mkuu wa helikopta za kampuni ya KIDL inayotoa huduma za usafiri binafsi katika eneo lote la Afrika Mashariki.

Pia, alikuwa mkufunzi aliyehitimu wa helikopta, alipata mafunzo kutoka kikosi cha ulinzi Kenya (KDF), ana uzoefu wa kuendesha ndege kwa zaidi ya saa 5500 kwenye ndege za injini moja na injini zaidi ya moja. **BBC**



Polisi Algeria wakiwatawanya waandamanaji wanaompinga Rais wa nchi hiyo, Abdelaziz Bouteflika, kuwania tena nafasi ya urais. **PICHA: REUTERS**

# Rwanda yawapiga 'stop' raia wake kwenda Uganda

**KIGALI,** Rwanda

SERIKALI ya Rwanda imewasihi wananchi wake kusitisha safari za kwenda nchini Uganda baada ya kuishutumu nchi hiyo kuwanyanyasa raia wake wanaoishi ama kutembelea nchini humo.

Pia, Uganda imeishutumu Rwanda kufunga mipaka baina ya nchi hizo mbili, lakini Rwanda imekanusha na kusema mipaka iko wazi.

Mwishoni mwa wiki mamlaka ya mapato ya Rwanda iliamrisha maroli ya mizigo kutotumia tena mpaka wa Gatuna kwa madai ya shughuli za ujenzi wa kituo kimoja cha mpakani baina yake na Uganda.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Mamlaka ya Mapato ya Rwanda (RRA) malori yaliombwa kutumia mpaka wa pili wa Kagitumba kaskazini mwa Rwanda.

Hata hivyo, watumiaji wa mipaka hiyo miwili hupendelea kuitumia njia ya mpaka wa Gatuna kwa kuwa ni rahisi na fupi kuliko ya mpaka wa Kagitumba.

Rwanda inaishutumu Uganda kuwanyanyasa Wanyarwanda wanaoishi ama kufanyia biashara nchini Uganda, pia kuunga mkono makundi ya waasi hususani kundi la Rwanda National Congres linaloongozwa na mkuu wa zamani wa majeshi, Jenerali Kayumba Nyamwasa aliyeko uhamishoni nchini Afrika Kusini.

Kadhalika, Uganda inaishutumu Rwanda kwa vitendo vya kijasusi kwenye ardhi yake, huku ikiwashuku baadhi ya raia wa Rwanda kuhusika na vitendo hivyo.

Ni eneo ambalo huruhusu kupita kwa bidhaa kutoka mji mkuu wa Uganda Kampala, au Mombasa pwani ya Kenya. Wakazi wa eneo hilo wanasema ni kama ghala kwa biashara kutoka maeneo hayo.

Diwani Abel Bizimana alisema: "Hali haijabadilika. Tunaathirika kama viongozi wa kieneo, kama jumuiya ya wafanyabiashara na wateja pia tunaowahudumia."

Kutokana na matatizo ya kibiashara na udhibiti wa watu kutoka na kuingia katika eneo hilo, watu ambao kawaida hufika kupokea bidhaa kutoka mjini na wilaya ya Kisoro kwa sasa hawafiki wakiwamo madereva bodaboda ambao pia wamesitisha shughuli zao.

Alisema siku mbili kuu za soko katika eneo hilo, Jumatatu na Alhamisi, ambazo hushuhudiwa shughuli nyingi za kibiashara, kwa sasa limekuwa kama jangwa.

Kutokana na mgogoro huo, wafanyabiashara wanaobeba mihogo na samaki wanapata hasara eneo la mpakani kwa sababu hakuna wanunuzi.

Wiki iliyopita, msemaji wa serikali ya Uganda, Ofwono Opondo, aliiomba Rwanda kuruhusu wafanyabiashara kuingiza bidhaa ili kuepuka hasara na uhasama zaidi.

Kwa upande wake Waziri wa masuala ya kigeni wa Rwanda, Richard Sezibera, alisema serikali ya Uganda inawadhulumu raia wa Rwanda wanaoishi Uganda.

**BBC**

## Polisi Algeria wapambana na waandamanaji

**ALGIERS,** Algeria

JESHI la Polisi Algeria limewatawanya waandamanaji, wengi wao wakiwa ni wanafunzi kwenye mji mkuu wa Algeria, Algiers, wakati Rais Abdelaziz Bouteflika akijiandaa kuwasilisha nyaraka za kuwa mgombea wa kiti cha urais kwa muhula wa tano.

Wanafunzi hao waliandamana jana katika sehemu kadhaa za mji mkuu wa Algeria, Algiers kupinga jitihada za Rais Abdelaziz Bouteflika mwenye umri wa miaka 82 kugombea muhula wa tano katika uchaguzi ujao utakaofanyika Aprili 18.

Bouteflika alipanga kujiandikisha rasmi kuwa mgombea wa kiti cha urais kwa kuwasilisha nyaraka zake kwa tume ya uchaguzi.

Katika mji mkuu Algiers, mamia ya wanafunzi walikusanyika katika chuo kikuu jijini Algiers na kuimba nyimbo za kuupinga mpango wa Rais Bouteflika wa kutaka achaguliwe tena ili ahudumu muhula wa tano kama Rais wa Algeria.

Taarifa kutoka Algeria zinaeleza kuwa polisi walizuia waandamanaji kutoka kwenye chuo hicho.

Hata hivyo, wanafunzi wengine waliweza kupenya vizuizi vya polisi na kushiriki kwenye maandamano kuelekea katika ofisi za Baraza la Katiba, halmashauri inayoshughulikia nyaraka za wagombea katika uchaguzi huo.

Waandamanaji hao walisikika wakipaza sauti wakiitaka halmashauri hiyo isikubali kupokea nyaraka za ushiriki za Rais Bouteflika.

Mamia ya maofisa wa polisi na wanajeshi wametawanywa kwenye mji mkuu wa Algeria na kwenye maeneo muhimu.

Maofisa hao wa usalama wameyazingira majengo ya ofisi za umma pamoja na kushika doria katika barabara kuu mjini Algiers.

Bouteflika ambaye afya yake imeendelea kudhoofika tangu alipopatwa na kiharusi mwaka 2013, alitarajiwa kuwasilisha nyaraka zake jana ambayo ni siku ya mwisho kwa wagombea kujisajili kabla ya uchaguzi wa rais utakaofanyika mwezi ujao.

Maandamano makubwa ya umma yamezuka nchini Algeria tangu Bouteflika alipotangaza mwezi uliopita nia yake ya kuwania muhula wa tano kwenye uchaguzi huo.

Baadhi ya vyama vya upinzani nchini Algeria vimesema vitasusia uchaguzi huo kupinga hatua ya kiongozi huyo kutaka kuchaguliwa tena kwa muhula wa miaka mitano.

**DW**

# Operesheni uvuvi haramu sasa EAC nzima

**Na Mwandishi Maalum,** ARUSHA

NCHI wanachama wa Jumuiya ya Mashariki (EAC), zimetiliana saini makubalino kuendesha operesheni ya pamoja ya kudhibiti uvuvi haramu kwenye Ziwa Victoria.

Hatua hiyo ni mkakati wa nchi hizo za Kenya, Uganda na Tanzania kulinda rasilimali hizo ziwe endelevu na zitumike kukuza uchumi wa wananchi wa mataifa hayo.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika mkutano wa mawaziri sekta za uvuvi zinazozungukwa na Ziwa Victoria uliofanyika makao makuu ya EAC jijini Arusha Tanzania.

Makamu Mwenyekiti wa Mawaziri wa Sekta za Uvuvi zinazozunguka Ziwa Victoria, Luhaga Mpina, alisema uamuzi uliofanywa na mawaziri hao, utawezesha kuongezeka kwa samaki na mazao yake kwenye Ziwa Victoria, hatua ambayo itachochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa wananchi wanaozunguka ziwa hilo.

Alisema wananchi wa Afrika Mashariki wanaozungukwa na Ziwa Victoria walikuwa wanalazimika kuagiza samaki kutoka nchi ambazo hazina hata maziwa, licha ya ziwa hilo kuwa na uwezo wa kulisha bara zima la Afrika kama likitunzwa vizuri.

Alisema samaki wachanga waliokuwa ziwani chini ya sentimeta 50, walikuwa asilimia 96.3, lakini kutokana na jitihada zilizofanywa za kudhibiti uvuvi haramu, vifaranga vimepungua hadi kufikia asilimia 62.8, kiwango ambacho kinakubalika kwa vifaranga kuwapo majini.

Pia samaki wanaoruhusiwa kati ya sentimeta 50 hadi 80 waliokuwa wamebaki majini, walikuwa asilimia 3.3 tu lakini baada ya kazi ya mwaka mmoja, wameongezeka hadi kufikia asilimia 32.

"Pongezi hizi ninazozitoa kwa nchi wanachama ni za kweli na uhakika, ndiyo maana kwa moyo mmoja nawapongeza sana Uganda kwa kazi nzuri, nawapongeza Tanzania kwa kazi pamoja Kenya kwa hatua wanazochukua, najua mwaka mwingine tukija kupimwa, ziwa letu litakuwa limeondoa kabisa zana haramu," Mpina alisema.

Mpina pia alizipongeza Taasisi za Utafiti za Kenya, Uganda na Tanzania kwa umakini na umahiri wa kukusanya taarifa za kitafiti ili kuzisaidia nchi wanachama kupanga mipango yake ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

"Leo tumefanya maamuzi makubwa ya kupanga mipango ya kufanya operesheni ya pamoja ili kuwa na uelewa wa pamoja na kupanga mipango ya pamoja ya namna ya kulitunza ziwa letu na kupambana na uvuvi haramu pamoja na biashara haramu ya mazao ya uvuvi," alisema.

Mpina aliongeza kuwa nchi hizo zimekubaliana ziwe zimelipa madeni yote kufikia Juni mwaka huu ili kuwezesha Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (LVFO) kutekeleza mipango yake kwa wakati.

Waziri wa Kilimo, Wanyama na Uvuvi wa Uganda, Vincent Ssempijja, alisema nchi yake tayari ilishaanza kuchukua hatua za kupambana na uvuvi haramu katika Ziwa Victoria na makubaliano hayo mapya yatawezesha kuimarisha ulinzi wa rasilimali hizo za uvuvi katika ziwa hilo.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Umwagiliaji wa Kenya, Prof. Micheni Ntiba, alisema kuwa katika kuunga mkono vita dhidi ya uvuvi haramu, Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alizindua Kikosi cha Polisi Maji kitakachotumika kudhibiti uvuvi haramu.



Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Athumani Kihamia, akikabidhi cheti kwa mmoja wa wahitimu wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari Tusiime kwenye mahafali iliyofanyika mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa shule hiyo, Emil Rugambwa na kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo, Dk. John Mbogoma. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Madaktari nchini watakiwa kufuata maadili ya taaluma yao

**Na Beatrice Shayo**

MGANGA Mkuu wa Serikali, Profesa Mohamed Bakari, amewataka madaktari nchini kuzingatia taaluma yao kwa weledi na kufuata maadili.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya siku ya madaktari, alisema mambo hayo mawili ni muhimu katika taaluma yao na endapo watazingatia wataheshimika.

"Nataka madaktari wazingatie mambo mawili kufanya kazi kwa kufuata weledi wa madakati na kufuata maadili ya kazi yao kama watazingatia hayo basi watakuwa wametimiza wajibu wao katika kuhudumia jamii," alisema Bakari.

Alisema serikali inatambua mchango mkubwa wa madaktari, hivyo ingependaza kuona madaktari wanajikita katika utendeji wao wa kazi katika kuhakikisha wanamjali mgonjwa kwa kumpatia huduma nzuri.

Aidha, alisema anatambua kuna changamoto ya rasilimali watu katika sekta ya afya ambao ni upungufu wa asilimia 47 pamoja na madaktari inapotokea fursa wanaajiriwa.

Bakari alisema serikali itaendelea kushirikiana na Chama cha Madaktari ili kupokea ushauri na maoni ikiwa ni kuipeleka sekta ya afya mbali zaidi katika huduma bora. Alisema serikali inajitahidi kufanya mapinduzi katika sekta ya afya katika kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma bora pindi wanapofikishwa katika vituo vya afya.

Naye Rais wa Chama cha Madaktari nchini (MAT), Dk. Elisha Osati, alisema maadhimisho ya siku ya madaktari nchini yanawafanya wajitathimini wapo wapi na wanakoelekea katika utendaji wao wa kazi. Alisema changamoto iliyopo ni rasilimali fedha kwa kuwa kwenye bajeti bado hawajafikia asilimia 15 iliyopangwa kwenye sekta ya afya.

Dk. Osati alisema kuna madaktari wengi ambao wamefuzu na wengine walikwenda kujiongezea elimu na mpaka sasa hawajapandishwa madaraja yao na kuiomba serikali iliangalie suala hilo pamoja na kuboresha mishahara yao.

# Mkurugenzi OBC asomewa mashtaka uhujumu uchumi

INATOKA UK 2

makosa hayo kinyume cha Sheria ya Utakatishaji Fedha kifungu cha 12 (c) na 13(1)(a) ya Sheria ya Utakatishaji Fedha Haramu na. 12 ya mwaka 2006.

Alidai kuwa Aprili 3, 2018 katika ofisi za Forodha za Holili zilizoko mkoani Kilimanjaro, alificha jina la mmiliki wa kampuni ya OBC na kutoa gari namba T.141 DNM aina ya Man Truck kwa jina lingine.

Alidai pia katika shtaka lingine la utakatishaji fedha haramu, Mollel akiwa katika kituo cha Forodha cha Holili, alitoa gari namba T.150 DNM aina ya Mercedes Benz kwa jina la kampuni ya OBC wakati gari hilo halikuwa mali ya kampuni hiyo.

Aidha, Tibabyakomya alitaja mashataka mengine yanayomkabili mtuhumiwa huyo kuwa ni ya kuisababishia hasara serikali kwa kushirikiana na OBC kati ya Januari, 2010 na Aprili, 2018, katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha kwa kutoa taarifa za uongo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kinyume cha vifungu vya sheria namba 57(1)(1) na 60(2)(3) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi (2002) na kuisababisha hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 2.86.

Pia alitaja mashtaka matatu ya kukwepa kulipa kodi kwamba Februari 18, 2017, akiwa jijini Dar es Salaam, aliandaa taarifa ya uongo na kuipeleka TRA ikionyesha magari mawili aina ya Nisani Patrol yenye chasis namba JN-8FY1NY3EX002626 na Mercedes Benz yenye namba WDCYR48F78X173956 yamelipiwa kodi na kuisababishia harasa serikali ya Sh. milioni 199.37.

Katika shtaka la kukwepa kodi, Mollel anadaiwa kati ya Julai, 2016 na Februari, 2017 akiwa jijini Dar es Salaam huku akijua ni kinyume cha sheria, aliandaa taarifa za uongo huku ikionyesha namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) Na. 106105774 na TIN Na.101873307 kuwa amelipa kodi ya magari mawili aina ya Land Cruiser Pick-up yenye chasis namba JTELB71J707112476 na Ford Ranger yenye chasis namba MN-CLS32958W735840 na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 111.38.

Tibabyakomya alitaja shtaka la tatu la kukwepa kulipa kodi kuwa alifanya kati ya Mei 25, 2013 na Februari, 2015 kwamba akiwa jijini Dar es Salaam, aliandaa taarifa za uongo huku ikionyesha TIN namba 106105774 na TIN namba 101873307 kuwa amelipa kodi ya magari sita ambayo ni Land Cruiser Pickup yenye chasis namba JTFLU73J3B4515463, JFL-LU73J2B4515292, JTFHX02P7B0060649 na gari aina ya Nissan Patrol zenye chasis namba JN8FY15Y27X560695, JN8FY15Y27X557203 na JNF8FY15Y27557682 na kuisababishia hasara serikali ya Sh. milioni 299.57.

Wakili huyo wa serikali aliendelea kudai kuwa mshtakiwa pia anakabiliwa na makosa mawili ya kughushi nyaraka, kinyume cha vifungu vya sheria namba 333 (a), 335 na 337 vya Kanuni ya Adhabu (2002).

Alidai kuwa katika madai hayo, kati ya Septemba 10, 2017 na Aprili 7, 2018, katika eneo lisilojulikana ndani ya jiji la Arusha akiwa na nia ovu, aliandaa ankara namba 9091 ikionyesha kuwa OBC imeagiza gari aina ya Mercedes Benz yenye chasis namba WDB 62433615367735 kutoka kampuni ya magari ya Everest (FZD) ya Dubai kwa gharama ya Dola za Kimarekani 12,800 jambo ambalo si kweli.

Pia alidai kuwa kati ya Septemba 15, 2017 na Aprili 7, 2018 katika eneo lisilojulikana ndani ya jiji la Arusha, Mollel aliandaa ankara ya kughushi yenye namba 9092 ya tarehe hiyo ikionyesha OBC imeagiza gari aina ya Man Truck yenye chasis namba WMA 5500231W007547 kutoka kampuni ya magari ya Everest ya Dubai kwa gharama za dola za Kimarekani 12,000.

Katika shtaka lingine lilimuhusu Mollel na kampuni ya OBC kwamba kati ya Julai, 2011 na Julai, 2015 katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro waliandaa nyaraka za uongo na kupeleka TRA zikionyesha kwamba wameingiza magari 31 kwa dharura aina ya Nisan Patrol Station Wagon 20, Toyota Land Cruser Pickup tano, Chevrolet Pickup Double tatu, GMC Yukon moja, Lexus Station Wagon moja, Toyota Van mbili na Mercedes Benz, Caravan Truck moja na kuisababishia hasara serikali ya zaidi ya Sh. bilioni 2.25.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo Mollel hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na Hakimu Niku aliahirisha hadi Machi 18, mwaka huu, itakapotajwa tena na kuamuru mshtakiwa kupelekwa mahabusu katika Gereza Kuu la Kisongo.

Awali kabla ya kusomwa kwa mashtaka hayo yaliibuka malumbano ya kisheria, baada ya Wakili wa Utetezi, Method Kimomogolo, kuiomba mahakama kuahirisha kesi hiyo kwa dakika 15 ili apate nafasi ya kupitia hati ya mashtaka ili kujiridhisha kama ni sahihi au inahitaji marekebisho.

Hata hivyo, Tibabyakomya alipinga hoja hiyo kwa madai kuwa si utaratibu kwa wakili wa utetezi kushauri chochote wakati mashtaka hayo hayajasomwa mbele ya mahakama na mahakama hiyo haina mamlaka yoyote ya kuhoji chochote katika kesi hiyo.

Baada ya maelezo hayo hakimu Niku alitupilia mbali hoja za upande wa utetezi na kuamuru mtuhumiwa kusomewa mashtaka yote 10 yanayomkabili.

Mollel alikamatwa na kushikiliwa na Takukuru Februari 21 usiku, mwaka huu na kushikiliwa hadi jana alipofikishwa mahakamani.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MASHAMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja kilichopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani,eneo la Sanzale "B" lenye Sq.meters 3920 linauzwa. Eneo hilo limepimwa na lina hati ya umiliki. Linafaa kwa shughuli za kibiashara, kujenga kituo cha kuuzia mafuta nk. Kwa maelezo zaidi piga simu Na.0715 263 683/0784 263 683.

### MAGARI/VIPULI

**LEYLAND DAF ZINAUZWA**, DAF TANKI YA MAJI LITA 10,000, DIESEL CC 5880. DAF PICK UP DIESEL CC 4200 TANI 4.5. MAGARI YAPO KWENYE HALI NZURI ZOTE ZINATEMBEA. MAWASILIANO: 0657 370655 DAR ES SALAAM.

### MCHANGANYIKO

**PATA RAMANI ZA MAJENGO MBAL**imbali kama vile ramani za nyumba,shule na kadhalika.Mawasiliano;0744113969


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### CHETI KIMEPOTEA



**GRACIA AMANI LUSASI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1638-0007** kilichotolewa na MTERA DAM SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **URP/RB/6897/2018**

115092102

Kuku Nzito Ltd.

P.O BOX.764
MOSHI

### REQUEST FOR WIDE LOAD PERMIT

We would like to transport a: Truck with lowbed loaded EXCAVATOR

*From ⟶ KIA JUNCTION-MOSHI KILIMANJARO*
*To ⟶ SANYA JUU-MOSHI KILIMANJARO*
*On ⟶ 5/3/2019*

***All the particulars of the combination as per below:***

| | |
|---|---|
| Registration number of prime mover: | T 724 BDR |
| Registration number of trailer: | RAMADHAN S. MBOGO |
| Vehicle tire configuration: | 1.2.2.2.2.2 |
| Length: | 19.90 m. |
| Width: | 3.10 m. |
| Height: | 4.40 m. |
| Escort Vehicle | T648 AKA |

115093202

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE LAND ACT, 1999**
**(NO. 4 OF 1999)**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**

**DATE: 29/01/2019**
**REF No. KUTC/LO/66552/6**
**APPLICANT: REHEMA RUMONGE**
**REGISTERED OWNER: REHEMA RUMONGE**
**LAND:**

**PLOT No: 73 BLOCK: A LOCATION: GUNGU**
Take Notice that Original Letter of Offer of the Land described above is said to be lost and I intend to issue a Certified True Copy of the Original Letter of Offer in lieu thereof unless causes to the contrary is shown within one month from the date of this publication.

The original Letter of Offer if found, should be delivered to the office of Municipal Director of P.O. Box 44 Kigoma.

215092302


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la The Guardian*

*Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,*

*au piga simu: 0767 223311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MORATA amwaga sifa baada ya kufunga

**MADRID,** Hispania

ALVARA Morata amewasifia wachezaji wenzake wa timu yake mpya ya Atletico Madrid kwa kumsaidia kujiimarisha yeye mwenye baada ya kuelezea kuwa msimu wake wa pili kule Chelsea ulikuwa mgumu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alirudi nyumbani kwake wakati wa dirisha dogo la usajili kwa mkopo wa miezi 18, na baada ya kufunga mabao mawili dhidi ya Real Sociedad Jumapili, sasa ana mabao matatu katika mechi zake sita alizoichezea klabu hiyo.

Akizungumzia mabao yake ambayo yaliisaidia Atletico kuibuka na ushindi wa 2-0 kwenye La Liga, Morata alichukua nafasi kwa kuwashukuru wachezaji wenzake kwa kuweza kumsaidia kuimarika kipaji chake baada ya kutoka England.

Ameiambia beIN Sports: “Mara zote washambuliaji huwa wanahukumiwa kutokana na mabao yao, lakini kwa yote mimi nina furaha kubwa kuzoeana na wachezaji wenzangu.

“Nina furaha kwa sababu nilikuwa na kipindi kigumu katika misimu ya hivi karibuni. Wachezaji wenzangu wamenifanya nizoee haraka hapa.”

Ushindi huo wa wikendi uliisaidia Atletico kubakia nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi, wakipitwa pointi saba na vinara Barcelona, Morata alidai kwamba Los Rojiblancos hao wanahitaji kushinda mechi zote 12 zilizobaki ili kuweza kuweka matumaini hai ya kutwaa taji hilo.

Aliongeza: “Kwa sasa tunatakiwa kuangalia kwenye matokeo yetu tu, na hapo ndipo tutaweza kuweka hai matumaini yetu ya kushinda.

“Tuna nafasi ya kuendelea kushinda katika kila mchezo na tutapigana hadi dakika ya mwisho ya msimu huu.”



# KANE aitaka Spurs kuimarika zaidi

**LONDON,** England

HARRY Kane amewataka Tottenham kujifunza kukabiliana na presha kubwa katika kila mechi ili kuwa kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu England.

“Kwa sasa sisi tunatakiwa kupunguza presha na kuhakikisha kwamba tunacheza kwa ajili ya kushinda kila mchezo,” alisema nahodha huyo wa timu ya Taifa ya England, ambaye alifunga bao la kusawazisha katika sare ya 1-1 dhidi ya Arsenal.

“Kwa sasa kila mchezo unakuja mbele yetu tunatakiwa kucheza kwa kujituma na kujiimarisha zaidi, ili tuweze kuwa tofauti.

“Hatujafanya mambo kama haya katika miaka ya hivi karibuni na hatujafanya hivyo katika wiki hii na itakuwa tofauti.

“Hii ndiyo nafasi nzuri zaidi ya kujiimarisha na tunahitaji kujaribu kucheza na kujiimarisha zaidi.”

Spurs leo Jumanne itacheza na Borussia Dortmund kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, huku wakiwa wanaongoza katika mchezo wa kwanza wakiwa na ushindi wa mabao 3-0.

Kane, ambaye amefunga mabao 22 msimu huu, alisema kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu huu ni jambo walilolipa kipaumbele kikubwa.

“Kuifunga Dortmund itaonyesha kuwa tunazidi kukua kwenye michuano ya Ulaya na kuwa timu kubwa,” alisema.

“Ni muhimu kufuzu kwa hatua ya robo fainali baada ya kufikia hatua kama hii.”



# ROBERTSON: Presha kubwa ipo kwa City

**LIVERPOOL,** England

BEKI wa Liverpool, Andy Robertson, anaamini presha yote ipo kwa Manchester City kwenye mbio zao za ubingwa wa Ligi Kuu ya hapa England msimu huu.

Mabingwa hao watetezi wa ligi hiyo wamerudi kileleni mwa msimamo baada ya Liverpool kutoka sare ya bila kufungana na Everton kwenye mchezo wa ‘dabi’ ya Merseyside Jumapili, na kuifanya City kuongoza kwa pointi moja zaidi.

Huku kukiwa kumebakiwa na mechi tisa ligi hiyo kufikia tamati, vijana hao wa Jurgen Klopp watatakiwa kuwapiku City, ambao waliwafunga Bournemouth bao 1-0 Jumamosi.

Robertson anahisi kwamba kikosi cha Pep Guardiola kipo kwenye presha, huku Liverpool ikiwania kutwaa taji lake la kwanza la Ligi Kuu tangu mwaka 1990.

“Tumekuwa na nafasi na presha yote ipo kwa Manchester City,” alisema akiiambia BBC.

“Tutapigana hadi dakika ya mwisho kabisa ya msimu huu. Presha imekuwa dhidi ya City kwa sababu wanatarajia kutetea taji lake.

“Everton wanafikiri kwamba wametuzuia kushinda taji la ligi. Inaonyesha jinsi tunavyofanya vizuri na wanataka kutusimamisha.”

Liverpool imeshinda mechi zake mbili zilizopita kati ya tano za Ligi Kuu na watakuwa nyumbani Jumapili dhidi ya Burnley.

# GUARDIOLA: Hatutajuta tukikosa ubingwa EPL

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola (pichani chini), amesisitiza wachezaji wa Manchester City hawatatakiwa kujutia kama watazidiwa kete na Liverpool kutwaa taji la Ligi Kuu ya England.

Guardiola anaamini kwamba timu yake inacheza soka bora zaidi kuliko msimu uliopita waliovunja rekodi na kulitwaa taji hilo.

City wanapewa nafasi kubwa zaidi ya kulitwaa taji hilo msimu huu baada ya Jumapili kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Bournemouth na sare ya Liverpool ya kutokufungana dhidi ya Everton ikawafanya wawapite pointi moja vijana hao wa Jurgen Klopp, huku wakiwa wamebakiwa na mechi tisa.

"Kwa namna tunavyocheza, tunacheza zaidi, bora zaidi kuliko msimu uliopita," alisema Guardiola.

"Kila mmoja anajua kwamba nini tunachofanya, kila mmoja anamsaidia mwenzake. Na ikitokea, tunaweza kushindana na kama tukishindwa, tunapoteza, lakini tukipoteza hatutakiwi kujutia.

Guardiola aliuelezea ushindi wa Manchester City wa 1-0 dhidi ya Bournemouth kuwa walicheza kwa kiwango cha juu.

"Najua jambo la msingi ni kuhakikisha wanashinda kila mchezo, lakini tukifungwa sio tatizo.

"Lakini ni vigumu kuhisi kwamba wachezaji wangu walicheza vizuri na naamini wataendelea kucheza kwa kiwango cha juu."

City msimu uliopita iliweka rekodi ya kutwaa taji la Ligi Kuu msimu uliopita kwa kufikisha pointi 100 na kufunga mabao 106.





# KLOPP

## alaumu upepo sare dhidi ya Everton

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amelaumu uelekeo wa upepo kuwa ndio sababu ya timu yake kuwa na kiwango kibovu wakati 'Wekundu' hao wakibanwa mbavu na kutoka sare ya bila kufungana na Everton katika dimba la Goodison Park juzi, Jumapili.

Kushindwa kupata pointi zote tatu kunamaanisha kwamba Liverpool imeshindwa kuipiku Manchester City kileleni mwa Ligi Kuu, baada ya City kuichapa Bournemouth bao 1-0 Jumamosi.

Akizungumza na Sky Sports, Klopp alisema: "Ni sawa, mchezo ulikuwa mgumu kwa sababu tofauti.

"Najua watu hawapendi wakati nikisema hivyo, lakini upepo ulikuwa unakuja kutoka pande zote na haukuwa msaada kwenye soka.

"Ulikuwa mchezo ambao ni mgumu kuutawala na tulikuwa na nafasi tatu au nne kupitia Mohamed Salah na Fabinho, na sikumbuki kama walikuwa na nafasi nyingine. Ni 0-0 na tuliendeleza rekodi ya kutopoteza mchezo, sio kitu tulichokitaka.

"Salah anafanya vizuri hadi sasa, tulikuwa na nafasi, lakini hatukuweza kuzitumia. Mchezo wetu ulikuwa mgumu.

"Ilikuwa ni muhimu kupata pointi kwenye mchezo wa leo (juzi) na vijana walionekana kuwa na hamasa kubwa."

Liverpool sasa imepitwa pointi moja na Manchester City, huku kukiwa kumebakiwa na mechi tisa za Ligi Kuu ya England kumalizika.

# Balotelli aomba simu ajipige 'selfie' dimbani

**PARIS,** Ufaransa

MCHEZAJI mtukutu, Mario Balotelli, ameibua mjadala kwenye mitandao ya kijamii pamoja na vyombo vya habari, baada ya kufunga bao na kuomba simu na kupiga 'selfie'.

Baada ya kufunga katika mchezo huo ambapo alifunga bao la kwanza dakika ya 12, aliamua kwenda kwa mpiga picha aliyekuwa karibu na golini na kuomba simu halafu akawaita wachezaji wenzake na kuamua wajipige picha ya pamoja.

Raia huyo wa Italia anajulikana kwa aina tofauti za ushangiliaji wake kuwa sio za kawaida.

Akiwa na klabu ya Manchester alipofunga bao alivua jezi na kuonesha maandishi yaliyoandikwa 'kwanini mara zote mimi tu'.

Marseille walishinda mchezo huo kwa mabao 2-0, huku mchezaji wa zamani wa Newcastle, Florian Thauvin akifunga bao la pili kwa mkwaju wa penalti.



## KWA UFUPI

### PENALT YA KANE SIYO- REFA

STRAIKA wa Tottenham, Harry Kane, 25, asingeweza kuzawadiwa penalti dhidi ya mahasimu wao wa kaskazini mwa London, Arsenal kama teknolojia ya msaada wa video kwa refa (VAR) ingetumika, amesema refa wa zamani wa Ligi Kuu England, Peter Walton. **(Times)**

### SUAREZ AMVUTIA GOMEZ LIVER

LIVERPOOL inamtaka straika wa Celta Vigo na Uruguay, Maxi Gomez, 22, kwa dili la pauni milioni 35 baada ya mshambuliaji wao wa zamani Luis Suarez kutoa maoni yake kuhusu raia mwenza huyo. **(Sun)**

### TIERNEY KUMRITHI NACHO ARSENAL

ARSENAL inavutiwa na nyota wa kimataifa wa Argentina na Ajax, Nicolas Tagliafico, 26, ama beki wa Celtic na Scotland, Kieran Tierney, 21, kama mbadala wa beki wa kushoto Mhispania Nacho Monreal, 33, endapo atajiunga na Barcelona. **(Mirror)**

### ISCO AZIVUTA UNITED, LIVER

MANCHESTER United na Liverpool zipo tayari kumsajili kiungo wa Real Madrid, Mhispania Isco, 26. **(Tuttosport - in Italian)**

### LIVER, BAYERN KWA WERNER

LIVERPOOL bado inahusishwa na kumsajili straika Mjerumani wa RB Leipzig, Timo Werner, 22, licha ya Bayern Munich kuvutiwa naye. **(Liverpool Echo)**

### INTER YAMFUATA DARMIAN

INTER Milan inavutiwa kumsajili beki wa kulia wa Manchester United, Mtaliano Matteo Darmian, 29, kwa pauni milioni 9.5. **(Football Italia)**

### ARSENAL YAMRUDIA CARRASCO

ARSENAL inataka kumsajili winga Mbelgiji Yannick ~~Carrasco, 25, kutoka kwa klabu ya China, Dalian Yifang,~~ baada ya kushindwa kumpata kwa mkopo katika dirisha la Januari. **(Express)**

### BALE ASHUSHWA BEI MADRID

THAMANI ya uhamisho wa mshambuliaji wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale, 29, imeshuka hadi pauni milioni 63, hiyo ikiwa na maana Real Madrid inajiandaa kupata hasara ya pauni milioni 30 kama itamuuza mchezaji huyo majira haya ya joto. **(Mirror)**

### PENGO LA COUTINHO BADO LIVER

LIVERPOOL bado inatafuta mbadala wa kiungo mshambuliaji, Mbrazil Philippe Coutinho, 26, ambaye alijiunga na Barcelona Januari mwaka jana, amesema beki wa zamani wa miamba hiyo ya Anfield, Jamie Carragher. **(Mirror)**

### WAJERUMANI WAVAMIA EPL

MASHUSHU kutoka timu za Ujerumani wametua England kutazama shule za vipaji za Arsenal na Chelsea, lengo likiwa ni kutafuta winga mpya kama "Jadon Sancho, 18" ambaye aliondoka Manchester City na kujiunga na Borussia Dortmund mwaka 2017. **(Sun)**

### ARSENAL WAMTAKA CHAMBERS

MASHABIKI wa Arsenal wameongeza presha katika klabu hiyo wakitaka Calum Chambers, 24, kurejeshwa klabuni kutoka Fulham anakocheza kwa mkopo. **(Express)**

### LESCOTT AMBAKISHA FODEN CITY

BEKI wa zamani wa Manchester City, Joleon Lescott, hadhani kama kiungo wa England U-21, Phil Foden, 18, anaweza kuondoka Etihad kwa mkopo. **(Manchester Evening News)**

### SOUTHGATE AMTAFAKARI TOWNSEND

KOCHA wa England, Gareth Southgate anafikiria kumuita winga wa Crystal Palace, Andros Townsend, 27, kuitumikia timu ya Taifa mwezi huu. **(Mirror)**

### RODGERS AMTAKA MCGINN

KOCHA mpya wa Leicester City, Brendan Rodgers, anataka kumsajili kiungo wa Aston Villa, Mscotland John McGinn, 24. **(Birmingham Mail)**

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR AIFUNGULIA MLANGO REAL MADRID

**RIO,** Brazil

HUKU akieleza kuwa mshambuliaji mwenza wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, atakuwa mmoja wa wachezaji bora katika historia ya soka duniani, nyota wa kimataifa wa Brazil, Neymar amekiri kuwa anavutiwa na Real Madrid na ni matarajio yake kuichezea, lakini akasisitiza hahitaji kuharakisha kuondoka kwa mabingwa hao wa Ufaransa.

Neymar alikuwa mchezaji ghali zaidi duniani baada ya kujiunga na PSG akitokea Barcelona kwa euro milioni 222 Agosti 2017.

Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye kwa sasa yupo chumba cha majeruhi akiuguza majeraha ya mguu baada ya kuumia Januari mwaka huu, hajawa sehemu ya mafanikio kwa miamba hiyo ya Ufaransa kushinda mataji yote manne ya ndani katika msimu wake kwa kwanza.

Lakini licha ya kauli ya mara kwa mara kutoka kwa Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi, kwamba Neymar hauzwi, haiwezi kumaliza kabisa tetesi za straika huyo kuhusishwa na kujiunga na miamba hiyo ya La Liga, Madrid, klabu ambayo nyota huyo anaitamani.

"Real Madrid ni moja ya klabu kubwa zaidi duniani," Neymar aliiambia Redio ya Brazil, Globo. "Mchezaji yeyote ambaye Real Madrid inamtaka atavutiwa kucheza pale.

"Sisemi kuwa ninakwenda kucheza Madrid. Ninajisikia furaha sana hapa... [lakini] kwa baadaye hakuna ajuaye.

"Kila mmoja anajua tayari nimetoa ndoto yangu, kucheza Barcelona. Hii mara zote ilikuwa ndoto yangu, kitu fulani ambacho ninazungumza kuhusu tangu nilipokuwa mdogo na nimeweza kukamilisha. Nimekamilika.

"Kwa sasa ni mwenye furaha [hapa PSG]. Ninazungumzia leo, macho yangu yapo Paris tu. Sivutiwi na mwingine yeyote, sitaki kuondoka Paris, lakini mambo yanatokea haraka sana.

"Miezi mitatu kutoka sasa, hakuna yeyote ajuaye nini kinaweza kutokea. Kama rais atakuja kuzungumza na wewe, kitu ambacho mchezaji hana njia nyingine ya kufanya. Kadri kama atakavyotaka ubaki klabuni, anapaswa kuondoka.

"Sizungumzi kuhusu suala langu, ni wazi ninatoa mfano namna maisha ya mchezaji yalivyo ya kasi, hayatarajiwi kabisa, mambo yanatokea kwa sekunde.

"Lakini ni wazi Real Madrid ni timu kubwa, moja kati ya klabu kubwa kabisa duniani. Ninaheshima sana [kwa klabu]. Lakini ninajiona mwenyewe nikiwa Paris leo."

Neymar ambaye alicheza La Liga kwa misimu minne akiwa na Barca, huku akitwaa ubingwa huo mara mbili na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara moja, akimzungumzia Mbappe alisema amewika tangu alipojiunga na PSG mwaka 2017 - wakati huu akiwa ameshacheka na nyavu mara 50 katika mashindano yote kufuatia mabao mawili aliyofunga Jumamosi wakati wakitokea nyuma na kushinda 2-1 kwenye mechi ya Ligue 1 dhidi ya Caen.

Kwa umri wake wa miaka 20, Mbappe tayari ana medali ya Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa na zingine mbili za Ligue 1, pamoja na ya Coupe de France na ile ya Coupe de la Ligue.

"Uhusiano nilionao naye ni mzuri, wa ndani na nje ya uwanja," Neymar aliiambia Globo.

"Ninamuita 'Golden Boy'. Ni kijana ambaye kwake ninaupendo wa kipekee sana, ambaye atakuwa mchezaji bora katika historia ya soka, na nitajaribu kumsaidia katika njia sahihi iwezekanavyo."

HABARI MICHEZO

# BABU MOLLEL WA TIGO KILI HALF-MARATHON APEWA MJENGO

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BAADA ya kuwa taswira halisi katika mbio za 'Tigo Kili Half-Marathon' kwa miaka minne mfululizo, hatimaye Kampuni ya Mawasiliano ya tiGO imemkabidhi Babu Joram Mollel (93), nyumba ya vyumba 17 ikiwa na samani zote za ndani.

Kwa miaka minne mfululizo iliyopita, Tigo imekuwa mlezi na mdhamini mkuu wa mbio za kilometa 21 zinazojulikana kama 'Tigo Kili Half-Marathon', ambapo Babu Mollel amekuwa akiwavutia watu wengi kumshangilia wakati akishiriki.

Mwaka jana, Tigo ilishirikiana na Babu Mollel katika kampeni maalum ya Tigo Kili Half-Marathon iliyoitwa 'Tisha Kama Babu'.

Kampeni hiyo ilikuwa na lengo kubwa la kuhamasisha Watanzania kuweza kuishi maisha ya kujali afya zao. Wakati huo huo, Tigo pia ilisitisha rasmi namba ya mbio aliyokuwa akiitumia Babu Mollel '1040' na alitambuliwa rasmi kama mwanamichezo wa heshima 'Hall of Fame'.

**Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika juzi eneo la Mushono nje kidogo ya Jiji la Arusha, ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari pamoja na Ofisa Biashara Mkuu, Tarik Boudiaf.**

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Karikari alisema nyumba hiyo ilinunuliwa na kukarabatiwa kisha kumkabidhi Babu Mollel kama ishara ya shukrani kwa kujituma na umahiri wake katika riadha.

"Babu Mollel amekuwa akishiriki mashindano ya Tigo Kili Half Marathon kwa miaka mingi sasa. Tulipoona hali ya makazi yake si nzuri Tigo tuliona njia sahihi ni kuwezesha apate nyumba yake mwenyewe," alisema Karikari na kuongeza:

"Katika nyumba yake hii ya hapa Mushono, Babu atakuwa anakaa katika nyumba ya kisasa, iliyo tayari na samani pamoja na vyombo vyote muhimu vya ndani. Nyumba hii pia imeunganishwa na umeme na maji. Hati ya nyumba pia ipo kwa jina lake, hivyo yeye ndiye mmiliki halali wa nyumba hii.

"Babu Mollel ni taswira halisi ya uanamichezo, ujasiri na jitihada. Yeye ni mfano aliye hai kwamba kama binadamu tunaweza tukafanikiwa katika lolote lile ambalo tukiamua kulifanya kwa dhati, na kuondoa dhana nzima kwamba umri au changamoto zingine zozote zinaweza zikawa sababu ya kutokufanikiwa kwetu."

Aidan Komba, ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, alisema nyumba hiyo imegawanyika sehemu tatu na kuongeza kuwa Babu Mollel atakaa katika nyumba moja na mbili zilizobaki ataweza kuzipangisha na kujipatia kipato cha kuendeshea maisha yake ya kila siku.

"Napenda kuwashukuru sana Tigo kwa zawadi hii ya kipekee. Maneno yangu hayawezi kuelezea furaha niliyonayo. Kitendo hiki kina maana kubwa sana kwangu. Maana hivi sasa ninaweza nikasema sasa nina mahali pakuita kwangu," alisema Babu Mollel.

Ushiriki wa Babu Mollel katika mashindano ya Kili Marathon ni wa zaidi ya miaka 15, ambapo amekuwa akiwavutia watu wengi kumshangilia wakati akishiriki mbio za marathon, pamoja na uzee wake.



Mkurugenzi Mtendaji wa tiGO Tanzania, Simon Karikari (wa pili kulia), akikata utepe kuashiria kumkabidhi rasmi nyumba mpya Mzee Joram Mollel mwenye umri wa miaka 93 (katikati), ambaye amekuwa akishiriki mbio za tiGO Kili Half Marathon kwa miaka minne mfululizo, hafla hiyo ilifanyika eneo la Mushono jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Wengine ni mwanawe Elibarik Mollel (wa pili kushoto), Ofisa Biashara Mkuu wa tiGO, Tarik Boudiaf (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Kanda ya Kaskazini, Aidan Komba. **MPIGAPICHA WETU**

## Sababu Stand United kupokea kipigo Simba

**Na Faustine Feliciane,** SHINYANGA

STAND United juzi ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani wa CCM Kambarage mjini hapa, ilikumbana na kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Simba ukiwa ni mwendelezo wa michezo mbalimbali ya ligi hiyo inayotoa mwalikishi wa Tanzania Bara katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo dharau kutoka kwa Kocha Mkuu wa Stand United, Athumani Bilalo 'Bilo' inaweza kuwa moja ya sababu ya timu yake kupokea kipigo hicho, kufuatia kabla ya mchezo huo, kusema Simba ni timu ya kawaida na kikosi chake kina uwezo wa kuibuka na ushindi katika mchezo huo.

Kauli hiyo ya Bilo ilionyesha wazi kuwa kikosi chake kitaingia kuikabili Simba bila kuwaheshimu mabingwa hao watetezi, jambo ambalo liliwagharimu katika mechi hiyo.

Kocha huyo alianza mchezo huo kwa kujaza viungo wengi katikati, huku akicheza soka la kushambulia na wachezaji 'kufunguka' muda mwingi wa mchezo.

Hilo lilikuwa kosa kubwa kwa Stand ambapo Simba waliamua kutumia mtindo wa pasi ndefu kutoka kwa mabeki wake na kusababisha mashambulizi mbele na mfumo huo ulionekana kuwasumbua Stand United hasa kutokana na kasi ya mshambuliaji, John Bocco ambaye alikuwa "mwiba mchungu" kwa wenyeji hao kuanzia kipindi cha kwanza.

Akizungumza na gazeti hili, Bilo alisema wamepoteza mchezo huo kutokana na makosa ya kimchezo uwanjani huku akikiri Simba wana kikosi kizuri.

"Tulikuwa na malengo mazuri ya ushindi, na hata mchezo tuliuanza kwa kasi na wachezaji walijitahidi, lakini wenzetu walikuwa wajanja zaidi," alisema kocha huyo.

Aidha, Kocha wa Simba, Patrick Aussems, alisema waliwaheshimu wapinzani wao kwa sababu ni timu nzuri na walikuwa kwenye uwanja wao wa nyumbani, hivyo walicheza kwa tahadhari zaidi.

"Nawapongeza wachezaji wangu kwa kazi nzuri, wamefuata maelekezo yangu na kufanikiwa kupata ushindi huu muhimu wa ugenini, Stand United walicheza vizuri, lakini nafikiri tulikuwa bora zaidi hasa kimbinu," alisema Aussems.

Mabao yote ya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara katika mchezo huo yalifungwa katika kipindi cha pili na nahodha wa timu hiyo, Bocco.

Kikosi cha Simba leo kinatarajia kuelekea Algeria kwa ajili ya kuwakabili wenyeji wao JS Saoura katika mechi ya Kundi D ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Jang'ombe Boys waukataa ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Jang'ombe Boys inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar umesema timu yao haina nafasi ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu kutokana na kufanya vibaya katika mzunguko wa kwanza.

Ligi Kuu Zanzibar inashirikisha timu 19 na bingwa wake hupata nafasi ya kuwakilisha visiwa hivyo katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Jang'ombe Boys, Ali Othman, alisema timu yake haikufanya vema katika hatua ya kwanza ya ligi hali ambao imewaondoa kwenye mbio za kutwaa taji hilo.

Othman alisema wanachoangalia sasa ni kupambana ili kuhakikisha timu yao inamaliza ligi ikiwa katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Timu yangu haina tena nafasi ya kutwaa ubingwa, sasa hivi mipango yetu ni kupambana kuhakikisha tunamaliza ligi tukiwa kwenye nafasi nzuri, ikiwezekana hata kumaliza katika "Tano Bora", sisi hapa kwetu itakuwa ni ushindi tosha," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa anakiamini kikosi chake kitafanya "maajabu" kutokana na anavyokiona tangu kuanza kwa mzunguko wa lala salama wa ligi hiyo baada ya wachezaji wao kujituma na kufuata ratiba ya mazoezi kikamilifu.

Jang'ombe Boys yenye pointi 33 iko katika nafasi ya 10 katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kucheza mechi 22.

# Michezo

Jumanne Machi 5, 2019

Nipashe


## Neymar aifungulia mlango Madrid



HABARI UK. 30

**MEDALI...**




Wafanyakazi wa Benki ya NMB wakifurahia medali walizokabidhiwa baada ya kumaliza mbio za Kimataifa za Kilimanjaro Marathon; tiGO Half- Marathon [Kilomita 21], zilizofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# YANGA NA DUA LA MWEWE SIMBA SC

●●● Zahera asema presha kwa Msimbazi na wataangukia pua wasipotarajia huku...

**Na Somoe Ng'itu**

ILE methali ya "dua la mwewe halimpati kuku", imeanza kujitokeza kwa miamba ya soka nchini Simba na Yanga kuelekea mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ambazo zimeanza kufikia patamu sasa.

Hali hiyo inatokana na wakati huu Simba ikiomba kumaliza viporo vyake vyote kwa ushindi ili kukaa kileleni mwa ligi hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, ameelekeza maombi yake katika kuwaombea mabingwa hao watetezi, wateleze na hatimaye kikosi chake kiweze kuendelea kuongoza ligi ili kutwaa ubingwa.

Yanga ambayo imecheza mechi 26 hadi sasa, inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 64 wakati mabingwa watetezi, Simba wenye alama 51 wameshuka dimbani mara 20.

Hata hivyo, Simba ambayo imekuwa na mechi nyingi za viporo kutokana na kubanwa na michezo ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na leo ikitarajia kuondoka nchini kuelekea Algeria kuwafuata wenyeji wao, JS Saoura, endapo itashinda mechi zake sita ilizo nazo mkononi, itafikisha pointi 69, tano mbele ya Yanga.

Akizungumza na Nipashe jana, Zahera, alisema hababaishwi na kasi waliyonayo watani zao, Simba katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo iko katika mzunguko wa lala salama, kwa sababu anaamini mabingwa hao watetezi 'watasimamishwa" na timu wasiyoitarajia.

Zahera alisema mechi zilizobakia ni nyingi na lolote linaweza kutokea kwa Simba ambayo imeshinda mechi zake tano mfululizo za ligi hiyo.

Kocha huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, alisema anakiamini kikosi chake na anaamini makosa ambayo walifanya katika mechi zilizopita kwa kukubali kufungwa ikiwamo dhidi ya Simba, hayatajirudia tena kutokana na kujipanga kutwaa ubingwa huo.

"Malengo yetu ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA, hatuna wasiwasi, tunaendelea kujipanga, wenzetu wao wamebakiza ligi tu, sababu hiyo watakuwa na presha zaidi na lolote linaweza kutokea huko mbele," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa katika kikosi chake wachezaji wote ni muhimu na anaamini wanapopata ushindi au kupoteza pointi hiyo inatokana na juhudi za pamoja.

"Tuko kitimu, hakuna mchezaji muhimu kuliko mwenzake, hata kikosi changu hukipanga kulingana na mazingira niliyonayo au aina ya mpinzani ninayekutana naye, ligi bado ina ushindani na sisi hatutaki kuwapisha pale kileleni," aliongeza Zahera.

Tayari Yanga imesharejea jijini Dar es Salaam ikitokea Mwanza ambapo ilifanikiwa kuifunga Alliance FC bao 1-0, shukrani kwa mshambuliaji wake wa kimataifa kutoka Burundi, Amissi Tambwe ambaye alitokea benchi na kupachika bao hilo pekee katika mchezo huo.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara watashuka tena dimbani Jumamosi kuwakabiri KMC kwenye Uwanja wa Taifa jijini, wakati wapinzani wao, Simba siku hiyo watakuwa na kibarua kigumu ugenini, Algeria kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya JS Saoura.

## Aussems afunguka kuifumua JS Saoura

**Na Faustine Feliciane,** SHINYANGA

BAADA ya ushindi wa mabao 2-0 katika mchezo wa juzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Stand United kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mjini hapa, Kocha wa Simba amesema sasa wanaelekeza nguvu zao kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya JS Saoura ya Algeria.

Simba itawakabili JS Saoura ugenini nchini Algeria Jumamosi Machi 9, katika mechi ya Kundi D itakayochezwa majira ya saa 4:00 usiku.

Akizungumza na Nipashe juzi, Aussems, alisema sasa anaanza maandalizi ya mchezo huo huku akiweka wazi kuwa leo wanaenda Algeria na mawazo ya ushindi na si kuomba kupata sare.

"Kwa nini tufikirie sare badala ya ushindi..., tunaeda Algeria kupambana kupata ushindi ambao kwa kweli utakuwa umetuweka karibu kabisa na kufuzu hatua ya robo fainali ambayo ndio malengo yetu kwa sasa," alisema Aussems.

Alisema michezo ya karibu ya Ligi Kuu waliyocheza imewapa maandalizi mazuri ingawa walikuwa na changamoto ya ratiba ya ligi.

"Tumecheza michezo mingi kwa muda mfupi, lakini hatukuwa na namna, tumebakiwa na siku chache kabla ya kucheza huko Algeria, hizi siku tutazitumia kufanya maandalizi ya mwisho," alisema.

Alisema timu yake ina nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo kama watafanya vizuri kwenye michezo yao miwili iliyobakia.

Baada ya mchezo dhidi ya JS Saoura ugenini, Simba itarejea nyumbani kujiandaa na mchezo wa mwisho dhidi ya AS Vita utakaochezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Machi 19, mwaka huu.

Aidha,Aussems pia alimzungumzia beki wake 'kiraka', Erasto Nyoni ambaye alikuwa majeruhi kwa muda mrefu, akikiri kuwa sasa amepona na ameanza kushiriki mazoezi ya nguvu na wenzake, lakini hatomtumia kwenye mchezo dhidi ya JS Saoura.

"Nyoni bado hana 'match fitness', taratibu ameanza kurejea katika hiyo ari, ni wazi hawezi kucheza dhidi ya JS Saoura, lakini ana nafasi kwenye mchezo dhidi ya AS Vita hapa nyumbani, alisema Aussems.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >